# Nipashe

Jumamosi Januari 26, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579824

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



## IPP kujenga kiwanda cha kubangua korosho

UKURASA 3




UKURASA 13

# Unyama wa kutisha

**MAJAMBAZI** wavamia gesti, wabaka wahudumu na kupora fedha... ni baada ya kuwapa vinywaji na biskuti zenye...*Endelea ukurasa wa 2*



Baadhi ya akina mama wakichagua korosho zilizomwagwa chini katika ghala la chama cha msingi cha Tuaminiane (Amcos), lililopo wilayani Masasi mkoani Mtwara jana. Zoezi hilo limekuja baada ya kudaiwa kuwa hazina ubora wa daraja la kwanza jambo ambalo limepingwa na wakulima kwenye korosho hizo. Katika ghala la Tuaminiane zaidi ya tani 100 zimekwama kupelekwa ghala kuu. **PICHA: HAMISI NASRI**

## Sababu Tido kukwepa jela

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**WAKOSA HUDUMA YA VYOO DENI LA UMEME MIL. 3.6/-**

SHULE ya Msingi Tandale Magharibi, Dar es Salaam, imejikuta katika wakati mgumu na wanafunzi wake kushindwa...

## KUMRADHI

KATIKA gazeti letu toleo Na. 057918 la Januari 19, 2019 tulichapicha habari yenye kichwa "RC aingilia kati DED, DSO kupigana ofisini". Habari hiyo ilimtaja DSO (ofisa) Usalama wa Taifa wa Wilaya ya Mwanga) kwa majina yake mawili.

Baada ya kurejea Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1996, tumejiridhisha kwamba haikuwa sahihi na ni makosa kumtaja kwa majina ofisa huyo.

Kutokana na kosa hilo, tunaomba radhi kwa wasomaji na jamii kwa ujumla kwa kuwa haikuwa dhamira yetu kufanya hivyo. – **MHARIRI.**

## Mama amchoma mtoto mikono

UKURASA 10

**MICHEZO** SIMBA, MBAO NAO WACHEMKA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Majambazi wafanya unyama wa kutisha

**Na Ibrahim Yassin,** MBEYA

WATU wanaodaiwa kuwa majambazi, wamevamia nyumba ya kulala wageni ya Malema Lodge katika mtaa wa Sinde jijini Mbeya, inayomilikiwa na Diwani Viti Maalumu (CCM), Mary Malema, kisha kuwabaka wahudumu na mlinzi na hatimaye kupora fedha.

Unyama huo waliufanya usiku wa kuamkia jana baada ya kuwapa ofa ya vinywaji na biskuti zinazodaiwa kuwa na dawa za kulevya.

Shuhuda wa tukio hilo (jina linahifadhiwa), alisema watu watatu waliingia ndani ya baa hiyo wakiwa kama wateja na kuanza kutoa ofa za vinywaji na biskuti na kwamba yeye aliondoka baada ya muda kufika na kwamba alipata taarifa kuwa baada ya kula vitu hivyo, walilala wakiwa hoi.

Alisema baada ya kuzidiwa kutokana na kulewa, watu hao watatu walianza kuwabaka wanawake hao hata kufikia hatua kuwaingilia kinyume cha maumbile kisha kupora fedha ambazo thamani yake haijafahamika na kwamba asubuhi alipokuwa anapita, aliona msamaria mwema amewabeba na kuwapeleka hospitali akipitia polisi.

Malema, mmiliki wa nyumba hiyo, alisema ilikuwa usiku wa saa tano waliingia watu watatu kama wateja na mlinzi alifunga geti kutokana na muda kuwa ulikwisha, hivyo walianza kunywa pombe na kuwapa ofa wahudumu pamoja na mlinzi ambaye alipewa soda na biskuti.

Alisema baada ya hapo, wahudumu walilala fofofo, ndipo watu hao wakafanya unyama huo na kwamba hajafahamu kama walibakwa au la kwa kuwa bado wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya wakiwa hawajitambuhi wakipumulia mashine.

Malema ambaye pia ni diwani wa viti maalumu katika kata ya Manga, alisema wakati anapita aliona msamaria mwema anawabeba ndipo katika kuchunguza akabaini kuwa vijana wake waliingiliwa na watu hao. Alisema alikwenda polisi akapewa barua kwa ajili ya matibabu.

"Watu hawa kuna uwezekano mkubwa wanafahamika. Wamevamia gesti zenye baa maeneo mbalimbali na hawakamatwi. Polisi walipowaona vijana hawa wakiwa hoi wakasema wamepewa biskuti, wamejuaje?" alihoji na kusema: "Hadi muda huu (akizungumza na mwandishi wa habari hii), hakuna polisi aliyefika kuwaona wala kufuatilia tatizo hili, "alisema Malema.

Alisema alipofika baa alikuta fedha zote zimechukuliwa na zikiwamo pia na za upande wa gesti na kwamba hajajua kiasi cha fedha kwa kuwa hawakufunga hesabu. Aliliomba

INAENDELEA UK 8



Mkurugenzi wa Dr Ntuyavaliwe Foundation, Jaqueline Mengi, akikata utepe kufungua Maktaba mpya katika Shule ya Msingi Tandale Magharibi iliyojengwa na taasisi hiyo jijini Dar es Salaam jana.Wengine ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Doris Msigalo (kushoto) na Mwakilishi wa Afisa Elimu wilaya ya Kinondoni, Grace Mtesigwa. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Sababu Tido kukwepa jela

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imemwachia huru Mkurugenzi Mkuu wa zamani wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Tido Mhando, baada ya kumwona hana hatia dhidi ya madai katika kesi aliyokuwa akishtakiwa.

Tido, ambaye ni mwanahabari nguli aliyewahi kufanya kazi ndani na nje ya nchi, alikuwa akishtakiwa kwa matumizi mabaya ya madaraka na kusababishia serikali hasara ya Sh. 887.1.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, baada ya kusikiliza ushahidi wa mashahidi watano wa Jamhuri na mmoja wa utetezi, ambayo yalishindwa kuthibitisha makosa dhidi yake.

Akitoa uamuzi wa kuachiwa huru kwa Tido, Hakimu Shaidi alisema upande wa Jamhuri ulidai mahakamani kwamba Tido alitia saini na kuingia mkataba wa kuipa zabuni kampuni ya Chanel 2 Group Corporation (BVI) kwa ajili ya kubadilisha mfumo wa matangazo kutoka analogia kwenda digitali.

Akifafanua hukumu hiyo alisema, mshtakiwa alidaiwa kuingia mkataba huo bila baraka za bodi ya TBC na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Hata hivyo, katika utetezi wake, Tido alidai Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kiwete, alimwagiza kulibadilisha shirika liwe na uwezo na sifa ya shirika la taifa.

Kutokana na agizo hilo , Tido alidai kuwa alifanya mabadiliko makubwa na kwamba ingetokea akaongezewa mkataba wa awamu ya pili, alitaka TBC itoe gawio kwa serikali badala ya shirika hilo kupokea ruzuku kutoka serikalini.

Aidha, Tido katika utetezi wake, alidai kuwa mwaka 2012 aliitwa kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na kwamba kampuni ya Chanel 2 ilifungua kesi lakini waliiondoa kwa sababu hakukuwa na mkataba kati yake na kampuni hiyo.

Kutokana na utetezi huo na ushahidi uliotolewa dhidi yake, Hakimu alisema mahakama yake bila kuacha shaka imeona kwamba mshtakiwa hana hatia dhidi ya tuhuma hizo.

"Mahakama hii inakuachia huru, imekuona huna hatia dhidi ya mashtaka yaliyofunguliwa dhidi yako," alisema Hakimu Shaidi.

Kutokana na hukumu huyo, Wakili wa Serikali, Leonard Swai, alidai kuwa upande wa Jamhuri haujaridhika na uamuzi huo, hivyo umeomba nakala ya hukumu kwa ajili ya kukata rufani.

Katika kesi ya msingi, Tido alikuwa anakabiliwa na mashtaka manne ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka.

Ilidaiwa kuwa Juni 16, 2008, akiwa Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), wakati huo akiwa mkurugenzi mkuu wa

INAENDELEA UK 8

# Wakosa huduma ya vyoo deni la umeme mil. 3.6/-

**Na Romana Mallya**

SHULE ya Msingi Tandale Magharibi, jijini Dar es Salaam, imejikuta katika wakati mgumu na wanafunzi wake kushindwa kutumia vyoo vipya vilivyojengwa kutokana na kukosa maji baada ya malimbikizo ya deni la umeme la Sh. milioni 3.6.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo yenye wanafunzi 1,195, Doris Misigaro, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa changamoto hiyo ya deni imesababisha wanafunzi kuendelea kutumia vyoo vya zamani ambavyo si rafiki kwao.

"Fedha ambazo tunapewa kila mwezi na serikali hazihusiani na masuala ya ulipaji umeme na hapa tunatumia maji ya kisima ambayo ili tuyapate tunatakiwa kuyavuta kwa pampu kwa kutumia umeme ambao tumekatiwa kutokana na deni hili la Sh. milioni 3.6," alisema.

Alisema Tanesco waliwaeleza ili kuendelea na huduma hiyo, wanatakiwa kila mwezi kupunguza deni, kitendo ambacho hadi sasa wameshindwa kutekeleza kutokana na ukosefu wa fedha.

Mwalimu mkuu huyo alisema deni hilo la umeme ni la muda mrefu na limewaathiri watoto kwa kushindwa kutumia vyoo vipya ambavyo vimejengwa shuleni hapo na kuachana na vile vya zamani.

Nipashe ilishuhudia vyoo vya wanafunzi na walimu ambavyo vinatumika hivi sasa havipo kwenye hadhi huku vile vipya vimeshindwa kutumika kutokana na kuhitaji maji mara mtu anapomaliza kupata huduma ndani yake.

Alitaja changamoto nyingine shuleni hapo kuwa ni ya uzio na kueleza kuwa shule hiyo iko pembezoni mwa barabara na pindi wanafunzi wanapokuwa darasani wamekuwa wakishindwa kusoma vizuri kutokana na mazungumzo ya wapita njia na kelele za magari.

"Kama unavyoona wakati mwalimu yupo darasani anafundisha mara unasikia 'Juma andazi hili hapa' sasa hapo unaona kabisa namna watoto wanavyovurugwa na mazungumzo ya nje ataangalia nje kuona andazi au kumsikiliza mwalimu," alisema.

Alisema wanaamini shule hiyo ikiwekewa uzio utasaidia kuondokana na changamoto hizo na kuondoa mwingiliano wa wapita njia shuleni hapo.

## HABARI ZA KITAIFA



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akibeba kichanga kilichozaliwa juzi kwenye kituo cha afya Kambarage mjini Shinyanga, na kuagiza serikali ya mkoa huo kupunguza vifo vya uzazi na watoto. **PICHA: MARCO MADUHU**

# IPP kujenga kiwanda cha kubangua korosho

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

KAMPUNI ya IPP Limited inakusudia kujenga kiwanda cha kubangua korosho mkoani Mtwara, ikiwa moja ya kampuni tano zilizoonyesha nia katika uwekezaji huo.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alisema hayo jana ofisini kwake mjini hapa alipozungumza na waandishi wa habari huku akibainisha kuwa IPP ni kampuni pekee ya kizawa inayomilikiwa na mfanyabiashara maarufu, Dk. Reginald Mengi, huku zingine nne zikiwa za kigeni.

Alisema Dk. Mengi, ambaye ni Mwenyekiti Mtendaji wa Kundi la Kampuni za IPP, alitembelea mkoani Mtwara wiki iliyopita kukagua eneo analotarajia kujenga kiwanda hicho katika kijiji cha Hiyari, wilayani Mtwara.

"Mwekezaji mzalendo Reginald Mengi alifika ofisini kwangu na kuwasilisha nia yake ya kujenga kiwanda cha kubangua korosho katika mkoa wangu. Nilimpeleka katika kijiji cha Hiyari eneo ambalo tumelitenga kwa ajili ya viwanda na tayari amechangua eneo alilopendezwa nalo," alisema Byakanwa

"Tunachosubiri ni mwendelezo wa utekelezaji wa nia ya wawekezaji hao ila kwa namna ya kipekee nimpongeze na kumshukuru Mzee Mengi kwa moyo wake wa kizalendo wa kuwekeza nchini kwake kwa ajili ya ustawi wa Watanzania wenzake kwani viwanda hivyo vitatoa ajira kwa Watanzania," aliongeza.

Byakanwa alizitaja kampuni zingine zilizoonyesha nia ya kuwekeza katika viwanda vya ubanguaji wa korosho kuwa ni ni MBR International Trading Company, Safi Group Company, Shafa Investment na Food Source Company Ltd.

Alisema uwekezaji huo ni mwitikio wa serikali wa kuzuia usafirishaji wa korosho ghafi nje ya nchi na kuagiza korosho zote kubanguliwa nchini lakini akasema kwa sasa ni mapema kuelezea uwezo wa viwanda hivyo.

"Kwa sasa tunajitahidi kuhakikisha miundombinu yote muhimu kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda inafika katika eneo la Hiyari. Tumeazimia huduma za uhakika za maji na umeme zisogezwe karibu ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi," alisisitiza.

Mkuu wa Mkoa alibainisha kuwa hadi sasa serikali imekusanya na kuhifadhi katika maghala tani 209,398 za korosho ambazo zinasumbiriwa kubanguliwa na kwamba kujitokeza kwa wawekezaji hao kutafungua

INAENDELEA UK. 8

# Jaji Mkuu atoa neno kesi ya Zitto

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Tanzania imesema haikatai kusajili kesi bali Msajili wa Mahakama Kuu ana mamlaka ya kutokusajili kesi yoyote yenye upungufu wa kisheria ili kuwapunguzia majaji mzigo wa majalada yasiyokidhi kusikilizwa kisheria mbele yao.

Kadhalika imempongeza msajili aliyekataa kuisajili kesi iliyowasilishwa na Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, kwamba haikukidhi vigezo vya kisheria na kwamba wahusika walielekezwa kufanya marekebisho ya kisheria.

Jaji Mkuu, Profesa Ibrahim Juma, alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Wiki ya Sheria na Siku ya Sheria nchini.

Alisema mahakama inafanya shughuli zake kwa uwazi na kwamba mtu ambaye hajaridhika ana haki ya kukata rufani.

"Msajili wa mahakama ni wajibu wake kupokea nyaraka za kufungua kesi zilizokamilika. Wanasiasa hatuwezi kuwazuia kusema, sisi mahakama tunafanya kazi zetu kimyakimya na kwa mujibu wa sheria," alisema.

Jaji Mkuu alisema mhimili wake umepokea malalamiko mengi ya kutupwa kesi kutokana na makosa ya kiufundi lakini Bunge limetunga Sheria ya Mahakimu na Majaji kuangalia kama kuna uwezekano wa kuendelea yakiwamo makosa hayo.

INAENDELEA UK. 8


Tanzania International Container Terminal Services Limited
Container Terminal Building
Dar es Salaam Port
P.O. Box 71442
Dar es Salaam
Tanzania
Tel : (255) 22 2134056
Fax: (255) 22 2134019
www.ticts.net

## TICTS yaweka rekodi mpya, kiwango cha kuhudumia kontena kufikia 592,000 mwaka 2018.

### TICTS yatoa shukrani kwa Serikali, TPA, TRA, wateja na hasa kwa wafanyakazi wa TICTS kwa kufanikisha mafanikio haya makubwa.

Kampuni ya Kimataifa ya kuhudumia shehena ya kontena bandarini (TICTS), ikiwa kama kampuni pekee ya inayotoa huduma kwa shehena ya kontena inayofanya kazi katika bandari kubwa nchini Tanzania imefikia hatua mpya ya mafanikio na kuweka rekodi mpya ya kuhudumia shehena ya kontena 592,000 katika mwaka 2018. Rekodi ya mwisho iliwekwa na kampuni hiyo mwaka 2017 ambapo ilihudumia kontena 501,690. Katika mwaka wa 2018, TICTS pia iliweka rekodi ya mwezi katika mwezi wa Agosti kwa kuweza kuhudumia kontena 54,447 na rekodi ya kontena 31,239 zilihudumiwa katika mageti katika mwezi Machi 2018.

Ongezeko la shehena ya ndani na kwa ajili ya nje ya nchi imeongezeka kwa asilimia 18, zaidi ya mwaka 2017. Mizigo ambayo ni kwa nchi mbalimbali zinazotumia bandari yetu iliongezeka kwa wastani zaidi ya asilimia 38.9 kwa mwaka 2018.Ongezeko la shehena linahitaji ufanisi na uharaka katika utoaji mizigo ili kupunguza muda wa mizigo kukaa bandarini na hivyo kuwezesha TICTS na Bandari kuongeza ufanisi na uwezo wa kuhudumia shehena kubwa zaidi. Kampuni imefanikiwa ukuaji huu licha ya changamoto za mazingira ya kiabiashara kimataifa na katika kanda.

Afisa mkuu Mtendaji, Jared Zerbe alisema, "Msaada na ushirikiano tunaopata kutoka kwa Serikali ya Tanzania, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Mapato (TRA), wafanyakazi wetu, wateja na wadau wanaotumia bandari hii ndio imekuwa chanzo cha ukuaji wa huduma za TICTS katika mwaka 2018. Binafsi, najivunia sana kwa timu yetu nzuri sana ya wafanyakazi wa TICTS ambao wamekuwa wakifanya kazi pamoja vizuri sana wakipambana na changamoto ya kuhudumia ongezeko la shehena."

Kuongeza ufanisi ili kuweza kuhudumia shehena hii inayokua, TICTS itaendelea kufanya kazi na Serikali ya Tanzania, TPA, TRA na wateja na kufanyia kazi changamoto zote zinazoathiri utolewaji haraka wa mizigo katika bandari ya Dar-es-salaam.




**Kuhusu TICTS**

Kampuni ya kimataifa ya kuhudumia shehena ya kontena bandarini (TICTS) inashughulika na huduma kwa shehena za kontena katika bandari ya Dar es Salaam, Tanzania. Ikiwa kama kampuni inayoongoza ya kushughulikia kontena, TICTS imejikita kusonga mbele na kuimarisha wajibu wake kama lango kuu la nchi kuelekea mashariki, kusini na Afrika ya kati.

TICTS ni mwanachama wa Makampuni ya Hutchison Port Holdings , kitengo cha huduma za bandari na nyinginezo husika katika kampuni ya CK Hutchison Holdings Limited (CK Hutchison). Ina mtandao wa operesheni katika bandari 51 katika nchi 26 zilizopo katika mabara ya Asia, Mashariki ya Kati, Afrika, Ulaya, Amerika na Australasia. Kampuni ya Hutchison imepanua biashara zake katika huduma nyingine zinazohusiana na usafirishaji, ikiwa ni pamoja na vituo vya meli za safari za matembezi, operesheni za uwanja wa ndege, vituo vya usambazaji, huduma za reli na vituo vya ukarabati wa meli.

A member of the HPH Group
A Hutchison Whampoa Company

715027302

# Matatani kwa kumweka kinyumba mwanafunzi

**Na Ibrahim Yassin,** KALAMBO

MKAZI wa kijiji cha Kateka, Kalambo mkoani Rukwa, Linus Mayaya (35) ametiwa mbaroni kwa kudaiwa kumbaka mwanafunzi wa darasa la nne kisha kumweka kinyumba.

Linus ameingia kwenye wakati mgumu kutokana na tuhuma hizo baada ya kumfuatilia kwa muda mrefu mwanafunzi huyo huku akimpatia fedha za chipsi na soda ili kuweka mazingira ya kumsogeza karibu ili kutimiza azma yake.

Tukio hilo la kusikitisha na kushangaza jamii, limetokea baada ya mama mzazi wa mwanafunzi huyo, kutoa taarifa polisi kutokana na mtoto wake kuachishwa masomo na kijana huyo kumweka kinyumba akimfanya mke hali akifahamu kuwa anastahili kupata haki yake ya elimu.

Oliver Edita, mama mzazi wa mtoto huyo, alisema baada ya kutomwona mwanawe kwa siku mbili, alimtafuta huku na kule kisha juzi akabaini kuwa amewekwa kinyumba na mtuhumiwa huyo.

Alisema baada ya kugundua hilo, alitoa taarifa kwa serikali ngazi ya tarafa na polisi ambao walimkamata mtuhumiwa akiwa na mwanafunzi ndani mwake.

"Mimi ni masikini lakini najitahidi kuwasomesha watoto wangu nikiwa na ndoto za kuwa waje kuwa viongozi wakubwa wa taifa hili. Kitendo cha baba huyo kumharibia maisha mwanangu kimenisononesha," alisema huku akiomba vyombo husika vichukue hatua dhidi yake.

Endrew Manyema, Ofisa Tarafa wa Matai, licha ya kuthibitisha kuwapo tukio hilo, alisema baada ya kupata taarifa kutoka kwa mama mzazi wa mtoto huyo, alipiga simu polisi ambao nao walifika eneo la tukio na kumkamata mtuhumiwa huyo ambaye kwa sasa bado anaendelea kuhojiwa polisi wilaya.

"Tukio hili limetusikitisha sana. Tumeweka mikakati ya kutoa elimu ngazi za vijiji na kata kwa wazazi ili wajue umuhimu wa kuwalinda na kuwasomesha watoto kwani kuna uwezekano kwa baadhi ya watu vijijini hawajui madhara ya kufanya ngono na watoto ambao pia ni wanafunzi.

George Kyando, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, amethibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kusema jeshi lake limemnasa mtuhumiwa huyo ambaye anaendelea kuhojiwa katika kituo kikuu cha polisi wilaya na atafikishwa mahakamani pindi uchunguzi utakapokamilika.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Taifa, ofisini kwa Waziri Mkuu, Mlimwa jijini Dodoma, jana. Kutoka kushoto ni Makamu wa Rais wa chama hicho, Deus Seif, Mweka Hazina , Abubakar Allawi, Katibu Mkuu, Christopher Banda na wapili kulia ni Rais wa CWT , Leah Ulaya. **PICHA NA OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Taasisi ya Dk. Ntuyabaliwe yazidi kuunga mkono elimu

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Dk. Ntuyabaliwe, imeendelea kumuunga mkono Rais John Magufuli katika sekta ya elimu kwa kukarabati chumba cha maktaba katika Shule ya Msingi Tandale Magharibi, Dar es Salaam na kuweka vitabu mbalimbali.

Akizindua chumba hicho jana, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Jacquiline Mengi, alisema hadi sasa taasisi hiyo imeshakarabati maktaba saba katika shule mbalimbali za msingi na kuziwekea vitabu ili kuwezesha wanafunzi kujisomea.

"Hakuna nchi iliyoendelea duniani bila watu kuelimika, namshukuru Rais Magufuli kwa kuamua kutoa elimu bure kwa watoto ambayo kwa sasa kila mzazi mwenye mtoto aliyefikisha umri wa kwenda shule anampeleka," alisema.

Alisema taasisi hiyo ambayo ilianzishwa kwa lengo la kumuenzi baba yake mzazi, Dk Ntuyabaliwe ambaye kwa sasa ni marehemu, Mei, mwaka jana, ilianzisha shindano la 'Andika Challenge' ambalo mwanafunzi wa shule za msingi wanatakiwa kutunga hadithi yake.

Alisema katika shindano hilo mwanafunzi wa darasa la saba, Nora Komba, katika shule hiyo (wakati huo akiwa darasa la sita), aliibuka mshindi baada ya kutunga hadithi iliyokidhi vigezo vyote vya shindano.

Alisema mwanafunzi huyo alipewa zawadi na kwa utaratibu wa taasisi yake, hukarabati maktaba ya shule ambayo mshindi ametoka na kuiwekea vitabu ambavyo vitawawezesha wanafunzi kupenda kusoma na kujua kuandika.

Jacquiline alisema taasisi yake inahimiza watoto wapende kujisomea kwa sababu huwasaidia kukuza uelewa wao.

"Baba yangu ambaye ni Dk. Ntuyabaliwe alipenda sana kusoma vitabu, nakumbuka wakati nikiwa na umri kama wenu alikuwa akiniambia nisome vitabu, nilikuzwa kwenye utamaduni huo. Ndio maana nimeanzisha taasisi hii ili kumuenzi na kuwezesha watoto kama nyinyi muwe na utamaduni wa kusoma vitabu, hii itawasaidia kujifunza mambo mengi na kupanua uelewa," alisema.

Alisema kwa sasa shindano hilo la 'Andika Challenge' liko mikoani, hivyo mwanafunzi ambaye atatunga hadithi nzuri, atawezesha shule yake kukarabatiwa maktaba na kuwekewa vitabu.

Alisema mbali na zawadi hiyo, wanafunzi hupatiwa madaftari, sare za shule na kufunguliwa akaunti.

Alisema hadithi hizo zilizotungwa na watoto zitapelekwa kwenye maktaba mashuleni ili vizazi vijavyo vije kusoma kile kilichotungwa na Watanzania wenzao.

Jacquiline aliwataka wazazi kuwapeleka watoto wao shule na kuwahimiza kusoma vitabu vikiwamo vya hadithi ili kuongeza maarifa na kukuza uelewa wao.

Pia aliwataka wazazi waliopo mikoani ambako kwa sasa shindano lipo, wawahimize watoto wao kushiriki Andika Challenge.

"Watoto maktaba siyo eneo la kuja kuangalia rangi zilizopakwa, huku mkiingia humu mjisomee vitabu mbalimbali vilivyomo,"alisema.

Mshindi wa shindano hilo la 'Andika Challenge', Nora alisema hadithi yake iliyomuibua mshindi ilikuwa ikisimulia kuhusu mkulima ambaye alikuwa hafuati ushauri ambaye alikuwa analima hadi kipindi cha kiangazi na mazao yakikauka alikuwa akisema

INAENDELEA UK. 8

# Kigwangalla ahamasisha utalii ughaibuni

**Na Mwandishi Wetu,** MADRID

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, ametumia kongamano la 10 la Uwekezaji na Biashara kwa kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya utalii.

Kongamano hilo lilifanyika juzi jijini hapa kwa kuandaliwa na Shirika la Utalii la Umoja wa Mataifa (UNWTO) kwa kushirikiana na Taasisi za Casa Afrika na Taasisi ya Maonesho ya Biashara ya Madrid (IFEMA) kwa kushirikisha nchi mbalimbali duniani.

Katika Kongamano hilo, Waziri Kigwangalla alipata fursa ya kuwa mmoja wa wazungumzaji na kuwahakikishia wawekezaji wenye nia kuwekeza nchini Tanzania na kwamba ni sehemu salama kwa kuzingatia hali ya amani na utulivu iliyopo lakini pia kuna vivutio vingi vya utalii na fursa za kuwekeza.

"Nawakaribisheni nyote, njooni Tanzania muwekeze kutokana na mazingira na miundombinu bora kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya utalii na viwanda," alisema.

Waziri Kigwangalla pia alitumia nafasi hiyo kuutangaza ukanda mpya wa kusini mwa Tanzania ambao umejaliwa kuwa na vivutio vya utalii vya kipekee vinavyopatikana katika hifadhi za taifa ya Ruaha, Mikumi na Pori la Akiba Selous.

Katika hatua nyingine, Waziri Kigwangalla aliwaeleza washiriki hao kuhusu juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali ya Rais John Magufuli kwa kutaja mifano michache kama vile kufufua kampuni ya ndege ya Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya sita na kujenga chanzo kikubwa cha kuzalisha umeme katika mto Rufiji.

Alisema serikali pia inaendelea na mradi wa kisasa wa ujenzi wa njia mpya ya kisasa ya reli na kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo.

Alibainisha kuwa kutokana na juhudi hizo zilizochukuliwa na serikali hiyo, sekta ya utalii itasonga mbele na kurahisisha usafiri kwa watalii na wawekezaji kwa ujumla.

## HABARI KITAIFA

# Waitara ataka uchunguzi Fedha ujenzi wa bweni

**Na George Tarimo,** IRINGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, ameagiza kumsimamisha kazi Mhandisi wa Ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, ili kupisha uchunguzi wa fedha zilizotumika katika ujenzi wa mabweni mawili ya wasichana katika Shule ya Sekondari Isimila.

Waitara alichukua uamuzi huo jana akiwa mkoani Iringa, baada ya kukagua ujenzi wa mabweni hayo yaliyojengwa chini ya kiwango kulinganisha na fedha zilizotumika. Ujenzi huo umegharimu Sh. milioni 184 huku majengo yakiwa hayajamalizika yakiwa yanahitaji fedha zingine ili kukamilika.

Kutokana na hali hiyo, Waitara alionyesha kukerwa na ujenzi huo ambao umetumia fedha za serikali na nguvu za wananchi na umesimama kutokana na kutokamilika.

Alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Robert Masunya, kumsimamisha kazi mhandisi huyo, Nestory Chacha, mpaka uchunguzi utakapofanyika ili hatua za kinidhamu zichukuliwe.

"Naona ninyi mnaichezea serikali, haiwezekani serikali itoe fedha kujenga mabweni ili watoto wetu waepukane na vitendo vya kikatili vikiwamo ubakaji na mimba za utotoni wasome katika mazingira mazuri na hatimaye kufikia ndoto zao. Sasa leo (jana) ninaagiza mhandisi apewe adhabu kali na ifikapo Februari 5, taarifa ya uchunguzi iwe imeshanifikia," alisema.

INAENDELEA UK. 8



Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Adrof Mkenda, akiagana na Balozi wa Ujerumani nchini, Dk, Detlef Waechter baada ya kumaliza mazungumzo yaliyofanyika wizarani, jijini Dar es Salaam jana. Kuhusu kujiandaa kushiriki maonyesho Ujerumani mwezi Machi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Diwani wa CCM atishia kujiuzulu

**Na Gurian Adolf,** MPANDA

DIWANI wa Uwanja wa Ndege katika Manispaa ya Mpanda, Stephano Mwakabafu (CCM), ametishia kujiuzuru udiwani sambamba na kugoma kusoma taarifa ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya kata yake.

Mwakabafu alifikia hatua hiyo kwa kile alichodai kuwa atatekeleza wajibu huo miundombinu ya barabara itakapotengenezwa kwenye kata hiyo.

Tukio la kuweka mgomo kusoma taarifa ya maendeleo ya kata yake lilitokea juzi katika kikao cha pili cha baraza la madiwani la Manispaa hiyo kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Manispaa ya Mpanda.

Kwa mujibu wa kanuni za vikao vya baraza la madiwani, kila diwani anatakiwa kusoma taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo zilizofanyika kwenye kata yake.

Meya wa Manispaa ya Mpanda, Willy Mbogo, ambaye alikua akiongoza kikao hicho, ilipofikia zamu ya kusoma taarifa ya Kata ya Uwanja wa Ndege, alimtaka Mwakabafu kusoma taarifa ya utendaji kazi ya maendeleo ya kata yake ya kipindi cha pili cha kuanzia Oktoba hadi Desemba, mwaka jana.

Baada ya diwani huyo kusimama, kwa mshangao mkubwa, aliwaambia wajumbe wa baraza hilo kuwa hayuko tayari kusoma taarifa za utendaji kazi wa shughuli za maendeleo ya kata hiyo.

Alisema akiwa diwani, anajisikia vibaya kusoma taarifa hiyo wakati kuna wanafunzi wanashindwa kwenda shuleni kwa sababu ya ubovu wa barabara inayounganisha kata hiyo na eneo la Mkumbo, hivyo hayuko tayari kusoma mpaka barabara hiyo itakapotengenezwa.

Diwani huyo alisema hakuchaguliwa na wananchi wa kata hiyo ili kuona wananchi wakiteseka, wakiwamo wanafunzi wanaolazimika kutembea kwenye madimbwi ya maji kipindi hiki cha masika kutokana na miundombinu ya barabara kuwa mibovu.

Alisema amechoka kutukanwa na wananchi wake kutokana na ubovu wa barabara na hakuchaguliwa kuwa diwani kwa ajili ya kutukanywa bali kusimamia maendeleo ya wananchi.

Pia alisisitiza kuwa, yuko tayari hata kujiuzulu udiwani endapo eneo hilo halitatengenezwa na kuwaondolea adha wakazi wa kata hiyo kuliko kuendelea kutukanwa na wapigakura wake.

Msimamo wa diwani Mwakabafu ulimfanya Diwani wa Kasokola, Chrisant Mwanawima, aingilie kati na kumsihi apunguze hasira na kumwomba ampatie ofisa mtendaji wa kata hiyo aisome taarifa hiyo kama hawezi kuisoma.

Naye Diwani wa Mpanda Hotel, Wiliam Liwali, alimwambia diwani huyo aliyegoma kusoma taarifa kuwa kwa umri alio nao yeye anamwona Mwakabafu sawa na mtoto wake, hivyo alimtaka apunguze hasira kwa kuwa jambo hilo analolilalamikia si mara yake ya kwanza na tatizo la barabara hiyo halmashauri inalifahamu.

INAENDELEA UK. 8

# Tusiime yang'ara tena kidato cha nne

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wote 272 wa Shule ya Sekondari ya Tusiime ya Tabata Dar es Salaam, waliofanya mtihani wa kidato cha nne mwaka jana, wamefaulu kwa alama za juu kwenda kidato cha tano.

Kwa mujibu wamatokeo yaliyotangazwa juzi na Baraza la Taifa la Mitihani (Necta), wanafunzi 86 wa shule hiyo wamepata daraja la kwanza na 118 daraja la pili.

Matokeo hayo yanaonyesha kuwa wanafunzi wengine 60 wamepata daraja la tatu na wanafunzi wanane daraja la nne lakini wote wamefanikiwa kupata alama za kuendelea na kidato cha tano.

Mkuu wa Taaluma wa Shule hiyo, John Kishefu, alisema matokeo hayo ni mazuri hasa ikizingatiwa idadi kubwa ya wanafunzi waliokuwa nao ambayo ni kubwa kuliko shule nyingi zilizofanya mtihani huo.

Kishefu alisema miaka yote Tusiime huwa haichagui wanafunzi wa vipaji maalum kama zinavyofanya baadhi ya shule bali huchukua wa aina zote hata wale wenye uwezo mkubwa na mdogo darasani na kuwaandaa vizuri.

"Sisi hatuchagui mwanafunzi, unaweza kukuta amekuja hapa akiwa na uwezo mdogo sana lakini timu mahiri ya walimu waliopo hapa wanamtengeneza hadi anapata daraja la kwanza au la pili hilo ni jambo la kawaida hapa Tusiime," alisema Kishefu

Kishefu alisema matokeo hayo mazuri ni mwendelezo ya matokeo kama hayo kwa shule za Tusiime kuanzia shule ya msingi na kidato cha pili ambapo wamekuwa wakifaulisha kwa alama za juu.

"Matokeo haya yamewafurahisha hata wazazi wengi ambao wamekuwa wakitupigia simu na kutupongeza. Tulikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi lakini tumemudu kuwapeleka kidato cha tano wote hii si kazi rahisi," alisema Kishefu.

Akizungumzia matokeo hayo, Mkurugenzi wa

Shule, Albert Katagira, alisema matokeo hayo mazuri yanatokana na dhamira waliyonayo kama taasisi kuhakikisha vijana wa Tanzania wanapata elimu bora katika mazingira yaliyo safi na salama.

"Napenda kuwathibitishia wadau wote wa elimu kuwa shule za Tusiime zimejipanga kuendelea kutoa elimu bora hapa nchini na hivyo tumewekeza vya kutosha katika miundombinu, zana za kufundishia, motisha kwa wafanyakazi na ushirikiano mzuri baina yetu, serikali na wazazi, haya yote kwa pamoja ndiyo yametufikisha kwenye matokeo haya," alisema.


## KUMBUKUMBU



115027202

**DR. TUKUNDONDA S. KYANDO**

Masaa, siku, wiki, miezi, miaka na hatimaye leo umetimiza miaka mitano (5), toka ulipotutoka siku ile ya tarehe 25-1-2014.

Ulipotuacha katika majonzi mazito ya kutokuamini Kama kweli umeondoka, lakini kwetu ni kama jana tu maana Upendo na Busara zako kwetu bado upo pamoja nasi na utaendelea kuwa nasi maisha yetu yote.

Unakumbukwa sana na Mke wako Yokebeth Kyando, Watoto wako, Wajukuu zako, Ndugu jamaa na marafiki.

*Mwenyezi akupatie pumziko la Amani. Ameni*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkanganyiko ratiba Ligi Kuu usiharibu ushindani

**MAPEMA** wiki hii Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi (TPLB) ilitoa ratiba ya Ligi Kuu Bara kwa kuweka tarehe ya mechi ambazo zilikuwa hazijapangiwa siku rasmi.

Ligi hiyo ndio hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambayo hufanyika kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Ratiba hiyo imetolewa kwa kuzingatia mechi za hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika zinazoendelea, Tanzania ikiwakilishwa na Simba ya jijini Dar es Salaam katika michuano hiyo.

Hata hivyo, wadau mbalimbali wamekuwa wakihoji baadhi ya mechi kupangwa mbali hali ya kuwa timu husika zipo, na hazina jukumu lingine ambalo linakwamisha michezo hiyo kuchezwa mapema.

Licha ya kuwapo kwa mkanganyiko huo, ni vyema timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara zikaendelea kujipanga kuhakikisha zinafanya vizuri kwa kupambana kusaka ushindi kila wanapoingia uwanjani.

Nipashe inazikumbusha timu zote 20 kutoka mikoa mbalimbali ya Bara kuhakikisha kwamba zinavuna pointi zake kwa njia halali na kujiepusha na vitendo vyovyote vya upangaji matokeo.

Kama klabu zitakubali kwenda kinyume na kanuni za mchezo huo, timu zitashusha thamani ya ligi na mchezo huo wa soka unaopendwa na watu wengi zaidi duniani na vile vile zitaifanya Timu ya Taifa (Taifa Stars) isiwe imara kwa sababu inaundwa na wachezaji wengi wanaocheza katika ligi hiyo.

Mara nyingine kumekuwa na "fununu" kuwa zipo baadhi ya timu ambazo ziko katika nafasi salama, kufanya "biashara" katika mechi za hatua ya lala salama kwa "kugawa pointi".

Gazeti hili inazikumbusha klabu zote kuhakikisha zinaonyesha ushindani katika michezo yote ya ligi iliyobakia ili mwisho wa msimu, nchi ipate bingwa aliyetokana na ubora wa uwanjani na usiochanganyika na upangaji wa matokeo.

Wachezaji wanaoshiriki ligi hiyo wanatakiwa kufahamu kwamba ligi hiyo inayoonekana sehemu mbalimbali inaweza kuwapa ajira kwa kusajiliwa na klabu za nje, hivyo wanatakiwa kujituma na kuonyesha viwango vya kawaida na kuacha kushiriki kwenye mipango "haramu" kama ipo.

Mapungufu yaliyopo katika ratiba hiyo mpya inayotarajiwa kumalizika Mei mwaka huu, yasiwe chanzo cha kuvuruga ligi hiyo ambayo mpaka sasa inachezwa bila ya kuwapo kwa mdhamini mkuu baada ya Kampuni ya Simu za mikononi ya Vodacom kumaliza mkataba wake.


Kufanya vizuri, kuongezeka kwa ushindani, marefa kuchezesha kwa haki na vilabu kutekeleza maelekezo yanayotolewa na wasimizi, ni mambo ambayo yatachangia msimu ujao kuwa na mafanikio na kusahau changamoto ambazo zimejitokeza katika msimu huu.

Hakuna kisichowezekana, kizuri kinajiuza na kibaya kinajitembeza, huu ni wakati wa wadau wote wanaoshiriki katika kufanikisha ligi hiyo inachezwa, kufanya majukumu yao kwa weledi na mwisho wa siku matunda yake yataonekana na kila mmoja atafurahia kushiriki kwenye mchezo huo wa soka.

Pia kufanya vizuri na kuheshimika kwa Ligi Kuu, ndio kutazivutia taasisi na kampuni mbalimbali kuwekeza katika Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Kuu ya Wanawake na timu za Taifa za vijana na ya wanawake maarufu Twiga Stars ambazo hazina udhamini wa kutosha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Yanga, Simba klabu zinazotesana kwa zamu!

**CHAKO** ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine. Methali hii yatufunza tuvitegemee vitu vyetu wala si vya watu wengine.

Shirikisho la Kandanda Nchini (TFF) limekuwa kimya kuhusu timu zinazoshiriki ligi mbalimbali ambayo inasimamia hapa nchini kutokuwa na viwanja vyake vya michezo. Hata TFF yenyewe haina uwanja wa mashindano makubwa unaoweza kuiingizia fedha. Nadhani hii ndio sababu yashindwa kuvishauri vilabu vya Ligu Kuu kuwa na viwanja vyao.

Timu zenye viwanja ni Azam FC ya Dar es Salaam, Mtibwa Sugar FC ya Manungu, Morogoro, Kagera Sugar FC ya Bukoba, Ruvu Shooting Mlandizi, mkoa wa Pwani na JKT Tanzania, pia ya mkoa wa Pwani, yenye uwanja mdogo usioweza kuingizia watazamaji wengi. Kwa sababu hiyo inautumia Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga. Sidhani kama kuna timu ingine yenye uwanja wake; kama ipo, natanguliza samahani (tamko la heshima linalotumika kuomba radhi).

Katika viwanja vyote nilivyotaja, kile cha Azam Complex kule Chamazi kwenye viunga (kando ya jiji) vya jiji la Dar es Salaam. Yaitwa 'Complex' yaani -enye sehemu/tabia nyingi, changamani. Ni uwanja wenye mambo yote yanayohusu michezo: Uwanja wa mazoezi ya kandanda na mechi, ukumbi wa michezo ya mazoezi ya viungo (gymnasium/gym), bwawa la kuogelea (swimming pool), kliniki, cafeteria (mkahawa) n.k.

Narudia tena kusema "Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Timu zenye viwanja vyao hazihangaiki kutafuta viwanja vya kufanyia mazoezi na kutumia fedha lukuki kila siku kukodi viwanja vya mazoezi vinavyotozwa kuanzia 200,500/-, 300,000/- mpaka 1,000,000/-kwa siku kulingana na ubora wa viwanja!

Kama klabu itafanya mazoezi kwa siku 15 tu kwa gharama ya 200,500/- italazimika kulipa 3,000,750/-. Itakuwaje kwa mwezi mmoja? Fedha hizo zikidundulizwa haziwezi kusaidia kupata fedha za ununuzi wa eneo la ujenzi wa viwanja na mambo mengine kama ilivyo Azam Complex?

Yanga itakapokuwa na viwanja vyake vya mazoezi na mechi, haitakatwa fedha za matumizi ya viwanja ila klabu ndio itakayotoza fedha za mechi zitakazochezewa huko. Kumbe badala ya fedha kwenda kwingine zitakuwa zinaingia klabuni.

Itakapokuwa hivyo, kuwe na ukaguzi wa mahesabu ya mapato na matumizi kila baada ya miezi sita. Kwa wanaoamini kuwa ushindi hupatikana kwa njia ya rushwa au uchawi, watumie fedha kutoka mifukoni mwao na wasithubutu kuidai klabu kwa hali yoyote iwayo.

Twataka viongozi wenye uwezo wa kuitoa Yanga hapa ilipo na kuipeleka kwenye maendeleo yatakayoonekana kama ilivyo Azam FC iliyoanzishwa miaka michache iliyopita lakini imeipita Yanga iliyoanzishwa mwaka 1935. Badala ya kuzeeka ikiwa inajitegemea, inazeeka ikiwa tegemezi!

Aidha twataka viongozi wanaojali na kuheshimu kazi za kocha na benchi la ufundi na kuwaheshimu wachezaji. Hatutaki viongozi wanaoingilia kazi za kocha na benchi lake la ufundi wala hatutaki kocha achaguliwe mchezaji anayependwa na kiongozi kuwa ndiye anayefaa kwenye timu. Uchaguzi wa wachezaji aachiwe kocha na benchi lake la ufundi, si viongozi.

Wahenga walisema "Mtego bila chambo haunasi." 'Chambo' ni kitu kinachowekwa mtegoni kunasia wanyama; aghalabu huwa kipande cha nyama. Hutumiwa kutukumbusha kwamba hatuwezi kufanikiwa katika mambo tuyafanyayo bila ya kuwa na nyenzo zifaazo. Kwa mfano, jambo linalohitaji pesa halitengenei kama hazipo.

Kadhalika ilisemwa zamani kuwa "Ufalme ni kama mvua hunyesha na kupita." Maana yake ufalme hauwezi kudumu milele kwani huisha baada ya kipindi fulani. Methali hii hutumiwa kwa mtu anayejitapa kutokana na hali yake ya kiuchumi; anapaswa kujua kuwa hali hiyo haitadumu milele.

Hii ndio Yanga yetu ya sasa. Ule wakati wa kuringia ufadhili wa mtu mmoja na kuidhalilisha Simba kwa hali na mali, sasa imekuwa zamu ya Simba kuidhalilisha Yanga kwa kusajili wachezaji mahiri, kulipa fedha za usajili na vilabu walivyotoka bila kuwacheleweshea mishahara yao. Ndo yasemwayo na watoto wa mjini "kutesa kwa zamu."

Ni wakati mwafaka wa TFF kuviamsha vilabu vya Ligi Kuu kuwa na viwanja vyao wenyewe badala ya kutegemea viwanja vya Serikali au vile vinavyomilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM).

**marobarnabas@yahoo.com**
0715/0784 33 40 96

# Mabula akerwa wadaiwa kodi ardhi kutoshtakiwa

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, ameshangazwa na halmashauri za wilaya za Mpwapwa na Kongwa mkoani Dodoma, kushindwa kuwafikisha katika mabaraza ya ardhi na nyumba wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi na baadhi yao kupelekewa hati za madai.

Kutokana na hali hiyo, Mabula ameziagiza halmashauri hizo kuhakikisha zinawafikisha wadaiwa hao katika mabaraza ya ardhi kwa hatua zaidi kwa kuwa huko uamuzi wake ni ama mdaiwa kulipa au kunyan'ganywa miliki yake kufidia deni.

Mabula alitoa agizo hilo jana alipozitembelea wilaya hizo mbili ikiwa ni mfululizo wa ziara zake kuzuru halmashauri mbalimbali kwa nia ya kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi.

Alisema halmashauri hizo zina wamiliki wengi wa viwanja wasiolipia kodi ya ardhi, hivyo kusababisha kudaiwa fedha nyingi lakini idara za ardhi zinashindwa kuwachukulia hatua jambo linaloikosesha serikali mapato.

Mabula alisema halmashauri ya wilaya ya Kongwa inadai Sh. milioni 152 kutoka kwa wamiliki wasiolipa kodi huku Mpwapwa ikidai Sh. 128,013,696.90.

Ofisa Ardhi Msaidizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Angelina Ndemera, alisema halmashauri yake pamoja na kuwa na madeni kutoka kwa wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi, haikutoa ilani za madai kwa wadaiwa hao.

Kwa upande wa Mpwapwa, Mkuu wa Idara ya Ardhi, Anderson Mwamengo, alisema halmashauri hiyo ina wadaiwa sugu 330 wa kodi ya pango la ardhi ambao wameandikiwa na kukabidhiwa ilani hizo.

Mabula alisema pamoja na Rais John Magufuli kuhimiza suala la kulipa kodi na Wizara kujitahidi kusaidia suala hilo, halmashauri hazifanyi jitihada zozote katika kukusanya maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi.

"Kila siku inaelezwa pelekeni ilani za madai ya kodi ya ardhi kwa wamiliki lakini hakuna ufuatiliaji wowote unaofanywa na watendaji wa sekta ya ardhi jambo linalorudisha nyuma jitihada za serikali kukusanya maduhuli ya serikali," alisema.

Naibu Waziri aliziagiza halmashauri hizo mbili kufikia Machi 31, mwaka huu, watendaji wake wa sekta ya ardhi wawe wamewafikisha katika Baraza la Ardhi wadaiwa wote waliopelekewa ilani za madai.

Pia aliitaka idara ya ardhi kuhakikisha orodha ya wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi waliopewa ilani za madai inafikishwa katika kila kikao cha Kamati ya Uchumi na Mazingira vya kila robo mwaka ya Baraza la Madiwani katika kila halmashauri lengo likiwa kuitaka kamati husika kuelewa suala hilo na kufanya ufuatiliaji.



Meneja maswala endelevu wa TBL Group, Irene Mutiganzi (kushoto), akitoa mada kwa washiriki wa mafunzo ya vijana yanayolenga kuwaletea mafanikio kupitia mpango wa be the Coach Program ya TBL wakati wa Uzinduzi uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Ticts yajivunia ongezeko la huduma

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Kimataifa ya Huduma za Makontena Bandarini (Ticts), imehudumia shehena 592,000 kwa kipindi cha mwaka jana.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Ticts, Jared Zerbe, aliyabainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya kampuni katika kipindi cha mwaka jana ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Alisema Agosti, mwaka jana, walihudumia makontena 54,447 na kuweka rekodi ya makontena 31,239 yanayohudumiwa katika geti kwa mwezi wa Machi.

"Ongezeko la shehena ya ndani kwa ajili ya nje ya nchi limefikia asilimia 18, zaidi ya mwaka 2017. Mizigo ambayo inatoka nchi mbalimbali zikiwamo Congo na Zambia wanaotumia bandari yetu, iliongezeka kwa wastani asilimia 38.9 kwa mwaka 2018,"alisema Zerbe.

Alisema ongezeko la shehena linahitaji ufanisi na uharaka katika utoaji mizigo ili kupunguza muda wa mizigo kukaa bandarini, hivyo kampuni hiyo na bandari zimeongeza ufanisi na uwezo wa kuhudumia shehena kubwa zaidi.

"Msaada wa ushirikiano tunaopata kutoka kwa serikali ya Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Mapato (TRA), wafanyakazi, wateja na wadau wanaotumia bandari hii, kimekuwa chanzo cha ukuaji wa huduma za Ticts katika mwaka 2018.

"Binafsi najivunia kwa timu yetu nzuri sana ya wafanyakazi wa Ticts ambao wamekuwa wakifanya kazi pamoja vizuri na kupambana na ongezeko la kuhudumia shehena," alisema Zebre.

Naye Mkurugenzi wa Huduma wa Ticts, Donald Talawa, alisema kutokana na juhudi walizoongeza kwenye kampuni hiyo, wamejipanga kuhudumia ongezeko la mizigo.

"Tunaongeza ufanisi ili kuhudumia shehena hii inayokuwa, Ticts imejikita kusonga mbele na kuimarisha wajibu wake kama lango kuu la nchi kuelekea Mashariki, Kusini na Afrika ya Kati," alisema Talawa.

# Muhimbili yajipanga kupunguza foleni za wagonjwa wa kliniki

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), unaangalia namna ya kuboresha mfumo wa kliniki ili wagonjwa wahudumiwe kwa wakati na hatimaye kupunguza msongamano wanapofika kupata matibabu.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Profesa Lawrence Museru, alisema hayo jana wakati akizungumza na madaktari bingwa wa hospitali hiyo kuhusu namna bora ya kuboresha huduma za matibabu katika taasisi hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma wa MNH, Aminiel Aligaesha, Muhimbili inahudumia wagonjwa wa nje 1,500 kwa siku na wagonjwa 1,200 hadi 1,300 wanalazwa wodini wakati wote.

"Wagonjwa wa nje walio wengi wanapenda kuja asubuhi hata kama kliniki zao zinaanza mchana, hivyo wamekuwa wakisababisha msongamano unaofanya Muhimbili kuweka utaratibu mpya wa kuwahudumia wanapofika ili kupunguza msongamano," alikaririwa Profesa Museru katika taarifa hiyo.

Alisema hatua hiyo ina lengo la kuboresha huduma katika kliniki hizo na kuondoa msongamano wakati mgonjwa au wagonjwa wakisubiri kuona madaktari bingwa.

"Wakuu wa idara kupitia kwa madaktari mtuletee mapendekezo ambayo tutaangalia jinsi ya kujenga mazingira bora ambayo wagonjwa watatumia muda mfupi kumwona daktari. Tunataka mgonjwa asikae kwenye foleni muda mrefu," alisema Prof. Museru kupitia taarifa hiyo.

Prof. Museru pia aliahidi kuwa uongozi wa hospitali chini ya bodi ya wadhamini, utaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi mbalimbali wanaofika hospitali hapo kupata matibabu.

"Naomba tuendelee kutumia vizuri na kikamilifu miundombinu iliyopo ili kuongeza tija na wananchi wametuamini ndiyo maana wengi wamekuwa na matumaini makubwa sana na huduma tunazotoa" alisema.

Kuhusu upatikanaji wa dawa katika hospitali hiyo, alisema licha ya kupatikana kwa zaidi ya asilimia 95, wanaendelea kuimarisha utoaji wa dawa kwa wagonjwa ili kuhakikisha kila mgonjwa anayetibiwa anapata dawa kwa wakati.

Katika mkutano huo madaktari walijadili njia za kuimarisha utoaji wa huduma bora za matibabu kwa wagonjwa mbalimbali sambamba na kukubaliana kufanya kazi kwa juhudi ili kufikia malengo yaliyowekwa na hospitali hiyo ya kutoa huduma bora za ubingwa wa juu nchini.

Muhimbili ina wafanyakazi 2,705, kati yao madaktari ni 328 ambao ni madaktari bingwa ni 186 na 142 wa kawaida. Aidha, Hospitali ina wauguzi 946 na waliobaki ni wafanyakazi wa kada nyingine.

# Jaji Mkuu atoa neno kesi ya Zitto

INATOKA UK 3

Akizungumzia Wiki ya Sheria, alisema mwaka huu mahakama imeyapa heshima Makao Makuu ya nchi, Dodoma, kwa kufanya maadhimisho ya Wiki ya Sheria kitaifa yatakayofanyika katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere Square.

Prof. Juma alisema wiki ya utoaji wa elimu ya sheria kitaifa itazinduliwa kwa maandamano yatakayoongozwa na Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa Februari 2, mwaka huu, saa 12:00 asubuhi.

Alisema pia wiki ya utoaji elimu ya sheria itafanyika katika kanda zote za kimahakama na kwa mwaka huu, jijini Dar es Salaam yatafanyika Mnazi Mmoja.

Jaji mkuu alisema wananchi wote wenye malalamiko ya kisheria wafike katika maeneo yaliyoandaliwa na mahakama katika wiki ya utoaji elimu ya kisheria yatakayoanza Januari 31 hadi siku ya kilele, Februari 6, mwaka huu, badala ya kubeba mabango wakati wa kilele cha maadhimisho hayo.

"Kilele cha siku ya sheria kitafanyika jijini Dar es Salaam na hafla hiyo itaongozwa na Rais Dk. John Magufuli," alisema Jaji Mkuu.

Alisema mambo yatakayotolewa elimu ya sheria mwaka huu kutoka kwa wadau wa mahakama ikiwamo taratibu za ufunguaji kesi, sheria na taratibu zinazotumika katika kuendesha kesi, taratibu ya kesi za mirathi na ardhi na msaada wa kisheria.

Pia itatolewa elimu ya sheria ya ushughulikiwaji wa malalamiko mbalimbali, kupokea maoni na mapendekezo ya namna bora ya kuboresha shughuli za mahakama na sekta nzima ya sheria.

Alisema maadhimisho ya mwaka huu yanabeba kauli mbiu kwamba "Utoaji wa Haki kwa Wakati ; Wajibu wa Mahakama na Wadau".



Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wanawake Tanzania (TWPG), Mhe. Margaret Sitta, akiongoza kikao cha pamoja cha wajumbe kutoka Umoja wa Wabunge wanawake Tanzania (TWPG) na ugeni kutoka Shirika la Umoja wa kimataifa la wanawake (UN Women) kilichofanyika jana katika ofisi za Bunge Jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

## Diwani wa CCM

INATOKA UK 5

Alimsihi kuwa akiwa sawa na mzazi wake, abadili uamuzi wa kugomea kusoma taarifa hiyo kwa kuwa yeye ni sawa na baba yake kwa kuwa amekuwa akimwona toka angali mdogo anakua. Diwani Philip Kalyalya alilieleza braza hilo kuwa, kitendo cha diwani huyo kukataa kusoma taarifa ni kosa kubwa kwa kuwa amekiuka kanuni za baraza la madiwani, hivyo suala hilo ni vema likafikishwa kwenye kikao cha maadili ili kumjadili.

Meya Mbogo alimwita mara ya pili diwani huyo ili asome taarifa hiyo lakini hoja zote hizo hazikutosha kumshawishi kwa kuwa aliendelea na msimamo wake.

Baada ya kuona msimamo huo, Meya alisema hakuna mtu anayemlazimisha kusoma taarifa hiyo kwa kuwa huo ndio uamuzi wake.

Alisema anaelewa uchungu alio nao lakini utaratibu alioutumia si mzuri kwenye kikao kama hicho na wala si wa kiuongozi kwa kuwa unaleta sura mbaya kwa watumishi wa Manispaa hiyo na kwa wananchi waliohudhuria baraza hilo na hata suala analolilalamikia sio la manispaa bali wahusika wa barabara ni Wakala wa barabara za Mijini na Vijijini (Tarura).

Meya alisema kwa kuwa amekataa kusoma taarifa hiyo, kama ataona itafaa, ataisoma kwenye kikao kijacho cha robo tatu ya mwaka kama baraza litaridhia.

# Waitara ataka uchunguzi

INATOKA UK 5

Aidha, aliwataka wakuu wa wilaya mkoani hapa kuhakikisha wanasimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa na fedha za serikali ili kukamilika kwa wakati huku ikiwa na kiwango kinachostahili.

Pia alionyeshwa kusikitisha na taarifa ya shule hiyo kuhusu wanafunzi 43 ambao wameshindwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu kutokana na utoro.

Waitara alisema pamoja na serikali kuipa kipaumbele sekta ya elimu, kumekuwa na utoro wa wananfunzi waliochanguliwa kuanza masomo. Aliutaka uongozi wa shule na wilaya kufuatilia kwa makini ili wale waliochaguliwa waanze masomo mara moja.

Akiwa mkoani Iringa, alikagua ujenzi wa madarasa matatu na matundu sita ya vyoo katika Shule ya Msingi Lyalamo, yaliyogharimu Sh. milioni 66, ujenzi wa mabweni mawili katika Shule ya Sekondari Isimila ambayo bado hayajakamilika pamoja na kuzungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

## Taasisi ya Dk. Ntuyabaliwe yazidi kuunga mkono elimu

INATOKA UK 4

amelongwa. Alisema siku wakitangaziwa kuhusu shindano hilo, mwalimu wao alikuwa akiwafundisha somo la Jeografia kuhusu kilimo hivyo alitumia somo hilo kutunga hadithi aliyoimaliza baada ya siku tatu.

Mwakilishi Ofisa Elimu wa Manispaa ya Kinondoni, Grace Mtesigwa, ambaye ni Ofisa Elimu ya Watu Wazima alisema ili taifa liendelee lazima mkazo uwekwe kwenye elimu kama alivyofanya Rais Magufuli kutoa elimu bure.

Alisema kupitia maktaba hiyo yenye aina tofauti ya vitabu sasa itawawezesha wanafunzi kusoma na kupata vitu ambavyo hawavijui.

"Umewarithisha wanafunzi hawa kile ambacho baba yako alichokufundisha kwa hiyo kijiti hiki kitarithishwa kizazi hadi kizazi, endelea na shule nyingine Tanzania ili tupate Watanzania wenye elimu na maisha bora," alisema.

Mwakilishi wa wazazi ambaye ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mwalitani Tandale, Sudi Makamba alisema kitendo kilichofanywa na taasisi hiyo ni cha kuingwa.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Doris Misigaro aliahidi kuitunza maktaba hiyo na kueleza kuwa itaondoa changamoto na kufanya wanafunzi kupenda kusoma zaidi.

## Sababu Tido kukwepa jela

INATOKA UK 2

TBC, kwa makusudi alitumia madaraka yake vibaya kwa kutia saini mkataba wa uendeshaji na utangazaji wa vipindi vya televisheni kati ya TBC na Channel 2 Group Corporation (BV1) bila kupitisha zabuni, kitu ambacho ni kinyume na Sheria ya Ununuzi na kuinufaisha BVI.

Katika shtaka la pili, Tido alidaiwa kutumia vibaya madaraka yake kwa kutia saini makubaliano kwa utangazaji wa digitali duniani kati ya TBC na BVI, yaliyofanyika Juni 16, 2018.

Katika shtaka la tatu, alidaiwa kuwa Agosti 11, 2008 na Septemba, 2008 akiwa Dubai, Tido alitumia vibaya madaraka yake kwa kutia saini mkataba wa makubaliano wa ununuzi, usambazaji, kufunga vifaa vya usambazaji na mnara wa utangazaji kati ya TBC na BVI na kuifaidisha BVI.

Pia katika shtaka la nne, alidaiwa kuwa Novemba 16, 2008 akiwa Dubai, alitumia vibaya madaraka yake kutia saini mkataba wa makubaliano wa kuendesha miundombinu ya utangazaji (DTT Broadcast Infrastructure) kati ya TBC na BVI na kuinufaisha BVI.

Katika shtaka la mwisho, alidaiwa kuwa kati ya Juni 16 na Novemba 16, 2008 akiwa UAE, Tido aliisababishia TBC hasara ya Sh. 887,122,219.19. aliposomewa mashtaka hayo, alikana na kuwa nje kwa dhamana.

## Majambazi

INATOKA UK 2

jeshi la polisi kufuatilia kwa kina suala hilo kwa kuwa vijana wake (majina yanahifadhiwa) wamelazwa hospitalini pamoja na mlinzi aliyemtaja kwa jina la Dickson.

Raykiza Ntepa, ofisa Mtendaji kata ya Manga, licha ya kukiri kuwapo kwa taarifa hiyo, alisema wako kwenye kikao cha kamati ya ulinzi na usalama ya tarafa ya Eying, kujadili mambo kadhaa, likiwamo tukio hilo na kwamba watafuatilia ili kuwabaini wahusika.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema hajapelekewa taarifa juu ya tukio hilo na mkuu wa polisi wilaya na kwamba atahitaji apate taarifa hizo ili kujua undani wake sambamba na kuweka mikakati ya watuhumiwa ili wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya dola.

# IPP kujenga kiwanda cha kubangua korosho

INATOKA UK 3

njia ya ukuaji wa sekta ya korosho katika kuliongezea thamani zao hilo.

Ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho Mtwara ni mwendelezo wa IPP katika kutekeleza sera ya taifa ya maendeleo ya viwanda nchini kuelekea uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Dk. Mengi kwa kushirikiana na mbia wake, Daktari Bingwa wa Upasuaji kutoka India, Nagesh Bhandari, wameamua kujenga kiwanda cha dawa kitakachojulikana kama M-Pharmaceuticals. Kiwanda hiki ambacho kitajengwa eneo la Kerege, Bagamoyo, kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha kwa siku chupa 100,000 za dripu kwa mwaka kitazalisha chupa milioni 30.

Kiwanda kingine cha kutengeza simu za mkononi za kisasa na za bei nafuu, kinatarajia kuanzishwa na Kampuni ya IPP Touchmate Ltd, ambayo pia itatengeneza vifaa mbalimbali vya kielektroniki, vikiwamo vya nyumbani.

Kiwanda hicho ambacho kitakuwa cha kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki kitajengwa eneo la Mikocheni, Dar es Salaam na uwekezaji huo unakadiriwa kuwa Sh. bilioni 11.5 na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha simu za mkononi 1,200 kwa siku, kuajiri watu 2,000 na watu wenye ulemavu kupewa kipaumbele.

Kiwanda kingine ni cha kuunda magari Tanzania na tayari Kampuni ya IPP Automobile Ltd imeshaingia mkataba wa makubaliano na kampuni ya Youngsan Glonet Corporation kutoka Korea Kusini.

Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha zaidi ya ajira 1,500 kwa Watanzania.

Kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuuza mabasi ya abiria na magari ya mizigo kuanzia tani 2.5 mpaka tani 28 na Oktoba, mwaka huu na baadaye mwaka 2022 kitaanza kuzalisha magari madogo.

# Takukuru yataja taasisi za umma vinara katika kuomba rushwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (Takukuru), mkoani Manyara, imesema wenyeviti wa serikali za mitaa na vijiji, watendaji wa kata na vijiji ndiyo vinara wa kuomba na kupokea rushwa.

Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Fidelis Kalungura, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu yao kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Oktoba hadi Desemba 2018.

Alisema kwa kipindi hicho jumla ya taarifa za kuomba na kupokea rushwa 146 zililipotiwa ofisini kwao huku wenyeviti wa mitaa na vijiji zikiripotiwa taarifa 27.

Alisema watendaji wa kata na vijiji kulikuwa na taarifa 23, idara ya elimu ziliripotiwa taarifa 12, jeshi la polisi taarifa 10, afya na utawala zikilingana zikiwa taarifa tisa kila moja, mahakama na mabaraza ya ardhi zikifungana kwa kuripotiwa taarifa saba kila mmoja..

Aidha, alisema chanzo cha wenyeviti wa serikali za mitaa na vijiji pamoja na watendaji wa kata na vijiji kuongoza kwa kuomba na kupokea rushwa ni kwa kuwa wanahudumia wananchi wengi huku akisema wengi wao ni watu wenye hali ya chini.

"Sababu nyingine inayowafanya waongoze kwa rushwa ni tatizo la kushindwa kusoma mapato na matumizi na wengine wanawaomba rushwa wananchi wanapoenda ofisini kuomba kugongewa mihuri ofisini kwao," alisema. Alisema wenyeviti wengine wanaomba rushwa kwa kisingizio kuwa hawana malipo wanayolipwa na serikali hivyo wanaona kuomba fedha kidogo kwa wananchi ili wawapatie huduma maana hawana mshahara.

Karungula alifafanua ameongea na wakurugenzi wa halmashauri za wilaya kuwa watafanya semina kwa watumishi wa serikali za mitaa na vijiji waliopo chini yao ili waweze kudhibiti kuendelea kwa vitendo hivyo vya rushwa.

Rushwa kwa upande wa elimu, alisema imekuwa ikijitokeza kutokana na tatizo la kusajili wanafunzi wasiokuwa na sifa hivyo wataalamu wa elimu kupitia maafisa elimu wametakiwa washirikishe ofisi ya katibu tawala wa mkoa ili kuepusha tatizo hilo.

Aliongeza katika sekta ya elimu wanafunzi wamekuwa wakipachikwa kwa njia zisizo halali maana wahusika wanapata nafasi ya wanafunzi ambao hawana sifa na siyo wanafunzi walio katika mfumo ulio rasmi.

Wakati huohuo, alisema Takukuru kutokana na ufuatiliaji wa miradi mbalimbali na shughuli zingine zinazotekelezwa na serikali mkoani hapa imefanikiwa kuokoa jumla yaSh. milioni 474.51 kiasi ambacho kimerejeshwa serikalini au kuelekezwa kwenye kazi zilizotarajiwa kufanyika.

Mtaalamu huyo wa kuzuia na kupambana na rushwa alijigamba kuwa kutokana na usimamizi ulio bora wa taasisi hiyo mkoani hapa ndio maana viongozi wa kitaifa wakifika hapa hawatoi maagizo ya kuchunguza miradi inayotekelezwa hapa yenye thamani ya Sh. bilioni 49.07.



Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri Arusha Vijijini, Dk.Wilson Mahera Wilayani Arumeru, akimkabidhi cheti maalumu mwakilishi kutoka shirika lisilo la kiserikali la A for Africa, Marianne Rick smith kwa kutambua mchango wao katika sekta ya elimu kwenye halmashaurihiyo.**PICHA: ALLANISACK**

## Mila potofu kwa jamii ya wafugaji pasua kichwa

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania, (UWT), Queen Mlozi, ameitaka jamii ya wafugaji kuacha mila na desturi potofu za ukeketaji kwa watoto wa kike, ndoa za ututoni pamoja na mimba katika umri mdogo ili wasikatishe ndoto zao.

Alisema hayo katika ziara yake ya kikazi wilayani Longido jana wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Mundarara, Tarafa ya Engarenaibor.

Alisema ameumizwa na kitendo cha kuona watoto wa kike wadogo ambao wanastahili kuwepo shule wamepata ujauzito na wengine wakilazimishwa kupelekwa (kuposwa) kwa wanaume wenye umri mkubwa. "Jambo hili linasikitisha kwa kweli, naomba wanaume waacheni hawa watoto wasome, ni viongozi wa baadaye," alisema.

Alieleza urithi pekee ambao mzazi unatakiwa kumpatia mtoto wa kike ni elimu, na kuwataka wote wenye tabia za kukatisha ndoto za watoto hao kuacha mara moja.

"Nasema waheshimuni watoto hawa, acheni kucheza na watoto wa shule, kwa nini mnakatisha ndoto zao," alihoji.

Alisema pia kumeibuka matukio ya rushwa ya ngono na kuwataka wanawake pamoja na watoto wa kike kupinga na kukemea rushwa ya ngono.

"Katаeni rushwa ya ngono, nawasisitiza kabisa mkawe mabalozi wazuri wa kuyasemea haya, rushwa ya ngono hapana," alisema. Aliwataka wanawake kuzungumza kwa uwazi na watoto wao wa kike juu ya ukuaji wao, na wasifiche kuwaeleza ili watambue jambo zuri na baya ni lipi.

"Wanawake ni jeshi kubwa, ni tegemezi kwa taifa, zungumzeni kwa undani na uwazi na watoto wenu wa kike, kumbuka pia mtoto wa mwenzio ni wako," alisema.

Aligusia pia watoto wadogo kutokupewa lishe bora, huku Mkoa wa Arusha ukiwa na asilimia 29.2 kwa watoto wenye utapia mlo, hali ambayo alisema ni hatari na akaomba wapewe lishe nzuri kwa afya zao.

"Nawakumbusha mtoto mchanga wa miezi 0-6 anatakiwa kupata maziwa ya mama,lakini baada ya hapo anaendelea kukua hivyo wapeni lishe bora nawaomba," alidai.

# Tanesco yaleta matumaini mapya uhakika wa umeme

**Na Joseph Mwendapole,** ARUSHA

WATEJA wa Shirika la Umeme Nchini (Tanesco), Mkoa wa Arusha wamelipongeza shirika hilo kwa mageuzi makubwa ambayo yamesababisha kuwe na umeme wa uhakika na kupunguza kukatika mara kwa mara.

Mmoja wa waliotoa pongezi hizo ni Mkurugenzi wa makampuni ya Lodhia Steel, Sailesh Pandit ambaye alisema kwa sasa umeme umetulia na wanaendesha shughuli za uzalishaji bila tatizo.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari wanaotembelea miradi ya shirika hilo, Pandit alisema kiwanda chake kinapata megawati 7 ambao ni wastani wa umeme unaotumika kuendesha baadhi ya mikoa kama Manyara na hajawahi kuwalalamikia Tanesco kuhusu kukatikakatika kwa umeme wala kuwepo kwa umeme mdogo.

"Kusema ukweli sina baya kwa Tanesco tunafanya kazi kwa karibu sana na wenzetu wa Mkoa wa Arusha na hata nikipiga simu kwa Meneja wa Mkoa saa nane usiku atapokea na kama kuna shida atatupa vijana wake ndani ya muda mfupi tu watarekebisha kama kuna kasoro," alisema.

"Tunaposema Tanzania ya viwanda mimi naamini kabisa itawezekana kwa sababu tumepata umeme wa uhakika maana kuzalisha nondo inatumia umeme mwingi sasa kama huna umeme wa uhakika huwezi kufanya lolote, viwanda ni Tanesco na Tanesco ni viwanda," alisema. Pandit alisema kwa uzoefu alionao umeme miaka minne iliyopita ulikuwa unakatika mara kwa mara na kusababisha baadhi ya viwanda kupata hasara ya malighafi lakini baada ya maboresho hayo maisha yamekaa sawa. "Kuhusu umeme niseme ukweli tu kwamba kwa sasa tuko dunia ingine kabisa sijawahi kusikia hapa Arusha wenye viwanda wanalalamikia umeme, Arusha mmejipanga vizuri kwa sababu mnasikiliza wateja na mnatenda.

"Nawaomba watu wanaotaka kuja kuwekeza Arusha kwamba huu ni muda mwafaka kwa sababu hakuna tena shida ya umeme mimi nalipa bili ya Sh. bilioni 1.1 kwa mwezi kwasababu uzalishaji wa nondo unahitaji umeme mwingi sana," alisema.

Meneja Utawala wa kiwanda cha Sunflag Arusha, Magesa Charles, alisema umeme wanaopata kutoka Tanesco unatosheleza mahitaji yao ya kila siku na kwa mwezi mzima wanaweza kutumia hadi uniti za umeme za Sh. milioni 2.1.

"Lazima tuwapongeze Tanesco kwa kutuletea umeme wa uhakika sisi hapa maboresho waliyoyafanya yametugusa kwasababu hatuna tena malalamiko nao hivyo tunakila sababu ya kuwapongeza.

"Hata ikitokea tatizo ukawapigia kwa kweli Tanesco Arusha wako vizuri watakuja haraka na kutatua tatizo na kama wanakata umeme kwaajili ya matengenezo wanatuarifu mapema tunajipanga kwa ujumla hali imekuwa nzuri sana," alisema. Naye Meneja Mkuu wa kiwanda cha Tanelec cha kutengeneza transfoma, Zahir Saleh, alisema kutokana na umeme wa uhakika wanaopata kutoka Tanesco hivi sasa wanafanya uzalishaji kwa masaa 24.

Alisema kwa mwaka uwezo wa Tanelec ni kuzalisha wastani wa transfoma 14,000 na kwa siku wanaweza kuzalisha hadi transfoma 30 hivyo ni dhahiri kuwepo kwa umeme wa uhakika ni jambo muhimu kwao.

"Changamoto tunayopata sisi hapa ni ucheleweshaji wa malighafi katika Bandari ya Dar es Salaam kwa sababu mzigo utakaofika Bandari ya Mombasa na Dar es Salaam siku moja basi ule wa Mombasa utafika na utatumika hadi uishe wakati ule wa Dar es Salaam haujafika ila umeme wa uhakika tunao," alisema.

Alisema kuanzia mwaka 2017/18 umeme haukatiki katiki kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ambako wakati mwingine walilazimika kusimamisha uzalishaji.





# Hasira za mama wa kambo zaishia kumchoma moto mtoto

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MTOTO wa miaka saba ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili, mkazi wa kijiji cha Chemchem katika kata ya Arusha Chini, Wilaya ya Moshi amedaiwa kufanyiwa unyama na mama yake wa kambo kwa kuchomwa moto mikono yake.

Mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa), alikumbwa na mkasa huo Januari 23 mwaka huu, baada ya kudaiwa kuomba tochi kwa mama yake ili aende chooni kujisaidia.

Taarifa kuhusu ukatili huo ilitolewa jana na wajumbe wa kamati ya ulinzi wa wanawake na watoto ya kijiji cha Chemchem ambao wamepatiwa mafunzo na Shirika la Tusonge kwa ajili ya kutekeleza mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA).

Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo ambaye pia ni Mwalimu wa Shule ya Msingi Chemchem, Anna Tarimo alisema aligundua ukatili huo na kutoa taarifa kwa serikali ya kijiji kutokana na kudhoofu kwa afya ya mwanafunzi huyo.

"Huyo mtoto amechomwa moto mkono wa kushoto kwa kutumia mwiko wa kusongea ugali. Mama yake wa kufikia aliweka mwiko huo jikoni ukashikana na ugali, akautoa na kumkandika nao mikononi. Kosa lake eti ni kumuomba tochi (kurunzi) ili akajisaidie haja ndogo," alisema mjumbe huyo wa kamati ya ulinzi.

Aidha, inaelezwa kuwa baada ya kukamatwa alihojiwa jana na serikali ya kijiji na kisha kuachiwa kwa kupewa onyo kali, badala ya kuripoti Polisi.

Alipoulizwa Ofisa Mtendaji wa Serikali ya Kijiji hicho, Patrick Mlay kuhusiana na tukio hilo alikiri kukamatwa kwa mama huyo aliyetekeleza ukatili huo, Eva Edson (19).

Akizungumzia ukatili na madhara yake, Mratibu wa mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia na ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto wa Shirika la Tusonge,Joyce Kessy alisema kuripotiwa kwa matukio hayo kunatokana na kukamilika kwa zoezi la kuundwa na kujengewa uwezo wanakamati hao.

Tayari wanakamati hao wamekutana katika kikao maalumu kwa ajili ya kupata mrejesho wa jamii kuhusiana na kazi zinazofanywa na kamati za Mtakuwwa ikiwa ni pamoja na kuibua matukio ya ukatili na kuyaripoti kunakohusika.

Mradi huo wa kupinga ukatili wa kijinsia na ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto, unatekelezwa na Shirika la Tusonge katika Kata ya Arusha Chini, Moshi Vijinini kwa ufadhili wa Foundation For Civil Society.

"Tusonge imeona umuhimu mkubwa wa kukutana na wanakamati hao ili kujadili hatua walizochukua baada ya mafunzo, mambo yaliyojitokeza, mafanikio na changamoto walizokutana nazo katika shughuli zao zinazolenga zaidi kupinga masuala ya ukatili wa wanawake na watoto.



Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii Professa Adrof Mkenda, akiangana na Balozi wa Ujerumani nchini Dkt, Detlef Waechter baada ya kumaliza mazungumzo yaliyofanyika Wizarani, jijini Dar es Salaam jana. kuhusu kujiandaa kushirika maonyesho Ujerumani mwezi wa 3. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shule ya walemavu yakabiliwa uhaba wa vyoo

**Na Paul William,** MOSHI

SHULE ya msingi ya watoto wenye mahitaji maalum ya Mwereni iliyopo Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vyoo vya walimu hali inayosababisha kuchangia huduma hiyo na wanafunzi.

Hayo yalisemwa jana na Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Damas Urenge wakati alipokuwa akitoa taarifa hiyo kwa Naibu Katibu mkuu wa Umoja wa wanawake wa chama cha Mapinduzi (UWT) Taifa, Jesca Mbogo alipotembelea shuleni hapo na kutoa msaada wa vyakula kwa wanafunzi hao wenye mahitaji maalum.

Mwalimu Urenge alisema kuwa, shule hiyo yenye jumla ya wanafunzi 700 ambapo kati yao 80 ni wanafunzi wenye mahitaji maalum kama ulemavu wa ngozi (Albino) pamoja na watoto wasioona haina vyoo kwa ajili ya walimu hali ambayo imepelekea kuchangia vyoo vya walimu.

Alisema kuwa, changamoto nyingine ambayo inaikabili shule hiyo ni ufinyu wa bajeti ya malazi na uendeshaji wa shule huku pia akilalamikia uwepo wa upungufu wa madawati kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la awali.

Akijibu changamoto hizo, Naibu Katibu Mkuu, Jesca Mbogo alisema kuwa, upo umuhimu mkubwa wa uongozi wa manispaa kuandaa harambee maalum itakayo wakutanisha wadau mbalimbali wa elimu pamoja na viongozi wa chama mkoa ili waweze kuchangia kwa ajili ya kutatua changamoto ya vyoo.

Jesca alisema kuwa, serikali ya awamu ya tano imejidhatiti kuhakikisha watu wenye mahitaji maalum wanaishi wa amani kwa kuimarisha ulinzi wao na kuwataka kuondoa hofu.

"Watoto wenye ulevu wa ngozi huko nyuma walikuwa wakiishi kwa mashaka kwa kuhofia usalama wao lakini tokea kuingia kwa serikali ya Dk. Magufuli imejidhatiti kuhakikisha ulinzi na usalama wao umeimarika" alisema Jesca.

Aidha, aliwataka wanafunzi kuendelea kusoma kwa bidii ili kulipa wema anaofanya Rais Magufuli kwa kutoa elimu bure huku pia akiwasisitiza kutambua kilichowapeleka shuleni hapo ni elimu pekee na sio mambo mengine.

# Wataalam watupiwa lawama migogoro ya ardhi

**Na Mary Mosha,** SAME

SERIKALI mkoani wa Kilimanjaro imesema uwepo wa migogoro kati ya wakulima na wafugaji imekuwa ikichangiwa na baadhi ya wataalamu wa ardhi, kushindwa kuweka na kusimamia mgawanyo sahihi wa matumizi bora ya ardhi.

Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Marwa Wilaya ya Same, Mkuu wa Mkoa Dk. Anna Mghwira, alisema kwamba serikali haitasita kuwachukulia hatua wataalamu katika idara mbalimbali ikiwemo idara ya ardhi ikiwa watashinwa kuwa chachu ya kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Alisema katika halimashauri wapo baadhi ya wataalamu ambao sio waaminifu wamekuwa chanzo cha migogoro kutokana na kushindwa kuweka matumizi bora ya ardhi pamoja na kutoa elimu kwa wakulima juu ya madhara hayo ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

"Baada ya kuonge na kuwasikiliza wakulima na wafugaji tumebaini kuwa wapo baadhi ya wataalamu wetu ambao wamekuwa chanzo cha migogoro kutokana na kushindwa kusimamia sheria na taratibu zilizowekwa pamoja na kupokea rushwa ili kupindisha ukweli hasa wanapofika vijijini, "alisema mkuu wa mkoa na kuongezea kuwa

"Nawaagiza watendaji wote katika halimashauri zote mkoa hapa kuhakikisha wanalitazama suala la wakulima na wafugaji katika kuweka sawa matumizi bora ya kwa ardhi wakionyesha eneo la malisho na la wakulima ili kupunguza migogoro,"alisema Katika hatua nyingine Dk. Mghwira aliwataka viongozi wa vitongoji na vijiji, kuainisha njia kwa ajili ya mifugo pamoja na kuchimba mabwawa ambayo yatatumika kwa ajili ya majosho ya mifugo.

Akizungumza Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Majid Kabyemela ambaye ni Ofsa Kilimo na Mifugo wilayani humo, alisema wametenga Sh. milioni 25 kwa ajili ya kufanya mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vinne vya kata ya Ruvu.

Alisema migogoro kati ya wakulima na wafugaji inachangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mifugo mingi katika eneo hilo, na kwamba kata ya Ruvu pekee inaongoza kwa kuwa na mifugo mingi katika wilaya ya same. Kwa upande wake katibu wa baraza la usuluhishi migogoro ya ardhi kata ya Ruvu Nangala Koole Mollel alisema kutokuwepo kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji inasababisha migogoro hiyo kuwepo

"Watendaji wamekuwa wakifika kwenye maeneo haya bila kuleta suluhu la kudumu kwani wamekuwa wakitoa majibu ya serikali imelichukuwa ....lakini ukweli ni kwamba hakuna matumizi sahihii ya ardhi katika eneo hili hivyo tunaomba mpango huo usimamiwe ili kutokomeza migogoro kati ya pande hizo mbili.



# Dk. Bashiri ataka UVCCM kufanya kumbukizi ya Mwalimu Nyerere

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Dk. Bashiru Ally ameitaka Jumuiya ya Umoja wa Vijana (UVCCM), kufanya kumbukizi ya miaka 20 ya kifo cha Mwl. Julius Kambarage Nyerere kwa kusimamia maeneo matatu ambayo ni uongozi, uchumi na uenezi aliyoyapa jina la (V3).

Dk. Bashiru alitoa rai hiyo juzi jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na viongozi na wanafunzi wa vyuo vikuu vilivyopo mkoani humo.

Alisema maadhimisho ya kumbukizi ya kifo cha Mwl. Julius Nyerere kwa mwaka huu 2019 yameanza mapema mwezi Januari ili kutoa nafasi kwa Watanzania kujua dhamira njema ya kiongozi huyo.

"Fikra za CCM zinalindwa zaidi katika kipindi hiki cha rais Dk. Magufuli kuliko kipindi chochote cha uongozi hivyo vijana mnapaswa kufahamu zaidi fikra sahihi za CCM na kuzieneza popote ulimwenguni,"alisema

Aidha, aliwataka vijana kutojibweteka badala yake wapambane katika kulinda umoja, amani na utaifa wa nchi kwa kuwa ulinzi wa vitu hivyo umesababisha chama kuwa na maadui wengi ndani na nje ya nchi.

"Vijana tukae mkao wa vita takatifu katika kulinda umoja wa kitaifa, kuulinda uhuru wetu, uchumi wetu, wana mapinduzi wetu, viongozi wetu pamoja na kumlinda na kumtetea jemedari wetu rais Magufuli,"alisema.

Dk. Bashiru aliwataka kutumia maarifa katika kupambana dhidi ya vita hiyo badala ya kutumia nguvu huku akiwakumbusha silaha mojawapo ya wasomi hao kuwa ni kufanya vizuri katika masomo yao na kuitumia elimu hiyo kwa manufaa ya umma badala ya kujikweza na kutukana Watanzania. "Tusitumie vyeti vya vyuo vikuu kwa kuwa viongozi wajeuri na wa ovyo, wenye viburi badala yake tutumie maarifa hayo kuwa viongozi bora watakaoleta tija kwa taifa hili,"alisema.

Aidha, alitaja baadhi ya miiko ya uongozi kuwa ni kutodhulumu watu, kuendekeza anasa, kumkemea anayekupinga, kubagua watu (kuwa na makundi) kujilimbikizia mali, kutoshaurika, pamoja na kutoa au kupokea rushwa.

Aliwataka viongozi kujitokeza kushiriki katika mijadala mbalimbali siyo kuikimbia kwa kuwa hiyo ndiyo nafasi pekee ya kuzungumzia mazuri yanayofanywa na CCM.

Kuhusu uchumi alisema kazi ndiyo kipimo cha utu kwa mujibu wa katiba ya CCM na utu ni heshima hivyo kila mmoja ni lazima afanye kazi kwabidii ili kuinua uchumi wake, familia na nchi kwa ujumla ili kutimiza falsafa ya serikali ya awamu ya tano ya hapa kazi tu.

Aidha, alisisitiza vijana kutumia mitandao ya kijamii kueneza ujumbe wa matumaini kwa wanyonge walio pembezoni na kukandamizwa hususani wanawake kwa kuwa sasa ukombozi wao unakuja.

"Serikali haitafuta mitandao ya kijamii kwa kuwa vita siku hizi inapiganwa katika mitandao hiyo, hivyo ni vyema tuitumie kutuma ujumbe wa matumaini kwa wanyonge wanaonyonywa na kupuuzwa hii ni moja ya mbinu za kivita kwa kuwa vita inahitaji hamasa na msisimko,"alisema.



Mchuuzi wa mifagio akisaka wateja katika eneo la Mnazi Mmmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Kamati ya siasa CCM yatoa maagizo mazito kwa MSD

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma imeiagiza Bohari Kuu ya Dawa (MSD), kuhakikisha inapeleka vifaa tiba na dawa katika vituo vya afya vilivyokamilika mkoni hapa.

Aidha, kamati hiyo imewataka wauguzi na wataalam wa afya kutoa huduma kwa kuzingatia weledi kama ambavyo sheria na kanuni za taaluma yao zinavyoelekeza.

Agizo hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo Wilayani Chamwino mkoani hapa.

Mkanwa alisema inashangaza kuona fedha za ujenzi wa vituo zinatolewa siku moja na fedha za vifaa tiba na dawa lakini MSD, wanashindwakupeleka dawa kwenye vituo baada ya kukamilika.

Alisema hali hiyo ni sehemu ya uzembe mkubwa ambao hauendi sambamba na dhamira ya Rais Magufuli, ya kuwaletea wananchi maendeleo hasa katika kuboresha sekta ya afya nchini.

"Nawaagiza MSD mpeleke vifaa mara moja katika vituo vya afya vilivyokamilika, ili viweze kufanya kazi na wananchi wapate huduma kama ilivyokusudiwa, " alisisitiza Mkanwa.

Aidha kuhusu watumishi wa afya alisema wanatakiwa kufanya kazi yao kwa upendo, huruma na uadilifu hali ambayo itawafanya wananchi watatamani kufika katika vituo vya afya kuhudumiwa.

"Ninyi mko Ikulu hivyo kituo chenu kinatakiwa kuonyesha mfano kwa kuwa kituo bora kabisa, na si kujaa kwa malalamiko na sifa mbaya kutoka kwa wagonjwa," alisema.

## UN Women lamwaga fedha kufanya takwimu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SHIRIKA la Kimataifa la UN Women limetoa fedha kiasi cha Dola za Marekani milioni moja kwa ajili ya kuzalisha takwimu zinazohusiana na jinsia nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Dk. Albina Chuwa, alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zilizopata ufadhili huo.

Aidha, alisema kupitia mradi huo kila mwanamke na mtoto wa kike atatambuliwa.

"Tanzania ni kati ya nchi chache Afrika ambazo zimepata ufadhiki huo utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu,"alisema Dk, Chuwa.

Alisema miongoni mwa kazi zitakazofanywa kupitia mradi huo ni pamoja na kuangalia sera za jinsia ukusanyaji wa takwimu matumizi ya data zote ili kuona nchi inafikia wapi ifikapo 2020. "Tutaendelea kufanya kazi na vyombo vya habari na kushirikiana sina shaka tutakwenda sawa ili tufike pale tunapotaka, "alisema Chuwa.

Mratibu wa mradi Mariam Kitenge kutoka ofisi ya Taifa ya takwimu alisema watafanya kazi na UN Women na wataangalia zaidi sera katika kuzalisha takwimu.

Alisema mradi huo utakuwa wa nchi nzima na Tanzania ni kama mwanzilishi nchi nyingine zitakuwa ni Kenya na Uganda.

"Hapa Tanzania pia tutafanya kazi na ofisi ya mtakwimu ya Zanzibar," alisema

Mkurugenzi Mkazi wa Mashariki Kusini mwa Afrika, Dk, Izeduwa Briggas, alisema anaamini fedha hizo zitatumika kama ilivyokusudiwa na kuleta matokeo yaliyokusudiwa.

Naye Mkurugenzi wa Sera kutoka NBS, Ephrahim Kwesigabo alisema mradi utawezesha kujua hali ilivyo kwa baba na mama na kuweka ili kutengeneza sera imara.

# Vijana 179 wawezeshwa mtaji wa kuku kujikwamua kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIJANA 179 wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja wamepatiwa mtaji wa kuku kwa ajili ya biashara ili kuweza kujikomboa kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Akizungumza katika zoezi la ugawaji wa kuku hao, Naibu Waziri wa

Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, alisema kuwa wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi wajiandae kujiondoa katika soko.

Alisema hivi sasa vijana wengi wamejitokeza kufuga kuku hivyo mahitaji ya kwa siku zijazo yatatosheleza.

Alieleza kuwa Zanzibar inaingiza tani 200 za kuku kila mwezi kutoka nje ya nchi, hivyo ni vyema vijana kufuga kwa wingi ili kuteka soko hilo.

Waziri wa Uwezeshaji Wanawake,Watoto na Wazee, Mauldlic Castico, alisema Serikali itaendelea kuwawezesha vijana ili waweze kujiajiri katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo na ufugaji.

Aliwataka vijana kuitumia vyema fursa hiyo ya mradi wa ufugaji kuku ili kujikwamua kiuchumi na kuwawezesha vijana wengine kupata Kuku hao ili uwe endelevu.

"Tutahakikisha tunatatua changamoto za ukosefu wa ajira kwa vijana kupitia wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali na washirika wa maendeleo," alisema.

Alieleza kuwa Serikali imeona umuhimu wa kuanzisha wizara hiyo ili kuona vijana wanasaidiwa katika kuwatafutia mbinu mbalimbali za kujiajiri kwa lengo la kuondokana na vitendo viovu ambavyo vitawaharabia malengo yao ya maisha.

Naye msimamizi wa mradi wa usimamizi wa ufugaji wa kuku, Rashid Muhammed alisema kuanzishwa kwa mradi huyo kwa vijana wataweza kujiingizia kipato.

Aidha, aliomba Serikali kuongeza nafasi na fursa za ajira kwa vijana wenye uwezo wa kufanya kazi kwa kuendeleza taifa.



Baadhi ya wakazi wa Mkoa wa Tabora wakiwa katika maandamano ya kuunga mkono kampeni za upandaji miti na utunzaji mazingira jana. **PICHA:MPIGA PICHA WETU**

# MCT latoa msimamo kukuza weledi tasnia ya habari

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

BARAZA la Habari Tanzania Ofisi ya Zanzibar, limeomba Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, kuendelea kushirikana nalo ili kukuza weledi katika tasnia ya habari.

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji kwa kamati ya Baraza la Wawakilishi inayoangalia maendeleo ya wanawake habari na utalii, Ofisa Mtendaji wa MCT Zanzibar, Shifaa Hassan Said, alisema ni vyema wizara hiyo kuongoza vyombo vya habari ili vijielekeze katika kujenga badala ya kubomoa.

Alisema kwa upande wake, baraza la habari limekuwa likifanya jitihada kubwa katika kuhakikisha vyombo na wanahabari vinazingatia maadili na sheria za nchi katika taarifa zao ili kuepusha mifarakano katika jamii. "Tumekuwa tukitoa mafunzo mbalimbali kwa waandishi wa habari ili kuhakikisha wanazingatia maadili ya kazi zao, " alisema.

Naye Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, alilitaka baraza hilo kuzipa mafunzo kamati zake ili zifahamu majukumu na changamoto zinazolikabili kwa lengo la kusaidia kuzitatua inapobidi.

Alieleza kuwa waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kutoa habari kwa lengo la kuielimisha umma lakini pia serikali inapata kufahamu changamoto zinazowakabili wananchi na kuzifanyia kazi.

Wajumbe wa kamati hiyo wamekuwa wakiendelea na utaratibu wa kuzitembelea taasisi zilizo chini ya wizara vya habari, utalii na mambo ya kale ili kujua mafanikio na matatizo yanayozikabili.

# Watano wapoteza maisha kwa kudaiwa kula sumu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WATOTO watano wa familia moja wakazi wa Shehia ya Shanake Wilaya ya Micheweni Pemba, wamefariki dunia baada ya kula chakula kinachosadikiwa kuwa na sumu.

Aidha, wengine wawili wamelazwa katika Hospitali ya Micheweni wakipatiwa matibabu baada ya kuathirika na chakula hicho.

Mwandishi wa Nipashe alifika katika hospitali hiyo na kuzungumza na mmoja wa waathirika wa tukio hilo, Chumu Sadik Shoka (28), alisema hali hiyo ilijitokeza mara baada ya kumaliza kula na alianza kutapika.

"Baada ya kula chakula kikiwa na samaki aina ya kasa nikanza kujihisi vibaya na kuanza kutapika," alisema Chum.

Daktari wa hospitali hiyo, Mbwana Shoka, alikiri kupokea wagonjwa hao ambapo mmoja alifariki baada ya kufikishwa kwa ajili ya matibabu.

Aidha, alisema, kutokana na uchunguzi wa awali, inakisiwa kuwa vifo hivyo vimesababishwa na sumu iliyokuwa kwenye chakula walichokula.

Baba mzazi wa mtoto, Asma Makame Ali, alieleza kuwa baada ya kumaliza kula waliona hali ya baadhi ya watoto inabadilika na akawawahisha katika kituo cha afya Kiuyu Mbuyuni.

Waliofariki katika tukio hilo ni Hafidh Khatib Rashid, Khifidh Khatib Rashid, Fatma Khatib Ali, Sabra Said Rashid na Hamida Hamad Rashid, na waliolazwa ni Chumu Sadik Shoka na Asma Makame Ali.

Naye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Micheweni, Mariam Omar Ali, alifika Hospitalini hapo na kuwataka waathirika wa tukio wasifiche ukweli juu ya chakula walichokula ili kuwawezesha madaktari kutambua chanzo cha tatizo.




## NDAUKA ATAMANI MTOTO MWINGINE

Soma UK.14

JUMAMOSI JANUARI 26, 2019

Nipashe
BT
BURUDANI TELE



# USIFURAHI MSAMAHA, JITATHMINI

## BASI SAWA



# Nuh agoma kurudi maisha ya ndoa

NUH Mziwanda ambaye kwa sasa anaishi kisela baada ya kuachana na mkewe, amesema hana mpango wa kuoa kwa sasa.

"Ninaweza kusema bado nipo nipo kwanza hadi hapo baadaye nitakapoona kuna haja ya kuvuta jiko, lakini kwa sasa ni bora niendelee kuwa peke yangu," amesema Mziwanda.

Msanii huyo wa muziki wa kizazi kipya, ambaye sasa anashuti video ya wimbo wa 'Natapatapa', amesema ameamua kuupa nafasi kubwa muziki wake akiamini kwamba bado ni kijana mdogo anaweza kuoa wakati ukifika.



# Papii Kocha amshangaa JPM

MWANAMUZIKI Papii Kocha, amemvulia koti Rais Dk. John Magufuli, akisema ana taarifa zote kuhusu yeye kiasi ambacho kilimshangaza kugundua tatoo aliyochora mkono wake wa kulia.

Akizungumza hivi karibuni, Papii Kocha, alisema tatoo hiyo ambayo ina maandishi ya JPM ameichora kama njia ya kumshukuru kwa yote aliyomfanyia katika maisha yake.

"Siku moja nilipokwenda kuonana naye aliniambia anajua mkono wangu una tatoo yenye jina lake, nilishangaa sana nikawaza amejuaje" amesema Papii.



# Rose Ndauka atamani mtoto mwingine

NYOTA wa Bongo movies, Rose Ndauka, amesema bado ana ndoto ya kupata mtoto wa pili kama akipata mwanamume sahihi.

Rose amesema anajisikia raha anapokuwa na mtoto wake wa kwanza, lakini anadhani ni wakati umefika wa kuongeza mwingine.

"Ninataka kuongeza mtoto wa pili, lakini tatizo ni mwanamume wa kuzaa naye sijampata, ila ninaamini Mungu ni mwema atanipa mtu sahihi wa kuzaa naye," amesema Ndauka.

## INSTA-TWITTER





**Hata** umvishe gamba mjusi hageuki kuwa chatu-**Dogo Janja.**



**Hivi** ulishawahi kuongopewa na mtu unaemuheshimu na kumpa thamani ya nyumbani kwako-**Babu Tale.**



## Dr. Ipyana afurahia kumwimbia Mungu

MSANII wa muziki wa Injili, DR. Ipyana Kibona, amesema miaka 15 ya utumishi wa kiroho umemlipa kuliko angebaki katika taaluma yake ya utabibu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, mwimbaji hiyo wa kibao 'Moyo Wangu' amesema anakuwa na furaha kuimba injili kwani anawatibu watu wengi kwa kiroho, kimwili na kiafya.

"Sijutii kuacha kazi yangu ya udaktari, kwa kutumia nyimbo zangu nawafikia watu wengi sana na huko nawatibu kiiroho, kimwili na kiafya jambo ambalo linanipa faraja na kunitia nguvu," amesema Dr Ipyana.




@burudanitele

>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow

### UNASEMAAA...

## Billnas, Roma waonya 'Funga Geti' majangili wanapita

MWAKA wa kolabo! Pengine ni mwanzo mzuri kwa wasanii wa Bongo Fleva ambao wameanza mwaka 2019 kwa kutoa kolabo za nguvu.


Wasanii Billnas na Roma, wamejiunga katika mwendelezo huo wa kolabo baada ya kuachia vuideo ya ngoma yao kali 'Funga Geti' ambayo inatikiza anga la muziki nchini.

Ngoma imefanywa na mtayarishaji wa video za muziki Nicklass huku audio ikitengenezwa na prodyuza maarufu nchini Mr T touch.



### BODA 2 BODA

## Profesa Jay atambulisha rasmi 'Women' yake



RAPA na mbunge wa jimbo la Mikumi, Profesa Jay, hatimaye ameachia video ya wimbo wake mpya aliyomshirikisha mrembo kutoka Kenya Victoria Kimani.

Ngoma hiyo inayoitwa 'Woman' imekuwa ikisubiriwa kwa hamu baada ya muda mrefu kutangaza ujio wake.

Hata hivyo, mara ilipoachiwa katika mtandao wa You tube, mashabiki wa muziki wa kizazi kipya wal-impongeza kutokana umahiri wake wa kuimba pamoja na kwenda sambamba na mrembo huyo.

### INSTA-TWITTER




Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Aisee** leo ndiyo nimeamini kuwa ndoto ni moja kati ya vitu vinavyokatisha tamaa vijana. Leo nimeota niko angani kwenye ndege naelekea Ujerumani, lakini mpaka sasa ni siku ya 10 tuko angani tu-**Peter Msechu**



**Tusemane,** tuchekane, tudharauliane, lakini kamwe usije ukamcheka binadamu mwenzio kwenye riziki, ulemavu na uzazi kwa sababu hivi vitu anavileta Mwenyezi Mungu. Akiamua kuvichukua wala hatumii nguvu-**Shamsa Ford.**



**Hakuna** lisiloweze-kana dhidi ya juhudi na maarifa-**Elizabeth Michael 'Lulu.'**

# Kuumbe!

# RAYVANNY

## Usifurahi msamaha, jitathmini upya

Na Adam Fungamwango

MSANII Rayvanny alimetoka kifungoni baada ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), kutangaza kutoa msamaha kutokana na kibao chao 'Mwanza' kuwa na maneno machafu yanayokiuka maadili.

Basata imemsamehe msanii huyo na wenzake baada ya kuomba msamaha na kuahidi hawatofanya kosa kama hilo tena.

Awali iliwafungiaa wasanii hao kufanya kazi ya sanaa ndani na nje ya Tanzania hadi kufutiwa kibali cha kufanya tamasha.

Mkasa mzima ulikuwa hivi. Baada ya kufungiwa wimbo huo, Rayvanny aliurudisha kwenye mitandao ya kijamii baada ya wimbo huo kukataliwa kuwekwa kwenye mtandao wowote, hapo ndipo Basata walipoongeza adhabu na kuwapiga faini ya milioni tisa.

Katika kile kilichoonyesha kuwa hawakujali chochote waliuimba tena wimbo huo kwenye tamasha lao ambalo lilifanyika mkoani Mwanza , kitendo hicho pia kilisababisha adhabu kuongezeka na mwisho wake wasanii hao walifungiwa kufanya kazi yeyote ya sanaa ndani na nje ya nchi lakini pia kufutiwa kibali cha kufanya tamasha lao.

Kitendo cha msanii huyo na mwenzake kufurahia kufutwa adhabu wala si tija, kinachotakiwa sasa Rayvanny na wengineo wajifunze kutokana na makosa.

Kitendo cha wao kurudia makosa hayo hayo mara kwa mara hakileti picha nzuri.

Mwenyewe ameona tangu alipofungiwa jinsi alivyokuwa akihaha huku na huku kuhakikisha mambo yanakaa sawa na kwa kiasi ilimuathiri.

Hili pia ni somo hata kwa wasanii wengine chipukizi kuwa hakuna mtu atakayefumbiwa macho kwa hili.

Kwa siku za karibuni baadhi ya wasanii wamekuwa watunga nyimbo zenye maneno yenye ukakasi na yasiyoleta maana nzuri mbele ya jamii.

Wenyewe wanadhani kuwa kufanya hivyo ndipo ngoma hizo zitavutia au zitapendwa na mashabiki wengi wa muziki, hasa vijana.

Cha kushangaza ni kwamba kwa sasa hata wasanii wakubwa ambao tayari wana majina yao na mashabiki wengi na hawalazimiki kufanya hivyo ili ngoma zao kupendwa, nao wamejiingiza kwenye mkumbo huo huo wa kuimba nyimbo zenye maneno 'machafu' yasiyotamkika mbele za watu waliostaarabika.







# JANUARI KWAO KAMA WANATELEZA

Na Adam Fungamwango

HII inaitwa hakuna kulala! Wakati mwaka 2019 umeanza kuchanja mbuga tayari baadhi ya wasanii wameanza kuonyesha makali yao kwa kutoa ngoma kali.

Wasanii hawa wanaingia kwenye rekodi ya kutoa ngoma mwanzoni mwa mwaka huu.

Hebu tuwaangalie wasanii hao ambao hawakutaka kusubiri sijui nani atoe, ili waangalie pa kusahihisha makosa yao na badala yake wao Januari wameshauwasha moto.

**Ruby-Alele**

Msanii Ruby amerejea tena, na safari hii mwezi Januari tu ametoa ngoma inayoitwa 'Alele'.

Ni ngoma ya mapenzi na wimbo huu ndiyo unaweka rekodi ya kuwa wa kwanza wa bongo fleva kutolewa kwa mwaka 2019.

Umetolewa na kuingizwa mtandaoni Januari 2 mwaka huu.

**Beka Flavour-Fainali**

Msanii huyu naye hajapoa. Amekuja na ngoma yake mpya anayoiita 'Fainali' Ameitoa rasmi Januari 9 mwaka huu.

Ni wimbo wa mapenzi, unaoonyesha mwanaume kunogewa na penzi la mwenzi wake na kumpatia ahadi kedekede za kulinda na kutunza penzi lake.

**Mbosso-Tamu**

Marombosso naye anakuwa mmoja kati ya wasanii waliotoa ngoma Januari mwaka huu, kwani tarehe 18, ametambulisha rasmi ngoma yake inayoitwa 'Tamu'.

Kama kawaida ya wasanii wengi wa kisasa wa bongo fleva, pia huu ni wimbo wa mapenzi.

**Enock Bella-I Swear**

Huyu ni msanii ambaye mwezi Januari haukumpita hivi hivi, badala yake ametoa ngoma moja hivi inayoitwa 'I Swear'.

Ni ya mapenzi, lakini ina tofauti kidogo na zingine. Hii inaonyesha kuwa kijana ameozeshwa ndoa ya mkeka na msichana ambaye si yeye aliyempa mimba ila alifananishwa sura na mhusika.

Kesi ya Juma kapewa Rashid. Kijana alifanana na mtu mmoja aliyempa mimba msichana, hivyo ndugu na majirani alikuwa wanamvizia mtu huyo, lakini kwa bahati mbaya kijana huyo aliyepita alifanana wajihi na mharibifu, akakamatwa na kufungishwa ndoa na msichana mjamzito, huku yeye siyo mhusika.

**Mr Blue ft Nandy-Blue**

Msanii mkongwe nchini Mr Blue, naye ameingia kwenye orodha ya waliowahi kutoa ngoma mwaka 2019.

Wimbo huo unaitwa 'Blue' akimshirikisha msanii wa kike bora kwa sasa Nandy.

Uimbaji wa Mr Blue unajulikana huku ukichagizwa na sauti laini yenye kubembeleza na kudeka ya Nandy na kuufanya wimbo uwe wa kuvutia.



Rubby



Beka Flavour



Mbosso



Enock Bella



Mr Blue ft Nanc

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA



1. Jamani hivi wanautani au nimekuwa mzembe kiasi gani? Ngoja nivunge - Baraka Sembosi, Kasera Tanga.
2. Huyu bosi anakuja saa ngapi? Maana safari yenyewe ni ndefu - Charles Ngadaya, Ifakara.
3. Yaani akizidi kuchelewa hiki kiti naondoka nacho nikakalie mbele ya safari - 0787 194 216.
4. Si nimekuambia ukae, hutaki. Sasa simama hivyo hivyo ukichoka utakaa mwenyewe - George, Upanga.
5. Mgeni anakuja, akijia mkaribishe kwenye kiti - 0718 554 254.
6. Duuuh, bisi hii dharau. Haja yako nidondoke uninyime msosi siyo? - 0715 555 233.
7. Hapa sikai, ngoja nikisogeze nikakae kule - 0717 544 033.
8. Hapana, sio kwa uzoba huo. Jiongeze basi utimke na hicho kiti - Mama Nah, Manzese DSM.
9. Hahaha, kweli farasi una ubongo wa panzi, yaani unatulia kabisa kwa kufungwa kwenye kiti! - Mama Nah, Manzese DSM.
10. Ngoja aliyenifunga aje, nampa teke la mbavu mpaka ajute. Hawezi kunidharau kiasi hiki - Mwanahawa Ally, DSM.
11. Babu wewe si una mbio kuliko mnyama ye yote, sasa unashindwa nini kutimua na kiti chao? - Mwanahawa Ally, DSM.
12. Kila siku wakae wao tu mie nisimame, leo hakai mtu hapa, ukibisha jaribu kukaa - Benali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
13. Ndio maana mtu akikuita farasi pigana naye. Si unaona akili zake zilivyo mbovu. Unafungwaje na kiti? - Sudi, Sinza DSM.
14. Bosi kaniambia nilinde kiti chake jamani, msianze kusema saaana, natimiza wajibu tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
15. Wewe acha ujinga kalia hicho kiti, kikivunjika unasepa kilaini kabisa - Mariam Benali, Migombani Zenji.
16. Leo bosi hapandi mgongoni mwangu, atakaa kwenye hiki kiti halafu tunaanza safari - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
17. Daaah kweli binadamu nuksi. Yaani farasi na ujanja wake wote kazuiwa na kiti hicho! - Julius Mbita, Ifakara Morogoro.
18. Haya sasa, anayejifanya mbabe aje achukue hiki kiti tuone - Bob Nizzo, Buguruni Chama DSM.
19. Hiki kiti changu jamani, nimenunua kwa machinga na nimeamu kukilinda, tatizo nini? - Beatrice Mbita, Ifakara Morogoro.
20. Hapo ndio utaamini binadamu mtawala wa vyote duniani. Farasi katulizwa kijiiinga! - Daima Uledi, Mabibo NIT DSM.
21. We si unajifanya una mbio, timua sasa mbio zako tuone kiti kitakavyokukimbiza - Sudi, Sinza DSM.

PICHA MPYA



TUMA MESEJI - 0773 477 311




## Ujauzito unapokuwa shida

**Na Adam Fungamwango**

HAKIKA akinamama lazima wapewe heshima zao kutokana na kuwa na sifa kuu ya kuwazaa binadamu wanaoipamba dunia na wakati mwingine kuivuruga.

Katika mchakato wa kuwaleta viumbe hao duniani, akina mama wanawalea watoto tumboni mwao kwa muda wa miezi tisa, ambazo ni sawa na wiki 38.

Maungo yao yamejengwa kama njia ya binadamu anayopitia kuja kuiona dunia na kufanya kile alichoagizwa na Mola wake.

Kiumbe hicho cha tumboni kinatumia uhai na chakula cha mtu mwingine ili nacho kuishi.

Akiwa na kiumbe tumboni, mama anakabiliwa na mabadiliko mengi ikiwamo kiafya na kitabia.

Filamu ya wiki 38, imejaribu kuwakumbusha watu hasa wanaume kuwa kinachofanywa na wapenzi au wake zao ambao wakiwa na ujauzito si tabia yao halisi bali ni mabadiliko yanayotokana na mchakato huo wa uzazi.

Imechezwa na Haji Salum maarufu kama Mboto, Yvonne Cherrie maarufu kama Monalisa na wengineo.

Inaanza kuonyesha maisha ya kawaida ya mume na mke mjamzito.

Mume anamwandalia mkewe mjamzito maji na kifungua kinywa kabla ya kuondoka

Pamoja na kuchelewa sana, hatimaye Mboto anakwenda kazini.

Njiani anapokea simu kutoka kwa mkewe, arudi nyumbani mara moja kuna dharura.

Anaporudi huku akiwa ametahayari, anamkuta mkewe mzima wa afya na alichomuitia ni kwamba anataka akamuitie kijana mmoja wa jirani ili aweze kukaa naye.

Jambo hilo linamkasirisha, lakini analitekeleza. Kila siku zinapozidi kusonga mbele ndipo Monalisa anapozidi kumchukia mumewe Mboto.

Siku moja anamtoa mkewe 'auti', lakini anampa sharti la kwenda wakiwa pia wameongozana na yule kijana wa kiume anayempenda.

Licha ya kuchukia, lakini Mboto kama kawaida anatekeleza maagizo ya mkewe.

Wakati wakipata chakula, Monalisa anamkatalia mumewe kukaa karibu naye kwa sababu eti ananuka shombo na anaweza kutapika.

Kwa shingo upande pia anatii.

Wanapofika nyumbani, Monalisa anatakaa kulala na mumewe kwa sababu zile zile. Anaamua kutoa godoro na kulala barazani.

Mbali na hili, Monalisa anakuwa na tabia ya kumtolea maneno makali mumewe mbele ya hadhara za watu. Lakini mume yote alivumilia akijua anasumbuliwa na ujauzito.

Siku ilipofika alijifungua. Monalisa alipata mtoto wa kike baada ya miezi tisa kufika au wiki 38. Anaanza kukumbuka visa alivyokuwa akimfanyia mumewe. Anamuomba msamaha mumewe, maisha yanaendelea wakiwa wanalea 'bebi' wao..

**Simu 0716 350534.**
**afungamwango@gmail.com**



# MTUKUDZI

## Wengi aliwafundisha, hakuwaaga

JUDITH Wambura maarufu zaidi kwa jina la Lady Jaydee amesema atamkumbuka daima nguli wa muziki wa Afro-Jazz kutoka nchini Zimbabwe, Oliver Mtukudzi maarufu kama Tuku.

Mtukudzi alifariki dunia Januari 23 mwaka huu katika Hospitali ya Avenues Clinic jijini Harare baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Amefariki akiwa na umri wa miaka 66 na Lady Jaydee ameamua kubainisha kile anachokikumbuka zaidi kwa nguli hiyo kuwa ni unyenyekevu wake.

Ikumbukwe Lady Jaydee aliimba pamoja na Mtukudzi wimbo walioupa jina la 'Mimi Ni Mimi' ambao waliutoa mwaka 2013.

Katika mahojiano yake na BBC Swahili, Jaydee ambaye alionyesha kuwa na huzuni kubwa anasema Mtukudzi alikuwa kama Baba yake wa muziki aliyemuonesha njia kwenye maisha ya muziki.

"Nakumbuka kwa mara ya kwanza kuonana na Oliver ni wakati niliportoka kutoa albamu yangu ya Machozi na nilikutana nae kwenye tuzo za Kola nchini Afrika Kusini," anasema Jaydee.

"Nilipomuona nilimkimbilia na alionyesha unyenyekevu wa hali ya juu na akasimama kunisubiri na tulizungumza kwa muda mrefu."

Anasema mara baada ya mazungumzo yake na Mtukudzi walibadilishana mawasiliano na baada ya kuwasiliana kwa muda mrefu, hatimaye wakajaliwa kushirikiana kwenye wimbo wa Mimi ni mimi walioutoa mwaka 2013.

"Kwakweli Mtukudzi ni mtu wa kawaida mno na ni mnyenyekevu na hilo ndilo nitakalomkumbuka daima, kwani hakuwa na makuu na alinipa misingi ya kuwa mwanamziki mkubwa Afrika.

"Alinipa ushauri mwingi na mara kwa mara tulikuwa tunawasiliana, ingawa kwa siku za hivi karibuni sikuwahi kuwasiliana naye hadi anapatwa na umauti."

Mtukudzi alizaliwa Septemba 22, 1952 katika eneo la mashambani la Highfield, Salisbury, Zimbabwe na kukulia huko. Anafahamika kwa jina la utani la Tuku.

Mbali na muziki, Mutukudzi pia ni mfanyabiashara, mwanaharakati wa haki za binadamu na balozi wa UNICEF Kusini mwa Bara la Afrika.

Alianza kutambulika zaidi kimuziki baada ya kuingia katika Kundi la Wagon Wheels mwaka 1977, akiwa na wenzake kadhaa, akiwemo Thomas Mapfumo.

Alikuwa anaimba muziki wake katika lugha tatu, Kishona, Kindebele na Kiingereza na huchanganya ala za muziki wa kiasili kwenye nyimbo zake, jambo lililompa umaarufu mkubwa dunia nzima.

Tofauti na wenzake katika Kundi la Wagon Wheels waliokuwa wakimuimba vibaya Rais wa zamani wa Zimbabwe, Robert Mugabe, Mutukudzi alikuwa akimsifia sana na kusababisha anufaike kwa misaada mbalimbali kutoka serikalini.

Mutukudzi ni baba wa watoto watano na mpaka sasa ana wajukuu wawili. Watoto wawili kati ya hao, ni wanamuziki.

Mwaka 2010, mwanaye kipenzi, Sam Mutukudzi ambaye naye alikuwa mwanamuziki, alifariki dunia kutokana na ajali mbaya ya gari.

Mutukudzi amekuwa akidaiwa mara kwa mara kwamba ni mwathirika wa ugonjwa wa Ukimwi ingawa mwenyewe amekuwa akikanusha vikali madai hayo.

Kati ya wasanii wenzake waliokuwa wakiunda kundi la Wagon Wheels, ni yeye pekee aliyebakia hadi umauti unamkuta. Wenzake wote wamekufa kwa Ukimwi.

Hivi karibuni, mashabiki wake nchini humo walipatwa na mshangao mkubwa baada ya kitabu kiitwacho Tuku Backstage kuvuja kikiwa na kashfa nyingi za ngono zinazomhusu gwiji huyo, mwandishi akiwa ni Shepherd Mutamba.

Mtukudzi katika maisha yake kaoa mara mbili, mke wake wa kwanza ni Melody Murape aliyemuoa mwaka 1979 na ndoa yao ikadumu hadi mwaka 1993 na mke wake wa pili ni Daisy Mtukudzi.

# Jay Z, Meek Mill kuwasaidia Wamarekani weusi



WASANII wawili wa Hip Hop, Jay Z na Meek Mill wameanzisha taasisi ya kutoa msaada wa kisheria kwa wamarekani weusi wanaotumikia vifungo nchini Marekani.

Kwa mujibu wa Jay Z, taasisi hiyo haitahusika na wanaotenda makosa, badala yake itajikita kwa kuwasaidia wale ambao wamekamatwa kwa makosa batili.

"Nataka tueleweke vyema, kama mtu amefanya makosa anapaswa kwenda jela kwa makosa yake lakini mambo haya hayana usawa na dunia nzima inajua hivyo".



## Gift kumbuka Kiafrika haikubaliki

KUONYESHA maungo nyeti katika mitandao ya kijamii ni kitendo ambacho kinawapa watu mitazamo tofauti.

Lakini kwa mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria, Gift, kwake jambo hilo halimshtui kiasi kwamba anasema hadharani hajutii na kuona jambo hilo la kawaida na hata mpenzi wake anafurahia.

Video iliyowachafua wafuasi wake wengi ni ile aliyoipost hivi karibuni ambayo alionekana akiwa na nguo ya ndani pekee. Watu wengi walimjia juu wakisema haistahili kuweka hadharani na inamvunjia heshima.

## Chioma wa Davido huyoooo

MPENZI wa mwanamuziki nyota wa Nigeria, Davido, amerudi katika mitandao ya kijamii baada ya kuwa kimya kwa muda mrefu.

Chioma, ambaye amekuwa akimpagawisha msanii huyo kwa mahaba mazito, amekuwa mbali na mitandao ya kijamii kwa kile kinachoelezwa kuwa bize na kuandaa kipindi chake cha televisheni.

Mrembo huyo wiki hii alishiriki kuweka picha kwenye akaunti yake ya Instagram na kuibua furaha kwa mashabiki wake.





## Jamani we mrembo unawadatisha

MREMBO kutoka Ghana, ameibua mjadala mzito katika mitandao ya kijamii baada ya kujinadi kwa msanii wa kiume anayetaka kumsogelea lazima awe anamiliki gari la kifahari.

Akitumia jina la Oheema Glory, katika Twiter, mwana dada huyo ambaye ameumbika kisawasawa amesababisha maadhi ya wasanii wa Nigeria kutaharuki kutokana na onyo lake hilo kupokewa katika maoni tofauti.


Baadhi waliotoa maoni yao walisema mrembo huyo ana umbo zuri linalomfanya kila mwanamume kumtolea macho, lakini sharti lake hilo ndilo linawashangaza wengi.

## 2Baba bora umekubali yaishe

NYOTA wa muziki wa Nigeria, 2baba, amejaribu kutuliza joto la bifu lake na msanii mwenzake Blackface, baada ya kusema hakuna ugomvi kati yao.

Hivi karibuni Blackface, alitangaza kuwa na ugomvi kati yao unaotokana na 2baba kuhama lebo waliyokuwa wakifanya kazi pamoja.

Mwimbaji huyo akihojiwa katika redio ya MAX 102 FM. Alisema analifunga rasmi jambo hilo kwa kueleza hakuna matatizo kati yao na kila kitu kipo sawa.



## SAFU



### Mionzi ya Sheria

Na John Juma
0716217615

# 'Ni sawa falsafa kidini, ila michezo ipo kisheria'

WIKI hii Rais John Magufuli, amekutana na viongozi wa dini waliompa ombi la kufutwa michezo ya kubahatisha. Hebu tuangalie sheria inasemaje?

Sheria ya Fedha Namba 4 ya mwaka 2017, iliyofanyiwa marekebisho na bunge kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura Na. 166.

Marekebisho yaliipa Mamlaka ya Mapato (TRA) jukumu la kukadiria, kukusanya na kuhasibu kodi kwenye michezo ya kubahatisha kuanzia Julai 1, 2017. Kisheria michezo hiyo inabaraka za kuchezwa nchini.

**MICHEZO YA KUBAHATISHA**

Ni michezo inayochezwa kwa njia ya karata, dau, kifaa cha kielekroniki, kifaa cha kiufundi au mashine za fedha, kadi ya malipo au chochote chenye uwakilishi wa thamani.

Pia ni bingo, gurudumu la bahati, kamari ya karata, mashine zenye upenyo wa kupenyeza sarafu na mbio za farasi .

Shughuli za michezo ya kubahatisha, haijumuishi michezo inayochezwa kwa karata maeneo ya nyumbani pasipokuwa na lengo la kujipatia fedha kupitia michezo hiyo.

**KODI**

Kodi katika michezo ya kubahatisha inatozwa katika aina sita za shughuli za michezo ya kubahatisha ambayo ni kasino, ubashiri kwenye michezo, bahati nasibu kwa njia ya ujumbe mfupi, bahati nasibu ya taifa, mashine zenye upenyo wa kupenyeza sarafu, na zile zinazojulikana kama forty site.

Bodi ya michezo ya kubahatisha inatoa leseni kwa waendesha shughuli za michezo ya kubahatisha kuendesha michezo hiyo nchini kila mwaka na pia kuhuishwa.

**KUWASILISHA `RITANI'**

Uwasilishaji wa ritani katika michezo ya kubahatisha unategemea na aina ya mchezo, kuna kasino inapaswa kuwasilisha ritani kila wiki na kwa michezo mingine inapaswa kuwasilishwa ritani kila mwezi.

Namna ya kufanya malipo katika michezo ya kubahatisha inaeleza kuwa , mlipakodi anapaswa kujisajili kupitia mfumo wa Revenue Gateway System (RGS) ili kupata namba ya udhibiti, pia atatakiwa kuwasilisha fomu iliyosainiwa kwenye benki yake kwa ajili ya mchakato wa kufanya malipo. Benki ya biashara itatumia fomu iliyosainiwa na kuwasilishwa na mlipakodi kwa ajili ya malipo kupitia akaunti ya TRA.

Kiasi chini ya Sh. 5,000,000 kitalipwa kwenye akaunti katika benki za biashara na kiasi kinachozidi Sh. 5,000,000 kitalipwa kupitia mfumo wa TISS katika akaunti ya Benki Kuu.

**MUHIMU**

Wadau wakiwamo walipakodi wanapaswa kuzingatia mambo yafuatayo, awali ni kulipa kodi inayotozwa kwenye michezo ya kubahatisha kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa chini ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura Na. 166;

Kusajili biashara ili kupatiwa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kwa wale wasiokuwa na usajili.

Aidha, kuwasilisha ritani za kodi ya michezo ya kubahatisha kwenye Ofisi ya TRA walikopatia usajili wa TIN na kutumia namba za utambulisho wa malipo ("GFS Codes") zilizoainishwa kwenye Jedwali hapo juu pindi wafanyapo malipo husika.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977, ibara ya 3(1) inasema bayana kuwa Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia, isiyokuwa na dini.

Na kama haitoshi, kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa imani na uchaguzi katika mambo ya dini. Tena basi, kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari la mtu binafsi, na shughuli na uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi. Hii ni kwa kujibu wa Ibara ya 19(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

**ANGALIZO**

Kwa mantiki hiyo itoshe kusema falsafa za kidini hazifai kutumika kuingia moja moja kwenye mapato ya serikali , kwani taifa linahitaji kuwa na kazi mbalimbali za uzalishaji na vyanzo vingi vya mapato lakini pia ni jambo lililokubalika kisheria kuwa na michezo ya kubahatisha.



### Kalamu ya Mwalimu

Reubeni Lumbagala

# REA ianzishe programu kufikisha umeme shuleni

TUMEONA juhudi kubwa zinazofanywa na serikali kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali nchini hasa vijijini. Jitihada hizo zinatokana na umuhimu wa nishati katika kuchagiza maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Kutokana na mahitaji makubwa ya kusambaza huduma ya umeme, serikali iliitenganisha Wizara ya Nishati na Madini na kuunda wizara mbili zinazojitegemea za Madini na Nishati.

Lengo mojawapo lilikuwa ni kuipunguzia wizara mzigo wa kushughulikia masuala mengi ambayo yaliielemea lakini zaidi kuiwezesha kila moja kuongeza tija na ufanisi katika kuwahudumia wananchi.

Katika kuongeza kasi ya usambazaji umeme maeneo mbalimbali nchini, serikali iliunda Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ili kushirikiana kwa karibu na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kufanikisha azma ya kuviwashia vijiji vya Tanzania umeme .

Awali, Tanesco ilikuwa na mzigo mkubwa wa kuwahudumia wateja wote wa mijini na vijijini katika kuwafikishia umeme , lakini uanzishwaji wa Wakala wa Umeme Vijijini umeongeza wigo wa usambazaji wa umeme kwa wananchi waishio vijijini.

Kutokana na umuhimu wa nishati hiyo kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ikiwamo elimu, ipo haja ya sekta ya elimu kupata upendeleo wa kipekee katika usambazaji wa huduma hiyo.

Katika muktadha huo tunashauri REA kuwa na mpango wa kuziunganisha taasisi za umma na umeme, kwa kuanza shule za msingi na sekondari.

Aidha baada ya hapo ifikishe kwenye zahanati, vituo vya afya, maduka ya dawa ya MSD na vituo vya kusukuma maji . Upo umuhimu wa shule kuwa na umeme kwa sababu baadhi ya shule za msingi na sekondari hasa za kata zilizopo vijijini hazijaunganishwa na umeme. Ukosefu wa nishati hii katika shule nyingi unakwamisha maendeleo ya taaluma.

Hivyo basi, katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo inayosimamiwa na REA kwenye vijiji na maeneo mbalimbali ya nchi ni muhimu shule za msingi na sekondari ambazo hazijaunganishiwa umeme zikapewa kipaumbele.

Wakala REA asiishie tu kutoa kipaumbele cha kuziunganishia kaya umeme lakini pia utoe kipaumbele kwa shule ambazo bado hazijaunganishwa na nishati hiyo ili kuongeza kasi ya ujifunzaji na ufundishaji shuleni. Baadhi ya walimu wamejiwekea mikakati ya kumaliza mapema mada zinazopaswa kufundishwa ili wapate muda wa kutoa mazoezi na majaribio ya kutosha kwa wanafunzi wao. Lengo ni kuongeza ufaulu na kuboresha viwango vya ufaulu na uelewa.

Miongoni mwa mikakati ya kufanikisha haya ni kufundisha muda wa ziada. Hivyo kama shule zitakuwa na umeme, mwalimu atakuwa na uwezo wa kuwafundisha wanafunzi wake nyakati za usiku ili kutimiza azma yake hiyo.

Upo umuhimu wa wakurugenzi wa halmashauri nchini kuzitambua shule ambazo bado hazijaunganishwa na umeme. Baada ya kuziainisha shule hizo, taarifa hiyo iwasilishwe kwa Meneja wa Tanesco wa Wilaya na Mikoa ili miradi mbalimbali ya umeme inapotekelezwa, shule zipewe kipaumbele.

Wanafunzi wengi wanakosa utulivu wa kujisomea wanaposoma nyumbani kwao. Hivyo, kama shule zao zitaunganishwa na nishati ya umeme, watavutiwa kujisomea shuleni kwao wakati wa usiku ikibidi kufanya mijadala.

Baadhi ya wanafunzi wanaishi jirani na shule wanazosoma, hali inayowafanya kuwa na uwezo wa kwenda kujisomea shuleni. Kama shule itakosa umeme, ni dhahiri watashindwa kujisomea shuleni kwao.

Pia zipo zana za ufundishaji ambazo zinahitaji nishati ya umeme katika ufundishaji wake, mathalani kompyuta na projekta. Kutokana na umuhimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) katika kufanikisha ujifunzaji bora, shule ni lazima ziunganishwe na umeme ili kwenda na wakati wa sasa wa sayansi na teknolojia tulionao.

Pia wapo walimu wa shule za msingi na sekondari wanaomiliki projekta na kompyuta zao ambazo ni nyenzo muhimu ya ufundishaji, lakini kwa kukosa umeme wanashindwa kuzitumia.

Hivyo basi, katika utekelezaji wa miradi ya umeme hasa umeme wa REA, shule ambazo hazijaunganishwa zipewe kipaumbele, kwa awamu za umeme zijazo.

Aidha, wapo wadau na wahisani wa elimu ambao wanaweza kuchangia vifaa vya umeme vya ufundishaji na ujifunzaji kama kompyuta na projekta lakini kwa kuona baadhi ya shule hazijaunganishwa na umeme wanaweza kusita kutoa misaada hiyo. Na kama wataamua kutoa vifaa hivyo, itakuwa ni ngumu kutumika kwa sababu ya ukosefu wa nishati ya umeme shuleni, jambo linalokwamisha malengo ya msaada huo.

Michael Kavavila, Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Chibalahwe wilayani Kongwa, anashauri serikali kuweka mkazo wa kuziunganishia shule umeme kwani nishati hiyo ina umuhimu mkubwa katika kuinua taaluma.

Kavavila anasisitiza: "Kama shule zitaunganishwa umeme hasa za vijijini, walimu wengi watavutiwa kufanya kazi maeneo hayo. Pia wanafunzi wengi wataweza kujifunza kupitia vyanzo mbalimbali ikiwamo mtandao na runinga".

Wakati ni huu kwa shule zetu kuunganishiwa umeme. Hata mradi wa Stiegler's Gorge wa megawati 2,100 utakapokamilika uzikumbuke pia shule jicho lisibakie kwa viwanda pekee. Tafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: 0764666349**



Na Elizabeth Zaya

NYUMBA YANGU

# Inakuwaje kamba hazina viwango?



Uanikaji huu wa nguo unachafua badala ya kupamba au kupendezesha makazi na mazingira.

UTUNZAJI wa mazingira ya nyumba ni uwanja mpana ambao unabeba mambo kadhaa yanayohusisha moja kwa moja ustawi wa nyumba na ubora wa makazi na mahali tunapoishi bila kusahau eneo lote linaloizunguka nyumba.

Nje ya nyumba yapo mambo mengi ambayo huzunguka makazi, iwe ni kwa ajili ya mapambo ya nyumbani au yanayohusu matumizi ya wakazi wanaoishi humo , hapa kuna bustani, mabanda ya mifugo wakiwamo mbwa, matangi au visima vya maji na vyoo vya nje.

Yote kwa yote lazima kila kitu kilichomo ndani ya eneo tunaloishi ni kiwekwe katika mazingira sahihi ambayo hayawezi kuharibu muonekano au mvuto wa nyumba.

Leo nizungumzie namna ambavyo tunaweza kutengeneza kamba ndani ya ua wa nyumba kwa ajili ya kuanikia nguo za familia.

Ikumbukwe kuwa kamba hii ni miongoni mwa mahitaji muhimu kwa matumizi ya watu wanaoishi ndani ya nyumba kwa vile kufua nguo kunafanyika mara kwa mara haijalishi ni kila siku , baada ya wiki au hata baada ya siku mbili au kila mwisho wa wiki.

Suala hili tunaweza kuliona kwamba ni jambo la kawaida, lakini binafsi kutokana na tathimini ambayo nimeifanya katika baadhi ya nyumba nimeona ni vema nalo nilizungumzie ili kukuongezea maarifa na uelewa mpana wa kuboresha nyumba zetu.

Katika baadhi ya nyumba ambazo nimebahatika kupita nimejifunza jambo moja ambalo baadhi tunashindwa kulizingatia nalo ni kupenda kufunga au kutengeneza sehemu mahususi ya kuanikia nguo. Badala yake tuinafunga kamba shaghala baghala na kuharibu muonekano wa nyumba.

**Hali hiyo ni uchafu badala ya urembo kwani wakati mwingine hata wageni wanapoingia nyumbani wanakutana na nguo zimezagaa chini badala ya kukaribishwa na bustani za maua na vivutio vingine.**

Inatokea mtu ana nyumba nzuri, lakini anashindwa kutafuta sehemu ya kuweka kamba ya kuanikia nguo hizo, badala yake baadhi wanaziweka hata mbele ya lango kuu la kuingilia kwenye nyumba.

Hali hiyo ni uchafu badala ya urembo kwani wakati mwingine hata wageni wanapoingia nyumbani wanakutana na nguo zimezagaa chini badala ya kukaribishwa na bustani za maua na vivutio vingine.

Jambo jingine ambalo tunapaswa kulitambua mbali na kuchagua sehemu ya kuwekea kamba kwa ajili ya kuanikia nguo, ni lazima pia tuwe na kamba bora.

Baadhi wanaweza kudharau hili, lakini kamba bora na imara zinapofungwa katika nyumba hata kama hazijaanikiwa nguo zinapendezesha nyumba.

Hivyo usiweke bora kamba eti kwa kuwa zinafichwa na nguo. Unakosea, badilika kuanzia sasa.

Baadhi ya kamba kutokana na ubaya au kwa sababu zinaachwa na kuchakaa sana, zinapokuwa hazijaanikiwa nguo huharibu na kuacha muonekano mbaya wa nyumba au kufanana na uchafu.

Unaweza kuona watu wanavyodharau kamba, mfano wapo wanaounganisha unganisha kamba za rangi za ajabu wapo wanaotumia vipande vya nguo au manila pamoja na mkonge na hivyo kuleta picha mbaya au kuonekana kama uchafu.

Pia ukiacha uzingatiaji wa mvuto wa kamba, lakini pia unaweza kutafuta eneo ambalo hata ukifunga kamba haziwezi kuharibu muonekano wa nyumba hususani katika eneo la uani au la nyuma ya nyumba ambako watu hawapiti au kuingilia huko mara kwa mara.

Fikiria kama kamba zimeungwaungwa namna hiyo au zimechoka na kuchakaa unaipendezesha au kuchusha nyumba?



:Iwapo una eneo dogo waweza kuweka kamba ukutani na kuipendezesha nyumba lakini pia ukiboresha usafi wa makazi. **PICHA: MTANDAO.**

### UFUNGAJI KAMBA

Kuna aina nyingi za utengenezaji au ufungaji wa kamba za kuanikia nguo, unatakiwa kuzifunga kwenye bomba au nguzo za vyuma.

Aidha hakikisha kuwa kama inawezekana unasimamisha bomba au vyuma vitatu ili kufunga kamba hiyo. Kuna bomba au nguzo ya kulia na kushoto na katikati ili kuziongezea kamba uimara.

Ni vizuri kila unapopaka rangi ya nyumba ukapaka na bomba za kamba ili kuleta mfanano na mvuto zaidi.

Bomba hizo unazisimamisha kwa zege na si kuzichimbia chini kama unayepanda mche. Hakikisha unazichimbia chini na kufunga kamba kikamilifu ili nguo zisidondoke.

Ni vizuri kuweka kamba eneo ambalo watu hawapiti ili kuepusha kuchafuliwa. Weka kamba pembezoni mwa eneo ambalo watu hawapita.

Usiweke kamba mlangoni au njia ya kwenda kwenye choo cha nje au bafuni, kisimani au usizifunge sehemu ambayo watu wanapita iwe ni kwenda kwenye shughuli nyingine kama jikoni hasa kwa jiko la nje au nyumba ya mifugo.

Kama eneo lako ni kubwa tenga sehemu maalumu ya kuweka kamba za kuanikia nguo zako. Unaweza kuweka bustani ya maua pembeni ila hakikisha maua hayakwamishi mtu anayekwenda kuanika nguo.

### UKUTANI

Unaweza kufunga kamba ukutani. Unanunua kamba na vyuma kisha tafuta fundi wa kuzipachika ukutani . Hii inafanyika kwa wakazi wa ghorofani na wale wanaoishi kwenye eneo finyu. La msingi ni kuhakilisha unaweza kuzifikia kuanika na pia kuanua nguo.

Zama hizi vifaa kama kamba na mabomba ya kuzifunga yanauzwa hivyo ni rahisi kuzipata kwenye maduka ya vifaa vya ujenzi. Cha msingi ni kuhakikisha kuwa unafunga kamba kwenye eneo lenye jua la kutosha kwa sababu lengo ni kuanika nguo sehemu zinapokauka na jua.

### KAMBA

Ni vizuri kutafuta kamba za nyaya za chuma. Hizi hazipati kutu wala hazichafui wala kuchubua nguo. Kamba za mkonge au manila zinaweza kutumiwa lakini zinatoa rangi na kuchafua nguo.

Epuka kuwa na kamba ambazo zitaharibu au kuacha rangi ya kutu kwenye nguo. Ni vyema pia kuwa na kamba ndefu kwenda juu ili nguo kubwa hasa pazia , shuka, nguo nzito hasa taulo zisishuke chini.

Kuna baadhi ya watu wanatumia nyaya nyeusi za mpira za simu kuanikia nguo zao . Mara nyingi hizi hulegea na kukatika , lakini kama zinapatikana zinaweza kutumiwa pia.

Unapoanika nguo futa kamba kuondoa vumbi kumbuka kuwa zipo nje na huchafuliwa na upepo, ndege kama kunguru na wengine wanaopenda kutua juu yake.

Na Marry Geofrey

# MOI HAISHIKIKI

## ■Yajizatiti kila idara tiba za kibobezi, hutoa nusu kaputi kisasa, upasuaji kichwa, kukarabati nyonga ....

UWEKEZAJI kwenye sekta ya afya unatajwa kuwa umeleta mafanikio makubwa kwa Tanzania. Baadhi ya masuala yaliyofikiwa ni kuhakikisha kuwa idadi kubwa ya wagonjwa wa rufani waliokuwa watibiwe nje kwa gharama kubwa wanahudumiwa nchini kwa weledi.

Taifa linajinasibu kuwa watu wengi wametambua na wanatibiwa kupitia Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF). Aidha , hospitali na kliniki za kisasa zimejengwa na huduma za kibingwa zinapatikana kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Hospitali hiyo ina madaktari bingwa wabobezi (super specialty) wakiwamo wa figo, moyo, mifupa pamoja na mishipa ya fahamu na fahamu.

Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), ni eneo mojawapo lenye huduma za kibobezi na za kibingwa nchini ambalo upasuaji wa mifupa, tiba za dharura za mifupa, mishipa ya fahamu na uondoaji vivimbe hufanyika . Inajivunia kuokoa maisha ya wagonjwa wakiwamo wa ajali mbaya na wa rufani.

"MOI leo inasifika kwa huduma bora na ina uwezo wa kuwafanyia upasuaji wagonjwa 1,000 kila mwezi baada ya kuboresha huduma zake kikamilifu. Tofauti na awali ambapo ilikuwa inapasua wagonjwa 500 hadi 700 kwa mwezi", anaeleza Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface

Anasema maboresho yaliyofanyika MOI ni ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli.

Dokta Boniface, anawatajia mafanikio hayo Maofisa Mawasiliano wa Taasisi za Wizara ya Afya, katika ziara yao ya kukagua uboreshaji wa sekta hiyo, chini ya kauli mbiu inayosema 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Akizungumza na maofisa hao jijini Dar es Salaam hivi karibuni, anasema idadi ya wagonjwa imeongezeka kutokana na kujengwa vyumba zaidi vya upasuaji na kuwa na wataalamu katika kipindi hicho cha miaka mitatu.

Anasema vimeongezeka kutoka sita hadi tisa na hivyo idadi ya wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji imekuwa maradufu.

"Awali MOI ilikuwa inawafanyia upasuaji wagonjwa 500 hadi 700 lakini baada ya ongezeko MOI inafanya upasuaji kwa wagonjwa 700 hadi 1,000 kila mwezi," alisema Dk. Boniface.

### WATOTO VICHWA VIKUBWA

Dokta Boniface anawaeleza wadau hao kuwa kati ya vyumba tisa vya upasuaji vilivyopo MOI kimoja kimetengwa kwa ajili ya watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, lengo ikiwa ni kuhakikisha watoto wanapata huduma kwa wakati ili kuokoa maisha yao.

Anasema maeneo waliyoboresha katika kipindi cha miaka hiyo mitatu ni utoaji wa huduma za tiba ya mifupa, majeruhi na magonjwa ya ajali, upasuaji wa ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu.

Dokta Boniface anasema serikali ilitoa Sh. bilioni 16.5 kwa ajili ya kukamilisha mradi wa awamu ya tatu ya MOI na kununua vifaa vya kisasa.



Mtaalamu wa radiolojia wa MOI Ngina Mitti (kulia), akitoa ufafanuzi wa namna x-ray ya CT scan inavyofanya kazi kwa maofisa mawasiliano wa taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Afya (hawaonekani pichani). Pamoja naye ni Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi.

Aidha, anasema imeiwezesha MOI kununua vifaa vya kisasa vya uchunguzi vya MRI, CT scan, X-ray za kidijitali na X-ray zinazohamishika (portable) ambazo zinatumika kuwafuata wagonjwa wasiojiweza wodini.

Kadhalika, anawaeleza kuwa kuna mashine za utrasound pamoja na vifaa vingine vya uchunguzi ambavyo vinawafuata wagonjwa waliolazwa wodini badala ya wagonjwa kufuata huduma hizo kwenye vyumba maalum vya uchunguzi. "Awali wagonjwa walilazimika kufuata vipimo hivi vikubwa katika hospitali za binafsi. Lakini pia kwenye wodi maalum na inakadiriwa wagonjwa 25 hadi 30 wanapata huduma hii ya uchunguzi kwa kifaa cha MRI pekee kila siku," anaeleza.

Kwa upande wa huduma za vyumba vya upasuaji, anasema taasisi hiyo imenunua vitanda vipya tisa vya kisasa kutoka Ujerumani vinavyowezesha madaktari kutekeleza vyema jukumu lao la kuwafanyia upasuaji Watanzania wenye uhitaji.

"Pia taasisi imenunua vifaa vingine vya chumba cha upasuaji na ICU vijulikanavyo kama patient monitors na ventilators na huduma mpya tunazotoa MOI katika kipindi cha miaka mitatu ni kufanikiwa kuanzisha tiba mpya za kibingwa za upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu."

Anasema pia wanafanya upasuaji wa kunyoosha viungo kwa watoto, upasuaji wa kuondoa vivimbe kwenye mishipa ya damu, ubongoni na upasuaji wa mgongo kwa kufungua eneo dogo.

### HUDUMA ZA KIBINGWA

Mkurugenzi Boniface anasema: "Taasisi imeendeleza huduma za kibingwa za kupandikiza nyonga na goti bandia pamoja na upasuaji wa kurekebisha mfupa wa kiuno kutokana na serikali kuimarisha upatikanaji wa vifaa tiba vya kisasa zaidi," anasema.

Anasema mafanikio zaidi yamepatikana kwenye kuanzisha wodi mpya ya kuwalaza wagonjwa na kufanyia upasuaji siku hiyo hiyo na kwamba miezi ya Novemba na Disemba mwaka jana imeshuhudia zaidi ya wagonjwa 150 wakifanyiwa upasuaji huo.

"Huduma hii mpya na ya kipekee ambayo haipatikani katika hospitali yoyote ya umma hapa nchini imelenga wagonjwa wenye maumivu ya goti, bega na vivimbe sehemu mbalimbali mwilini," anasema Dk. Boniface.

Anaeleza zaidi kuwa, lengo la huduma hiyo ni kuhakikisha wagonjwa wanapata matibabu bora na kwa wakati badala ya kuzungushwa muda mrefu kusubiri foleni.

Anasema pia huduma nyingine ni ongezeko la vitanda vya ICU kutoka nane vya awali hadi 32 na vitanda 16 vitakuwa ICU na vingine ni huduma ambayo haikuwepo hapo awali.

Kadhalika, Taasisi imeanzisha huduma ya vyumba vya kisasa vya kulipia kwa wagonjwa wakulipia ambao pia wanapata huduma mbalimbali.

### NUSU KAPUTI KISASA

Tiba za upasuaji wa kisasa, zimeendelea kutumiwa MOI kwa kuachana na mazoea ya kumpa mgonjwa nusu kaputi inayomlaza uzingizi mzito badala yake dawa ya usingizi huwekwa eneo la upasuaji pekee, anaeleza Dk. Boniface.

Huduma hiyo ya kutoa dawa za usingizi eneo linalofanyiwa upasuaji pekee inahakikisha kuwa dawa inatolewa kwenye eneo hilo pekee ili kuzuia mishipa ya fahamu yote kulala.

Kwa mbinu hiyo badala ya kumlaza mgonjwa usingizi muda mrefu hivyo kumfanya kuwa macho kwa muda na kuendelea na shughuli zake kama kuzungumza na kusoma gazeti.

Dk. Boniface anasema huduma hiyo inaanzishwa nchini kwa mara ya kwanza na wakufunzi wawili kutoka Chuo Kikuu cha Latvia cha nchini Latvia ambao watatoa mafunzo hayo ya kibingwa kwa madaktari bingwa wa MOI na waliopo mafunzoni kwa siku 10.

"Huu ni mwendelezo wa mafunzo ambayo tulishayaanzisha kwa madakatari wetu, lengo kubwa la mafunzo haya na ujio wa wakufunzi hawa ni kuhakikisha huduma hii inaendelea kutolewa hapa MOI," anasema Dk. Boniface na kuongeza kuwa,

"Ni mbinu bora na salama ya kumlaza mgonjwa kwa ajili ya upasuaji, mgonjwa anaweza kufanyiwa upasuaji huku anasoma kitabu na baada ya upasuaji kama mgonjwa hapati maumivu makali anaweza kuruhusiwa kwenda nyumbani siku hiyo hiyo."

Dk. Boniface anasema pamoja na wakufunzi hao kutoa mafunzo, MOI itasaini mkataba wa ushirikiano na chuo hicho kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika utoaji wa huduma za kibingwa za usingizi.

"Kwa kuanza tutasaini mkataba wa ushirikiano wa miaka mitatu utakaowezesha watalaamu kutoka chini kupata fursa ya kujifunza kwenye chuo chao lakini pia watakuja hapa kutoa mafunzo ya muda mfupi kama ambavyo hawa wamekuja," anasema Dk. Boniface.

Kwa upande wake Profesa Alex Miscuks kutoka Chuo Kikuu cha Latvia, anasema ni heshima kupata fursa ya kuja nchini kubadilishana uzoefu na madaktari bingwa wa MOI.

Anasema kwa kutoa huduma kwa pamoja na kutoa mafunzo atapata fursa ya kujifunza mambo mengi yatakayokuwa na manufaa kwao.

"Nashukuru sana kwa kunialika, nimefurahi kukutana na madaktari wazuri na wazoefu hapa MOI, naamimi mimi pia nitajifunza mambo mengi kwenu," anasema Profesa Miscuks.

Kwa upande wake Dk. Iveta Gobovska, ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha Wagonjwa Mahututi katika hospitali ya Chuo Kikuu cha Latvia, anasema amefarijika kupata fursa ya kuja kubadilishana uzoefu na madaktari wa Tanzania na anamini pande zote mbili zitanufaika na mafunzo hayo.



Madaktari wabobezi wa upasuaji ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu wa MOI wakishikiana na wenzao kutoka Chuo kikuu cha Weill Cornell cha Marekani kuondoa vivimbe kwenye mishipa ya damu ubongoni kwa kutumia darubini ya kisasa. **PICHA ZOTE: MOI.**

MAKALA

# Kuboresha miundombinu Tanesco kunavyochochea kujenga viwanda

**Na Joseph Mwendapole,**
ARUSHA




Baadhi ya wafanyakazi wa kiwanda cha nguo cha A to Z wakiwa kazi wakati wahariri wa vyombo vya habari nchini pamoja na maofisa wa Tanesco, walipofanya ziara kiwandani hapo kuona shughuli za uzalishaji pamoja na hali ya upatikaji umeme.



Mkurugenzi Mkuu wa Tanelec , Zahir Saleh akiwaongoza wahariri wa vyombo vya habari pamoja na maofisa Tanesco kuingia kwenye kiwanda hicho cha kuzalishaji trasfoma kilichoko mkoani Arusha. **PICHA ZOTE NA JOSEPH MWNDAPOLE**

HIVI karibuni Shirika la Umeme (Tanesco), limefanya mageuzi na marekebisho makubwa ikiwamo kuweka mitambo mipya ili kuwa na mfumo na miundombinu madhubuti ya umeme. Hizi ni jitihada zinazolenga kufikisha huduma za uhakika za nishati hii kwa wateja wake.

Tanesco inatimiza azma hiyo kwa kutekeleza mradi mkubwa wa kukarabati, kuimarisha miundombinu na mifumo ya umeme ya shirika hilo nyeti nchini.

Wiki hii shirika hilo limeandaa ziara ya wahariri kutembelea miradi inayotekelezwa na Tanesco mkoani Arusha. Ili kufahamu hatua mbalimbali za uwekezaji huo Nipashe inazungumza na Mhandisi Mwandamizi, anayesimamia miradi, Emmanuel Manirabona kuhusu mradi huo unaofahamika kama Tanzania Energy Development Access and Expansion Projects (TEDAP).

Manirabona anasema kukamilika kwa mradi huo kumeleta manufaa makubwa kwa Watanzania, wawekezaji wakubwa, wadogo na wa kati ambao kwa sasa wana uhakika wa umeme saa 24.

Mhandisi anasema kupitia mradi huo ambao ulifadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), Tanesco imeweza kuifanyia marekebisho mitambo mingi na kuweka mipya kila ilipohitajika hali ambayo imewezesha kuwa na umeme wa uhakika.

Anabainisha kuwa hata malalamiko ya kukatikakatika kwa umeme kutoka kwa wateja yamepungua sana kutokana na kukamilika kwa mradi huo wa TEDAP, ulioanza kutekelezwa tangu mwaka 2012 na kukamilika mwaka 2017-2018.

"Hivi sasa ukienda kwenye ofisi za Tanesco huwezi tena kuona misururu ya wateja wakipeleka malalamiko au matatizo yanayohusu shirika na hii yote ni kutokana na maboresho makubwa ambayo yamefanyika na kusimika mitambo ya teknolojia ya kisasa," alisema.

Anaongeza kuwa shirika limeweka mifumo ya kisasa ambayo kila inapotokea hitilafu huibaini mapema kabla ya wateja kwenda kulalamika na mafundi wa shirika kwenda haraka kutatua tatizo lililopo tofauti na kabla ya utekelezaji wa mradi huo.

Mhandisi Manirabona anasema Tanesco haipendi kuona mteja anakatikiwa umeme au kukosa kabisa nishati hiyo hivyo ndiyo sababu iliamua kutekeleza mradi huo mkubwa uliohusisha ununuzi wa mitambo na mashine mbalimbali zinazotumia teknolojia ya kisasa.

Vituo vingi vya kupoozea umeme nchini vimeongezewa uwezo kupitia mradi huo na vyote vina umeme wa kutosha mahitaji na vimekuwa na njia za umeme za akiba ambazo hazijaanza kutumika, anaongeza mhandisi huyo.

"Ukitembelea vituo vyetu vingi utashuhudia kuna njia za umeme ambazo hazitumiki zinasubiri wateja sasa kabla ya mradi huu wa TEDAP hili halikuwezekana limewezekana tu baada ya kukarabati na kuweka vifaa vya teknolojia ya kisasa kwenye vituo vyetu vyote," anafahamisha.

Anasema kutokana na mabadiliko makubwa yaliyofanyika kwenye shirika hilo hivi sasa akijitokeza mwekezaji yeyote anayehitaji umeme mkubwa kwaajili ya uzalishaji viwandani wanamuunganishia haraka.

Baadhi ya vituo vya mkoani Arusha vilivyonufaika na mradi wa TEDAP ambavyo wahariri walivitembelea ni pamoja na kituo cha Njiro B, Mount Meru, Kiltex, Sakina, Themi na Unga Ltd.

Mhandisi huyo anataja chimbuko la mradi wa TEDAP kuwa ni uchakavu wa miundombinu ya shirika hilo hali iliyosababisha kuwepo kwa malalamiko mengi kutoka kwa wateja ambao walikuwa wakilalamikia kukatikakatikaa kwa umeme.

"Vifaa vya zamani vilisumbua kwa mfano likitokea tatizo ilikuwa mnalazimika kuwasiliana kwa kutumia redio call lakini kwa mitambo ya sasa likitokea tatizo wataalamu wanawasiliana kupitia mfumo wa kisasa uliopo na tatizo linatatuliwa haraka sana tofauti na zamani," anasema.

Anaeleza zaidi kuwa mfumo huo ambao kwa kimombo unajulikana kama System Control and Data Acquisition (SCADA), umerahisisha mawasiliano kwa wataalamu wa shirika hilo kwani kila kitu kwa sasa kinakwenda kidigitali na tatizo linabainika na kutatuliwa mapema sana.

"Hivi sasa likitokea tatizo kwenye gridi kila kitu kinaonekana kwenye kompyuta TEDAP imesaidia sana kuifanya Tanesco ijiendeshe kisasa kwasababu vituo vingi vimeongezewa uwezo na wataalamu wa ndani wamekuwa wanafanya mambo mengi wenyewe bila kutegemea wa nje," anasema.

Shuhuda wa maboresho ndani ya shirika hilo ni Mkurugenzi wa Makampuni ya Lodhia Steel, Sailesh Pandit, ambaye anasema kwa sasa umeme umetulia wanaendesha shughuli za uzalishaji bila tatizo.

Anasema kiwanda chake kinapata Megawati 7 ambao ni wastani wa umeme unaotumika kuendesha baadhi ya mikoa kama Manyara na hajawahi kuwalalamikia Tanesco kuhusu kukatikakatika kwa umeme wala kuwepo kwa umeme mdogo.

"Kusema ukweli sina baya kwa Tanesco tunafanya kazi kwa karibu sana na wenzetu wa mkoa wa Arusha na hata nikipiga simu kwa meneja wa mkoa saa nane usiku atapokea na kama kuna shida atatupa vijana ndani ya muda mfupi watarekebisha kama kuna kasoro,' anasema Pandit.

"Tunaposema Tanzania ya viwanda mimi naamini itawezekana kwasababu tumepata umeme wa uhakika maana kuzalisha nondo inatumia umeme mwingi sasa kama huna umeme wa uhakika huwezi kufanya lolote, Viwanda ni Tanesco na Tanesco ni viwanda" anasema

Pandit anasema kwa uzoefu alionao umeme miaka minne iliyopita ulikuwa unakatika mara kwa mara na kusababisha baadhi ya viwanda kupata hasara ya malighafi lakini baada ya maboresho hayo maisha yamekaa sawa.

"Kuhusu umeme niseme ukweli tu kwamba kwa sasa tuko dunia nyingine kabisa sijawahi kusikia hapa Arusha wenye viwanda wanalalamikia umeme, Arusha mmejipanga vizuri kwasababu mnasikiliza wateja na mnatenda,"

"Nawaomba watu wanaotaka kuja kuwekeza Arusha kwamba huu ni muda mwafaka kwasababu hakuna tena shida ya umeme mimi nalipa bili ya Sh. bilioni 1.1 kwa mwezi kwasababu uzalishaji wa nondo unahitaji umeme mwingi sana," anasema

Meneja Utawala wa kiwanda cha Sunflag Arusha, Magesa Charles anasema umeme wanaopata kutoka Tanesco unatosheleza mahitaji yao ya kila siku na kwa mwezi mzima wanaweza kutumia hadi uniti za umeme zipatazo za milioni 2.1 .

"Lazima tuwapongeze Tanesco kwa kutuletea umeme wa uhakika sisi hapa maboresho waliyoyafanya yametugusa kwasababu hatuna tena malalamiko nao hivyo tunakila sababu ya kuwapongeza," anasema.

"Hata ikitokea tatizo ukawapigia Tanesco Arusha wako vizuri watakuja haraka na kutatua tatizo na kama wanakata umeme kwaajili ya matengenezo wanatuarifu mapema tunajipanga. Kwa ujumla hali imeimarika sana," anasema

Meneja Mkuu wa kiwanda cha kutengeneza transfoma cha Tanelec, Zahir saleh, anasema kutokana na umeme wa uhakika kutoka Tanesco wanazalisha kwa saa 24.

Anasema kwa mwaka uwezo wa Tanelec huzalisha wastani wa transfoma 14,000 na kwa siku zinazalishwa hadi transfoma 30 hivyo ni dhahiri kuwepo kwa umeme wa uhakika ni jambo muhimu kwao.

"Changamoto tunayopata ni ucheleweshaji wa malighafi katika bandari ya Dar es Salaam kwasababu mzigo utakaofika bandari ya Mombasa na Dar es Salaam siku moja basi ule wa Mombasa utafika na utatumika hadi uishe wakati wa Dar es Salaam haujapokelewa ila umeme wa uhakika tunao," anasema

Anasema kuanzia mwaka 2017/2018 umeme haukatiki ovyo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ambako wakati mwingine walilazimika kusimamisha uzalishaji.

## HABARI KIMATAIFA

# Nkurunziza aishtaki televisheni ya Ufaransa

**BUJUMBURA, Burundi**

MAHAKAMA jijini Paris, nchini Ufaransa, imeanza kusikiliza kesi iliyofunguliwa na Rais wa Burundi Pierre Nkurunziza, dhidi televisheni moja ya nchini Ufaransa, mwanasheria wa Ubeligiji na mwandishi wa habari wa Burundi kwa makosa ya kuikashifu nchi yake na kuishushia hadhi yake.

Rais Nkurunziza (pichani) , anaituhumu televisheni hiyo ya Ufaransa miaka miwili iliyopita ilionyesha picha za video za mauaji ya kimbari kwa madai kuwa chama tawala cha Burundi ndicho kilichohusika.

Rais Nkurunziza alidai kuwa televisheni hiyo ya Ufaransa, miaka miwili iliyopita ilionyesha picha za video za mauaji ya watu wengi,na kudai kuwa chama tawala cha Burundi ndicho kilichotekeleza mauaji hayo.

Alisema kuwa picha hizo za video zilizoonyeshwa na televisheni ya Ufaransa ya Channel 3, zilidai mauaji hayo ya watu wengi yalifanyika katika viunga vya makazi ya Rais Nkurunziza jambo linalokanushwa na ambalo kwa sasa limefikishwa mahakamani

Mwandishi wa BBC Prime Ndikumagenge, alisema kuwa, Nkurunziza amekanusha vikali kwamba picha hizo wala si za ndani ya Burundi bali zinavyoonekana ni kama zilichukuliwa mahala fulani katika nchi za Afrika Magharibi.

Televisheni hiyo ya Ufaransa Channel -3 ilizirusha picha hizo mwaka 2016,wakati wa uchaguzi mkuu wa Burundi, ulioandamana na vurugu.Video hizo katika matangazo kupitia televisheni ya France Channel 3, zilionyesha mauaji ya watu wengi,yanayodaiwa kutekelezwa na wafuasi wa Nkurunziza.

Picha hizo za video zimepewa jina la Proof of acts of violence in Burundi"ikimaanisha 'Ushahidi wa vitendo vya ukatili vya Burundi.

Ndani ya picha hizo pia ,baadhi ya watu wanaoonekana wakizungumza lugha ya Kihausa, lugha ambayo haiongelewi nchini Burundi.

Mshitakiwa Bernard Maingai ambaye ni mwanasheria, anatuhumiwa kwamba ndiye aliyepeleka video hiyo ili ichezwe katika runinga na mwandishi wa habari David Gakunzi, anayeshitakiwa na Rais Nkurunziza kwa tuhuma za mahoajiano aliyoyafanya kwenye runinga akizungumzia picha hizo.

Serikali ya Burundi imekuwa ikipata vikwazo kutoka kwa jumuiya za kimataifa, kwa madai ya kukiuka haki za binadamu na kwamba chama tawala nchini humo kina kundi la vijana linaloitwa Imbonerakure.

Hata hivyo serikali ya Burundi imekuwa ikikanusha madai hayo kila wakati.

**BBC**



Wanafunzi wakilia kuomboleza kifo cha mwalimu: **PICHA: DW**

# Mwanafunzi ndani mauaji ya mwalimu

**NAIROBI, Kenya**

MWANAFUNZI wa kidato cha nne nchini Kenya ni mmoja wa watuhumiwa watatu wanaoshikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumuua mwalimu, ambaye kabla ya kufa anadaiwa alimpokonya simu mmoja wa watuhumiwa hao.

Taarifa kutoka shuleni hapo zilieleza kuwa aliyeuawa ni Peter Omari aliyekuwa mwalimu wa Fizikia, aliyeshambuliwa juzi Alhamisi akiwa nyumbani kwake.

Mwalimu huyo alimpokonya mwanafunzi wa kidato cha nne simu ya mkononi aliyokuwa amepewa na watu wawili kwa siri kupitia ua wa shule.

Maofisa wa polisi wanaamini kuwa, watu hao wawili walipanga njama na mwanafunzi huyo kumuua mwalimu Omar kwa nia ya kulipiza kisasi, kwani inasemekana mwaka 2017 watu hao hao walikamatwa wakimpa mwanafunzi mwingine simu ya mkononi.

Chifu anayesimamia eneo la Barut David Kering, alieleza kuwa mwili wa mwalimu huyo ulipatikana usiku wa Alhamisi nyuma ya nyumba yake, dakika chache baada ya kutoka shuleni alikokuwa akisimamia na kufundisha masomo ya ziada.

"Mimi pamoja na maofisa wetu wa polisi tulifahamishwa jana usiku kuwa kuna mwalimu ameuawa katika shule ya Hopewell. Tulifika hapa na kweli tukaupata mwili wa mwalimu ukiwa chini, ukiwa amepasuliwa kichwa kwa kupigwa na kitu kizito," alisema chifu Kering na kuongeza kuwa maofisa wamemkamata mwanafunzi mmoja kutoka shule hiyo na mwingine kutoka shule jirani ambao wanasaidia kwa uchunguzi.

"Kama serikali tutafanya uchunguzi na tuone kwamba waliohusika wametiwa nguvuni na kushtakiwa." Aliahidi chifu huyo.

Eneo palipo shule hiyo limehusishwa na uhalifu mwingi kama dawa za kulevya, vileo na simu za mkononi kati ya vitu vingine vinavyosemekana kuingizwa shuleni humo kwa njia isiyo halali. Vitalis Kahenda, mkurugenzi wa shule hiyo ya Hopewell alieleza hali hiyo kama changamoto kubwa inayowakabili. "Tuna wanafunzi zaidi ya 400, wavulana kwa wasichana ingawa huduma za bweni ni za wasichana pekee. Suala la uhalifu katika eneo hili ni kero kubwa na limeathiri pakubwa." Alilalamika Kahenda.

Mkuu huyo wa shule alisema pia wamelalamika mara kadhaa kwa maofisa wa usalama hasa kuwahusu hao watu wawili ambao walionekana shuleni hapo.

"Sio vileo pekee, hata dawa za kulevya huuziwa wanafunzi wetu, lakini hakuna lolote lililofanywa na maofisa hao. Hatuna udhibiti wa mambo lakini maofisa wa usalama wana kazi kubwa ya kufanya." alilalamika.

**BBC**

# Angola yaruhusu uhusiano jinsia moja

**LUANDA, Angola**

BUNGE la Angola limeifuta sheria ambayo ilikuwa inatafsiriwa kama inapinga mahusiano ya jinsia moja.

Serikali ya nchi hiyo tayari imekataza ubaguzi wa watu kulingana na hali zao za mahusiano ya kingono na kwamba yeyote anayemnyima mtu kazi au huduma kutokana na uhusiano wake wa kimapenzi anajihatarisha kufungwa jela kwa kipindi cha mpaka miaka miwili.

Angola ni koloni la zamani la tatu la Ureno barani Afrika kufuta sheria zinazokataza uhusiano wa kingono wa jinsia moja, nyingine ni Visiwa vya Sao Tome na Cape Verde.

Hata hivyo, hakuna mtu yeyote anayefahamika ambaye alishawahi kufungwa ama kukamatwa kama sehemu ya utekelezaji wa sheria hiyo iliyofutwa. Angola inatazamwa kama nchi ambayo watu wake wengi hawana mtazamo hasi na matendo ya kujamiiana kwa watu wa jinsia moja.

Nchi nyingi za Afrika zina sheria kali zinazopingana na matendo ya ushoga.

Mapenzi ya watu wa jinsia moja yaliharamishwa nchini Uganda chini ya sheria za ukoloni katika kifungu kinachokataza mtu kufanya ngono kinyume na maumbile.

Waziri wa Maadili nchini Uganda, Simon Lokodo, mwezi uliopita alisema shughuli zote za wapenzi wa jinsia moja ni haramu na kinyume na utamaduni wa watu wa Uganda.

Wanaharakati wa kupigania haki za wapenzi ya jinsia moja nchini Uganda walisema kuwa watu walio wapenzi wa jinsia moja wanastahili kuendelea na shughuli zao ikiwa watahitaji kufanya hivyo.

Serikali hatahivyo, ilisema kuwa haitawafumbia macho wale wanaoshabikia mapenzi ya jinsia moja na kujaribu kusambaza harakati hizo zinazotazamwa kuwa za haramu nchini.

Kwa upande wa Kenya mapenzi ya jinsia moja ni kinyume na sheria na mtu anaweza kuadhibiwa kwa kutupwa miaka 14 gerezani.

Mwaka 2006 Afrika ya Kusini ilikuwa nchi ya kwanza Afrika na ya tano duniani kuruhusu ndoa za wapenzi wa jinsia moja. Hata hivyo, si wote wanaokabiliana na hatua hiyo, na nje ya miji mikubwa wapenzi wengi wa jinsia moja wanakumbana na mashambulizi na kutengwa na jamii zao.

**BBC**

HADITHI

AJALI kubwa iliyotikisa nchi inatokea eneo la Mikese mkoani Morogoro baada ya basi la abiria kuungua moto, kuua na watu wengine kadhaa kujeruhiwa. Awali inachukuliwa poa kama ajali za kawaida. Lakini nyuma ya pazia, ni ajali iliyopangwa na muuaji , mwenye akili za kiwendawazimu, akibebwa na hisia za chuki, wivu na kisasi bila kujali madhara kwa watu wengine wasiohusika. Eddy Kamal, mpelelezi makini, anategua kitendawili hiki. Fuatilia kisa hiki....

# Kisanduku Cheusi-32

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

"NILISEMA kuwa kabla sijakuua nitaeleza kila kitu kwako na hata wafanyakazi wangu kila kilichofanywa kijulikane, kuanzia Careen kuuawa hadi kukamatwa kwa wewe mchumba wake. Furaha yangu leo ni kuona wewe unauawa mbele yangu na Careen pia aliuawa nami , kinachofuata baada ya mauaji yako ni kumvisha pete mchumba wangu Lisa."

"Mimi ndiye mmiliki wa Paradise Hoteli. Miaka kadhaa nyuma nilimpokea mrembo mmoja anaitwa Careen. Alikuja kuomba kazi baada ya kumaliza kozi ya uhotelia. Kwa jinsi alivyo mrembo nilimpa kazi haraka sana. Lakini pia nilimpenda na akawa mpenzi wangu.

Baada ya mwaka mmoja akaniambia kuwa ana ndugu yake, pacha mwenzake walikuwa naye kozi moja naye anataka amlete hapo. Hakukuwa na pingamizi, akaletwa Hellen."

Jina la Hellen lilisababisha Eddy kupatwa hasira, lakini iliyoishia tumboni, kwani alijua kabisa kuwa kifo cha mpenzi wake kilitokana pia na hila za Banson. Alijipanga pia kumuuliza juu ya kifo cha Hellen jinsi kilivyokuwa.

"Walifanya kazi kwangu kwa muda wa miaka minne. Lakini tabia ya Careen ilianza kubadilika siku hadi siku. Sikujua ni kwa nini. Mpaka ikafika wakati akaacha kazi bila taarifa na hata nilipokuwa nimempangia nyumba nzima Sinza akawa ametoroka." alisema Mapunda na kunyanyua glasi ya maji huku akimtazama Eddy kwa jicho kali, akionyesha kuwa sababu ya matatizo yote ni yeye kwani mpaka wakati huo bado alidhani anayezungumza naye hapo ni Mayambua.

"Simu zake zote zikawa hazipatikani." Nilichofanya nikaandika ule waraka kwa kutumia kompyuta badala ya mkono kukwepa wavumbuzi wa maandishi kunitia mikononi. Nilimwambia hata kama umekimbia, simu umezima, lakini mimi ni mtu mwenye uwezo na maarufu naweza kukutafuta popote pale na nikakupata."

Eddy aliukumbuka ule waraka aliokuta kwenye mkoba wa mpenzi wake hayati Hellen. Akakumbuka mpaka maneno yaliyoandikwa humo.

'Nilipokupangia umehama. Umehamia kusikojulikana. Simu zako zote nasikia umebadilisha. Unadhania kufanya hivyo sitoweza kukufikishia ujumbe. Hivi we mwanamke unanitafuta nini mimi? Hakuna mtu nisiyemjua, au sehemu ambayo utahamia mimi nikose kufahamu. Nitakutafuta popote pale. Huwezi kuniacha mimi kibwegebwege. Nimepoteza gharama zangu na muda wangu kwa miaka mitano kwako, leo uniache kwenda kuolewa na wajinga wengine. Careen nitahakikisha huolewi kwa gharama yoyote ile.'

"Ujumbe ule nilipouandika nikamwambia sekretari wangu afanye kila njia auweke kwenye mkoba wa Hellen kwani kwa kufanya hivyo utamfikia ndugu yake Careen kwa sababu mpaka wakati huo alikuwa hajui anaishi wapi na tayari kazi ameshaacha."

Ndipo Eddy alipogundua kuwa huenda ujumbe ule haukumfikia mlengwa, au Hellen alipouona alipuuzia kumpelekea pacha mwezake, au alipouona aliona si vizuri kwenda kumpa presha mwenzake ambaye tayari alikuwa amejiandaa kuolewa. "Au hata mwenyewe Hellen hakuuona?" Alijiuliza Eddy ambaye aliukuta kwenye mkoba wa Hellen, lakini kumbe uliwekwa na sektretari wa Benson .

Katika uchunguzi wangu, nilituma watu wakaniambia kuwa anatarajia kwenda Ifakara mkoani Morogoro kwa ajili ya ndoa. Kila nikipiga akili haiji, nikaona chochote nitakachofanya hakitokuwa na mimi moyo wangu hauwezi kuona Careen akiolewa niko hai, nikaona bora tu nimtangulize tukose wote." Mapunda alizidi kueleza.

"Mimi ninavyojua Careen alipata ajali kwenye basi ya Bomoa Trans iliyoungua moto, serikali imethibitisha hilo, sasa wewe hapa unaniambia Careen umemuua wewe, huoni kwamba Mapunda unatudanganya?" Eddy aliuliza swali ambalo nia yake ilikuwa ni kumfungua mdomo na kueleza mkakati mzima aliofanya.

Mapunda aliangua kicheko cha kipesa-pesa kilichochanganyikana na dharau.

"Wewe mtoto mdogo sana, watu wana mbinu za kijasusi hata serikali yenyewe haijui nini kimetokea, na hakuna mtu aliye hai atakayejua hili zaidi ya wewe ambaye tunatarajia kukumaliza muda si mrefu, lakini pia wasaidizi wangu waliotekeleza mpango huo kabambe." alisema kwa kujigamba.

"Mimi siwezi kuamini hadi uniambie nini umefanya vinginevyo basi unajaribu kujigamba ili unionyeshe kuwa umemuua mchumba a'ngu Careen." Eddy alizidi kuchoma utambi.

"Napenda mtu jasiri kama wewe." alisema huku ageuzagauza kiti.

"Uko karibuni kuuawa, lakini unaonekana kama mtu usioogopa chochote, ingawa hiyo haikusaidii sana kutufanya sisi labda tukuone wa ajabu tukusamehe.

**"Ujumbe ule nilipouandika nikamwambia sekretari wangu afanye kila njia auweke kwenye mkoba wa Hellen kwani kwa kufanya hivyo utamfikia ndugu yake Careen kwa sababu mpaka wakati huo alikuwa hajui anaishi wapi na tayari kazi ameshaacha."**

Kwani nilishaapa yoyote aliyesababisha mimi kumkosa Careen, akamrubuni ni lazima nimuue, lakini pia tayari kuna baadhi ya siri zetu unazijua, kwa hiyo hakuna namna, utakufa tu." Alijigamba.

"Ulikuwa mchezo mdogo tu kaka, tulishapata jina la mmoja Careen kuwa anasafiri na basi la Bomoa Trans na ilikuwa ni safari maalum kwa ajili ya kwenda kujiandaa kufunga ndoa. Wakati huo tayari tulishapeleka oda ya kutengenezewa bomu lililotengenezwa kwa petroli na madini mengine kwenye gereji moja ya rafiki yangu sehemu za Mabibo. Kazi hiyo nikamkabidhi Seif. Huyo ndiye mtaalam aliyefanya hivyo shughuli." Mapunda aliposema hivyo alitabasamu.

"Na yeye alifia kwenye basi?" Eddy aliuliza.

"Wewe unamjua Seif vizuri? Huyo ni zaidi ya mafia. Bomu aliliweka kwenye 'breafcase' akapanda nalo basi ambalo Careen alikuwa mmoja wa abiria. Ulikuwa ni mchezo mdogo tu kama kuua nzi au kubaka panzi. Lilipofika Mdaula aliomba ashuke akajisaidia, akiacha kisanduku cheusi karibu kabisa na siti aliyokuwa Careen ili asiwe mmoja wa majeruhi, akashuka kwenda kujisaidia.

Nasikia kuna baadhi ya abiria walishuka kwenda kujisaidia hao walipona, lakini bomu lile lilitegwa kupasuka sekunde 30 sawa na nusu dakika, pale 'fyuzi' itakapofunguliwa na Seif alifanya hivyo akaacha kisanduku akateremka haraka."

Eddy alimtazama kwa mshangao Mapunda kwa jinsi alivyokuwa akielezea kwa madaha, kana kwamba anaelezea mechi ya soka jinsi wachezaji wa timu anayoishabikia walivyokuwa mahiri dhidi ya wapinzani wake, kumbe ni masuala hatari ambayo yamesababisha vifo vya raia wasio na hatia, na wengine kubaki na ulemavu wa maisha.

"Sasa ndugu yangu nikuulize, mtu ameshuka kwenda kujisaidia huku nyuma bomu linapasuka ndani ya kisanduku atakufaje?"

Hapo ndipo Eddy alipokumbuka maelezo ya walishuhudia tukio hilo akiwemo Nassy kuwa wote walioteremka kwenda kujisaidia waliletewa basi lingine, lakini yupo abiria mmoja tu ambaye hakuwepo naye ni yule mtu aliyevaa pama kichwani na suti nyeusi.

Wao walidhani kwa sababu jinsi alivyo alionekana mtu mwenye pesa, hivyo hakuona haja ya kusubiri basi la kuletewa na badala aliondoka kivyake.

Lakini hapo imepatikana uthibitisho kuwa mtu yule mvaa suti aliyeonekana kama ameacha kisanduku cheusi ndani ya basi na kwenda nje kujisaidia ndiye mlipuaji na basi hilo. Jina lake anaitwa Seif.

"Hivi Mapunda, kweli mwanamke uliyempenda kutoka moyoni, unachukua hatua ya kumuua hivi hivi kama mnyama, je ulimpenda kweli?"

"Na ndiyo maana nilimuua. Kwa sababu sikuweza kukubali kushuhudia akiolewa mbele yangu wakati mimi niko hai?"

"Sasa kwa nini hukumuoa tangu awali wakati mmeshakaa miaka minne?"

"Nilimwambia asubiri kwanza, nilikuwa na mambo mengi ya kufanya, lakini yeye aliona kama vile mimi sitaki kumuoa kwa sababu ya umalaya wangu, eti nina wanawake wengi sana ndiyo maana sitaki kuona mapema, mara pesa zinanizuzua. Kusema kweli yeye alitaka kuolewa mapema, mimi nilikuwa sitaki hivyo, na ndiyo maana akakubali kuoana na wewe na sasa nyie wote limewagharimu maisha ."

**Itaendelea Jumamosi**



## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.


### ELIMU/MAFUNZO

**NAFASI ZA MASOMO:** Tanzania research and Career development institute. Reg pwf/041.Certificate na diploma za kilimo,mifugo, na maendeleo ya jamii. Mawasiliano:0767574701/0758753063. www.tracdi.ac.tz


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


### CHETI KIMEPOTEA



**KUSEKWA PETER** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0496-0236 kilichotolewa na JITEGEMEE SEKONDARI mwaka 2014.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CD/TR/RB/498/2019.**

115027002

### CHETI KIMEPOTEA



**WILSON MGOMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.4798-0126** kilichotolewa na shule ya sekondari SHISYETE ,Mwaka 2012 na cheti cha daraja la tatu A.cha chuo cha Ualimu Songea kilichotolewa na mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBI/RB/2253/2018**

115025302

### CHETI KIMEPOTEA



**BEATRICE RAMA MANYAMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index S.0369/0020** kilichotolewa na shule ya sekondari RUVU ,Mwaka 2006. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/RB/070/2019**

115026002

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FATUMA IDDI MASASI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARRER** yenye namba za usajili **T.580 CB2.** Chasis namba ACU **150004869,**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CID/TR/RB/Q60/2019.**

115025002

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FLAVINUS MOMBA MAHITI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SCANIA yenye namba za usajili **T. 244 APS.** Chasis namba **4362217**, engine **4021435** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CID/TR/RB/0411/2019.**

115025102

### KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**ADAM KASSIM ASSIR** wa P.O BOX 117-TANGA anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HUONIAO** yenye namba za usajili **MC 272 AJQ.** Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi. **TAN/TR/RB/219/2019.**

215025902

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**SIMBA MTOTO TRANSPORT LTD** wa P.O BOX 1018- TANGA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SCANIA. yenye namba za usajili **T482 ABF.** CHASSIS Namba. **4384042** na ENGINE Namba. **5722427** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi Taarifa Polisi.**TAN/TR/RB/214/2019.**

15024902


**Uza,**

*Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223311*

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# ARSENAL yajitosa kwa Nkunku wa PSG

**LONDON, England**

ARSENAL imefungua mazungumzo na Paris Saint-Germain kwa ajili ya uwezekano wa kumsajili kiungo, Christopher Nkunku baada ya mpango wao wa kumchukua Denis Suárez kutoka Barcelona kushindikana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ni mmoja wa wachezaji chipukuzi wanaopewa nafasi kubwa ya kung'ara siku za usoni akiwa ametokea kwenye akademi ya PSG, na amecheza mechi 65 kwenye mashindano yote na kufunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho tatu.

Gazeti la Ufaransa la L'Équipe, limeripoti kwamba, Nkunku sasa anaweza kuwa njiani kwenda kujiunga na Arsenal.

Mkataba wake wa sasa na PSG unamalizika mwaka 2020, lakini majaliwa ya Nkunku kuendelea kukaa hapo bado hayajajulikana.

Nkunku anaweza asiwe jina kubwa barani Ulaya, lakini kwa mashabiki wa Arsenal wanamjua kwa sababu walimuona wakati wa maandalizi ya msimu mpya.

Wakati wa mchezo huo, Nkunku alionyesha kiwango cha juu na sasa Unai Emery amemtolea macho.

Tayari Emery ameshasema wazi kwamba hana mpango wa kumsajili mchezaji yoyote kwa mkataba wa kudumu wakati huu wa dirisha dogo la Januari, lakini kwa Nkunku inaweza kuwa tofauti.

# BAYERN

## YAMSAJILI MMAREKANI RICHARDS

**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich wamekamilisha usajili wa Chris Richards kutoka FC Dallas kwa mkataba wa kudumu baada ya kuwa na mafanikio makubwa wakati akicheza kwa mkopo wa miezi sita na miamba hao wa soka la Ujerumani.

Beki huyo wa kati wa Marekani amecheza mechi 20 kwenye mashindano yote kwa kikosi cha Bayern chini ya umri wa miaka 18 tangu alipojiunga kwa mkopo akitokea Dallas Julai 2018.

Bayern imethibitisha kwamba Richards amesajiliwa kwa mkataba wa kudumu, akiwa amesaini kukaa hapo kwa kipindi cha miaka minne na nusu na atakuwa hapo kwenye dimba la Allianz Arena hadi mwaka 2023.

"Tuna furaha kubwa kwamba tumekubaliana kwenye uhamisho wa Chris kutoka FC Dallas," amesema Meneja wa Bayern, Jochen Sauer, akiiambia tovuti ya Klabu hiyo.

"Chris amecheza vizuri kwa kipindi cha miezi sita na ametushawishi kuendelea kubaki nae na sasa yeye ni sehemu ya FC Bayern."

Richards ni mchezaji wa kwanza kujiunga na Bayern akitokea Dallas tangu klabu hizo zilipoanzisha program ya uhusiano wa kuendeleza wachezaji Februari mwaka 2018.

Richards ameichezea Timu ya Taifa ya Marekani chini ya umri wa miaka 20 na kuwa nyota kwenye michuano ya CONCACAF wakati walipoifunga Mexico 2-0 kwenye fainali.



# BRAZIL YAPEWA PERU, ARGENTINA KUIVAA COLOMBIA COPA AMERIKA

**SAO PAULO, Brazil**

MWENYEJI Brazil amepangwa kundi moja na Peru, Venezuela na Bolivia kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Amerika Kusini 2019, Copa America, itakayoanza kutimua vumbi Juni mwaka huu jijini Sao Paulo.



Katika droo iliyotolewa juzi Alhamisi, Argentina ipo kwenye kundi moja na Colombia, Paraguay na mgeni mwalikwa kwenye michuano hiyo, Qatar ambayo itaandaa michuano ya Kome la Dunia mwaka 2022.

Wao Uruguay wapo kundi moja na mgeni mwingine mwalikwa Japan, pamoja na Ecuador na bingwa mtetezi, Chile.

Michuano ya kwanza itaanza kwa Brazil kufungua dimba la Bolivia mjini Sao Paulo Juni 14 na itachezwa katika miji mitano ya Brazil.

Na fainali yake imepangwa kuchezwa jijini Rio de Janeiro kwenye dimba la Maracana Julai 7 mwaka huu.

"Watu wameniuliza kuhusu droo hii na nimesema, ni rahisi na wengine wameniambia niwe makini," amesema kocha wa Brazil, Tite.

"Majukumu yetu ni kucheza kwa kiwango cha juu, kucheza kwa furaha na kujisikia fahari tukiwa tunaiwakilisha Brazil."

"Tunahitaji kucheza vizuri, na hilo ndilo linaloweza kukufanya ukawa bingwa."

Bosi mpya wa Shirikisho la Soka la Brazil, Rogerio Caboclo ameiambia Reuters kwamba majaliwa ya Tite hayategemeani na mafanikio ya Brazil kwenye michuano hiyo.

"Hakuna uhusiano na vitu hivi viwili. Mkataba wake ni wa miaka minne na anatakiwa kuutumia kwa miaka minne. Hata kama hatutakuwa mabingwa."

Brazil haijawahi kutwaa taji la Copa America tangu mwaka 2007 na kocha Tite, ambaye kikosi chake kilitolewa hatua ya robo fainali ya Kombe la Dunia mwaka jana, ana presha kubwa ya kuhakikisha anatwaa taji na timu hiyo.

Argentina, ambayo imefika fainali mara mbili katika michuano ya Copa America iliyopita na zote kufungwa kwa mikwaju ya penalti na Chile.

HABARI MICHEZO

# MOSES
## AJIUNGA FENERBAHCE KWA MKOPO



**ANKARA, Uturuki**

VICTOR Moses ameripotiwa kuwa amekamilisha kufanyiwa uchunguzi wa afya yake na Fenerbahce, ambapo anajiunga na miamba hao wa Uturuki kwa mkopo hadi mwisho wa msimu huu akitokea Chelsea.

Uhamisho huo umekuja baada ya mchezaji huyo raia wa Nigeria mwenye umri wa miaka 28 kucheza mechi mbili tu za Ligi Kuu England msimu huu, akiwa ameshinda kuwapo katika kikosi cha kwanza cha Chelsea chini ya kocha, Maurizio Sarri, na amehitimisha uvumi kwamba alikuwa anarudi katika klabu yake ya zamani ya Crystal Palace.

Sky Sports imeripoti kuwa, Moses amemaliza kufanyiwa vipimo vya afya, na sasa amejiunga rasmi na timu hiyo.


Moses anajiunga na timu hiyo ambayo inayosuasua kwenye Ligi Kuu ya Uturuki, Super Lig, ikiwa katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kucheza mechi 18, na huko atakuwa pamoja na mshambuliaji wa zamani wa Tottenham na Real Madrid, Roberto Soldado, pamoja na mshambuliaji wa Leicester City, Islam Slimani ambaye amekwenda huko kwa mkopo.

Moses alikuwa na mchango mkubwa kwa Chelsea wakati akicheza kama winga wa kulia wakati kikosi hicho kiliposhinda taji la Ligi Kuu England msimu wa 2016/17 chini ya kocha, Antonio Conte, lakini ujio wa Sarri ukamfanya kukosa namba.

Amecheza dakika 176 katika mechi sita za mashindano yote msimu huu, huku akishindwa kupenya kwenye kikosi hicho mbele ya Eden Hazard, Pedro, Willian na Callum Hudson-Odoi.

Hajaanza katika mchezo wowote wa Ligi Kuu chini ya Sarri, na hajawahi kujumuishwa katika kikosi cha kwanza tangu kwenye mchezo wa sare na Liverpool Septemba mwaka jana.

## THIERRY HENRY ATIMULIWA MONACO



**MONACO, Ufaransa**

KLABU ya AS Monaco imemtimua kazi kocha wake, Thierry Henry kutokana na kutoridhishwa na utendaji wake katika kuitafutia mafanikio timu hiyo uwanjani.

Hatua hiyo imetangazwa na AS Monaco kupitia taarifa iliyowekwa kwenye tovuti yake, ikiwa ni siku tano tu tangu ipokee kipigo cha 5-1 kutoka kwa Klabu ya Strasbourg.

Monaco ilikumbana na kipigo hicho Jumamosi iliyopita katika mchezo wa Ligi Kuu Ufaransa na kuwaliza mashabiki wa timu hiyo, na Henry alilazimika kuomba radhi kwa kutumia lugha isiyokubalika dhidi ya mlinzi wa Klabu ya Strasbourg, Kenny Lala kwa kumuita bibi.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa msimu wa 2016-17, wamejikuta wakipata rekodi mbovu ya kushinda michezo mitano kati ya 20 katika msimu huu, tangu Henry alipokabidhiwa mikoba hiyo Oktoba mwaka jana. Wameshinda michezo miwili tu ya Ligi wakiwa na Henry.

Wakati Monaco wakieleza kuwa Henry ataendelea kusimama hadi watakapotangaza uamuzi kuhusu hatma yake ndani ya klabu hiyo, mikoba yake amepewa aliyekuwa msaidizi wake, Frank Passi.

Monaco ndiye mwajiri wa kwanza aliyemkabidhi kikosi cha kwanza Henry anayekumbukwa kwa uwezo wake mkubwa akiwa na klabu ya Arsenal na Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Kazi yake ya awali kabla ya kukabidhiwa Monaco, alikuwa kocha msaidizi wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji iliyoshiriki Fainali za Kombe la Dunia nchini Urusi.

Alijiunga na Monaco Oktoba 13 mwaka jana akichukua nafasi ya Leonardo Jardim, wengi waliweka matarajio makubwa kwake, lakini maji yamemfika shingoni na anasubiri neno la mwisho kutoka kwa muajiri wake.

## SOLSKJAER: POGBA ANAFAA KUWA NAHODHA MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba ana sifa za kuwa nahodha wa Manchester United, kwa mujibu wa kocha wa muda wa kikosi hicho, Ole Gunnar Solskjaer.

Pogba alikuwa nahodha msaidizi wa United kabla ya kocha Jose Mourinho kumvua wadhifa huo mwanzoni mwa msimu huu kutokana na kutoelewana kwao.

Kiungo huyo mwenye miaka 25 alivaa kitambaa cha unahodha msimu huu katika mechi tatu wakati Antonio Valencia alipokuwa majeruhi. Hata hivyo, alivuliwa madaraka hayo Septemba mwaka jana.

"Namjua kijana huyu (Pogba) kwa muda sasa na ni kiongozi," amesema Solskjaer, ambaye alimfundisha Pogba akiwa kinda kati ya miaka ya 2008 na 2010.

"Ana ushawishi mkubwa mbele za watu. Anajali na ana uchu wa mafanikio."

Maisha ya Pogba nje ya uwanja yamekuwa yakisimangwa, sawa na namna anavyotembea kwa madaha kabla ya kupiga mikwaju ya penalti msimu huu.

Lakini masimango hayo yanaonekana kugonga mwamba, na kiwango chake mchezoni kimeimarika maradufu toka Solskaer alipochukua mikoba ya Mourinho aliyetimuliwa Desemba mwaka jana.

Katika mechi sita chini ya Solskjaer, Pogba amefunga mabao matano na kupiga pasi za mwisho zilizozaa magoli manne.

"Paul ana mbwembwe nyingi pia, lakini hivyo ndivyo alivyo," amesema Solskjaer.

"Mitandao ya kijamii ni sehemu ya maisha tunayoyaishi kwa sasa. Ndiyo jamii ya leo. Tuna kanuni kadhaa, lakini sina tatizo na mitandao."


Mustakabali wa nahodha Valencia hapo kwenye dimba la Old Trafford ni finyu, na tangu Septemba mwaka jana amecheza mechi moja tu ya Ligi Kuu England.

Wakati Valencia akiwa nje, na Pogba kuvuliwa madaraka, Mourinho alimkabidhi mikoba ya uongozi, Ashley Young na Solskjaer hana mpango kwa sasa kufanya mabadiliko.

"Yeye (Young) ni aina ya mwisho ya kizazi cha manahodha wa kizamani," amesema Solskjaer. "Ni muhimu kutokuogopa kusimama mbele ya wachezaji wenzako na kuwakosoa pale inapobidi."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MATA AKARIBIA KUTUA BARCELONA

**Juventus, PSG nazo zatajwa kuwania saini ya Mhispania huyo...**

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imeanza mazungumzo na Juan Mata ambaye kwa sasa hana namba kwenye kikosi cha kwanza cha Manchester United ilimsajili kiungo huyo kama mchezaji huru katika kipindi cha majira ya joto.

Kiungo mchezaji huyo Mhispania ameshindwa kufurukuta katika kikosi cha kocha wa muda wa United, Ole Gunnar Solskjaer, huku raia huyo wa Norway akijipanga kuifufua upya safu ya ushambuliaji.

Mata, ambaye mkataba wake na klabu hiyo ya Old Trafford utamalizika katika kipindi cha majira ya joto, kwa sasa anawaniwa na mabingwa hao wa La Liga, Barcelona ambao wanalazimisha kuingia naye makubaliano ya awali. Gazeti la Goal limeripoti kuwa, vigogo hao wa Catalan tayari wameshafanya mawasiliano na mwakilishi wa Mata na kueleza wanamhitaji nyota huyo ambaye aliwahi kuzichezea Chelsea na Valencia.

Pia kuna taarifa kwamba Juventus ya Italia na Paris Saint-Germain ya Ufaransa nazo zinamwania Mata kama mchezaji huru endapo atashindwa kufikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na United.

United au Mashetani Wekundu wako katika mazungumzo na Mata lakini hadi sasa hakuna makubaliano ambayo yamefikiwa katika majadiliano yaliyofanyika. Kwa sasa mchezaji huyo anaweza kusaini mkataba wa awali na klabu yoyote atakayoridhia kufanya hivyo.

Mapema mwaka jana, United ilifanikiwa kumpa mkataba wa mwaka mmoja kiungo huyo ambao utamalizika ifikapo Julai mwaka huu.

Inaelezwa kuwa Mhispania huyo analipwa mshahara wa pauni 140,000 kwa wiki katika klabu hiyo ya Old Trafford lakini Barcelona inatajwa imejipanga kumlipa kiasi kikubwa zaidi lakini ikiwa haitaki kulipa ada yoyote ya usajili.

Mata alijiunga na United Januari mwaka 2014 akitokea Chelsea na kwa muda wote aliokaa hapo ameichezea timu hiyo michezo 208 katika mashindano mbalimbali.

Kwa muda wa miaka mitano aliyokaa katika klabu hiyo, Mata amefanikiwa kufunga mabao 44 na akitengeneza nafasi 35.

## KWA UFUPI

### DE LIGT KUTUA CITY
MANCHESTER City imeweka wazi nia yake ya kutaka kumsajili beki wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt (19), na usajili huo unamaanisha kuwa beki wa kati ya Argentina, Nicolas Otamendi (30), anakaribia kujiunga na Barcelona. ***(Sun)***

### UNITED YAMWANIA BERTA
MANCHESTER United wanajiandaa kumwajiri Mkurugenzi wa Michezo wa Atletico Madrid, Andrea Berta lakini klabu hiyo ya Hispania imempa ofa nono mpya Mtaliano huyo ambaye sasa ana umri wa miaka 47. ***(Mirror)***

### JARDIM KUREJEA MONACO
UONGOZI wa Monaco umekubaliana kumrejesha kocha wake wa zamani, Leonardo Jardim kuchukua nafasi ya Thierry Henry, ikiwa imepita miezi mitatu tangu atimuliwe kazi katika klabu hiyo. ***(L'Equipe - in French)***

### MONCHI KUMFUATA EMERY
MKURUGENZI wa Soka wa Roma, Monchi anajiandaa kujiunga na Arsenal katika kipindi cha majira ya joto ili kuwa Mkurugenzi wa Ufundi mpya baada ya kuwahi kufanya kazi na Kocha wa timu hiyo maarufu Gunners, Unai Emery katika klabu ya Sevilla. ***(Mirror)***

### CLARKE SOKONI EPL
KOCHA wa Leeds United, Marcelo Bielsa bado hajafanya mazungumzo yoyote na winga, Jack Clarke (18), kuhusiana na hatima yake, licha ya kuwapo kwa tetesi za kuwania na klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu England. ***(Manchester Evening News)***

### LUKAKU KUTUA NEWCASTLE
BEKI wa Lazio na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Jordan Lukaku (24), ambaye ni kaka wa straika wa Manchester United, Romelu anakaribia kujiunga kwa mkopo katika klabu ya Newcastle United. ***(Chronicle Live)***

### ARNAUTOVIC AIMARIKA
MSHAMBULIAJI wa West Ham na Timu ya Taifa ya Austria, Marko Arnautovic amerejea katika mazoezi ya klabu hiyo maarufu Hammers na huenda akapangwa katika kikosi kitakachoivaa AFC Wimbledon kwenye mechi ya Kombe la FA baada ya mchakato wa kwenda kucheza China kuyeyuka. ***(Sun)***

### BEGOVIC AJINADI
GOLIKIPA wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Bosnia, Asmir Begovic (31), amefungua milango wazi kwa klabu za Ligi Kuu England kufanya naye mazungumzo. ***(Sun)***

### KAMARA ATAKIWA UTURUKI
KLABU ya Uturuki iitwayo Malatyaspor bado inasisitiza kumhitaji straika wa Fulham, Aboubakar Kamara (23), licha ya Mfaransa kuwa bado kuwa kilizini kutokana na kupigana na mwenzake walipokuwa mazoezini. ***(Guardian)***

### ROGERIO AGOMBEWA
WOLVES na Southampton zimeweka wazi nia yake ya kumsajili beki wa Juventus na Timu ya Taifa ya Brazil, Rogerio (21), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu ya Sassuolo inayoshiriki Serie A ya Italia.***(Mirror)***

### RODRIGUEZ KUREJEA MADRID
BABA wa kiungo mchezeshaji wa Colombia, James Rodriguez (27), ambaye yuko kwa mkopo Bayern Munich, amesema kuwa mwanae anajiandaa kurejea katika klabu ya wazazi wake ya Real Madrid. ***(Evening Standard)***

### WERNER AIVURUGA RB
RB Leipzig imempa ofa ya mwisho straika wake, Timo Werner (22) ili aweze kubakia katika klabu hiyo na kumaliza ndoto za Liverpool, Barcelona, Real Madrid na Paris St-Germain ambao wameweka wazi nia ya kumtaka Mjerumani huyo. ***(Bild - in German)***

HABARI MICHEZO

# AJIBU ATAMBA YANGA ITAFANYA MAKUBWA FA

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Ibrahim Ajibu amesema kuwa pamoja timu yao kuondolewa katika michuano ya SportPesa ambayo inaendelea hapa jijini Dar es Salaam, bado kikosi chao kina uwezo wa kufanya vyema kwenye mashindano ya Kombe la FA na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ajibu, nahodha mpya wa Yanga, alisema kuwa bado wapo kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu pamoja na Kombe la FA, hivyo nguvu na akili zao wanazielekeza huko.

" Malengo ilikuwa kushinda kila taji, hatujafanya vizuri katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi na Sportpesa, lakini bado tupo kwenye mbio za ubingwa na pia FA, haya ni makombe mawili ambayo tutayapigania kuhakikisha tunafikia malengo yetu," alisema Ajibu.

Mshambuliaji huyo aliongeza kwa kuwataka mashabiki wao kutokuwa na hofu na timu yao, kwa sababu wachezaji wanaahidi kuendelea kupambana katika mechi zilizobakia katika mashindano hayo mawili wanayoshiriki.

Yanga kwa sasa wanaendelea na mazoezi kujiandaa na mchezo wao wa Kombe la FA dhidi ya Biashara United kutoka Mara ambao utachezwa Jumatano ijayo kwenye Uwanja wa Taifa.

Kocha wa timu hiyo, Mwinyi Zahera amesema mchezo huo ni muhimu na watahakikisha wanapunguza machungu yao kwa kuibuka na ushindi.

Zahera alisema hawajafaya vyema katika mechi mbili zilizopita, hivyo huu ni wakati wa kurekebisha makosa yao na kurejesha furaha kwa mashabiki na wanachama wa Yanga.

Mtibwa Sugar ndio bingwa mtetezi wa mashindano ya Kombe la FA ambayo hutoa tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.



Golikipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga akipangua penalti iliyopigwa na kiungo wa Tottenham, Lucas Moura (hayupo pichani) na kuifanya timu yake kuingia hatua ya fainali ya Kombe la Ligi katika mechi iliyochezwa juzi usiku. Chelsea ilisonga mbele baada ya kushinda penalti 4-2.**PICHA: MTANDAO**

# Fountain Gate kukuza vipaji

**Na Renatha Msungu,Dodoma**

SHULE ya Fountain Gate Akademi ya jijini hapa imeteuwa wachezaji chipukizi 30 ambao itawasomesha kwa ajili ya kuendeleza vipaji vyao.

Yosso hao wamepatikana baada ya wachezaji zaidi ya 500 kujitokeza katika usaili ulioendeshwa na kusimamiwa na makocha mbalimbali wenye vyeti vinavyotambuliwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF). Mkurugenzi wa shule hiyo, Japhet Makau alisema kuwa anaamini uamuzi waliouchukua utasaidia kuwaendeleza watoto hao na vile vile baadaye kuisaidia nchi.

"Mipango yetu ni kuendeleza vipaji vya mchezo wa soka, mwalimu wetu Mkuu wa michezo ni Alex Kashasha, tunauhakika hawa vijana watafika mbali katika mchezo huu," alisema Makau.

Wakati huo huo mwanafunzi, Christopher Alex aliyekatwa miguu yote miwili na kupewa miguu bandia na Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ambaye pia anamsomesha anaendelea vizuri.

# TCRA, wasaniii wafikia muafaka

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imewaagiza wasanii walioingia mikataba na kampuni za simu au mawakala kwa ajili ya kutumia kazi zao kama miito ya simu ambao hawajalipwa stahiki zao, wawasilishe madai yao katika ofisi hizo kwa ajili ya kupatiwa haki zao.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Mhandisi James Kilaba, aliyaeleza hayo, muda mfupi baada ya kumaliza kikao na wasanii na mawakala waliokuwa wakijadili kuhusu kutokuwapo na mgawanyo sawa wa malipo ya miito ya simu baina ya wasanii wa muziki, kampuni za simu na mawakala wanaotumia kazi za wasanii.

**Katika kikao hicho, wa likubaliana malipo kuwa kwa kipindi cha miezi sita yakutafuta suluhu ya kudumu, malipo ya kazi za wasanii, mawakala, kampuni za simu na mtoa huduma yawe asilimia 50 kwa 50 kabla ya kuja na mfumo rasmi.**

Aliongeza kuwa wamekubaliana kuwapo uwezekano wa msanii kusaini makubaliano ya kazi zake kutumika kama miito ya simu katika kampuni husika ya simu moja kwa moja na endapo atataka kutumia wakala afanye hivyo.

Pia walikubaliana kuwa kampuni za simu ziwasilishe TCRA mgawanyo halisi wa gharama za utayarishaji wa kazi hizo za wasanii ambazo hutumika kama miito ya simu.

Mhandisi Kilaba, alitaja azimio lingine ni TCRA kuangalia uhalisia wa mikataba inayoingiwa baina ya kampuni za simu na mawakala au wasanii kuona kama ni rafiki katika mazingira ya biashara ya miito ya simu.

"Mpaka mwezi wa June mwaka huu, tutakuwa tumeshaangalia namna ya gharama watakazokuwa wanalipana kati ya kampuni za simu, mawakala na wasanii," alisema Mhandisi Kilaba.

# Makutupora, Dundee, kimeeleweka Dodoma

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

CHAMA cha Soka Mkoa wa Dodoma (DOREFA) imezitangaza timu sita zilizofanikiwa kuingia hatua ya Sita Bora ya Ligi ya Mkoa baada ya kumalizika kwa mechi za hatua ya awali.


Timu hizo ni Makutupora FC na New Dundee United kutoka katika Kituo cha Dodoma Mjini, Ajax FC ( Kondoa), Gunners ( Mji Mpwapwa) na Kanisani FC kutoka Kituo cha Kongwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini hapa, Msemaji wa Dorefa, Alex Mtalika alisema hatua ya Sita Bora inatarajiwa kuanza hivi karibuni kwenye Uwanja wa Mgambo uliopo katika Wilaya ya Mpwapwa. Mtalika alisema hatua ya makundi imemalizika bila ya kuwapo na malalamiko yoyote na hiyo imetokana na waamuzi kuchezesha vyema kwa kufuata sheria 17 za mchezo wa soka.

Kiongozi huyo alizipongeza klabu ambazo zimeingia hatua hiyo huku akizitaka kujiandaa kwa ajili ya hatua hiyo ya pili ambayo itatoa bingwa wa jiji la Dodoma ambaye atapata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa wa mikoa.

# Michezo

Jumamosi Januari 26, 2019
Nipashe



Mata akaribia kutua Barcelona

HABARI UK 30



Beki wa Bandari, Bernard Odhiambo (kushoto), akipambana kumzuia mshambuliaji wa Simba, Emmanuel Okwi katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya SportPesa iliyochezwa kwenye Uwanja vya Taifa jijini Dar es Salaam jana. Simba ilifungwa mabao 2-1. **PICHA: HALIMA KAMBI**

# SIMBA SC, MBAO NAO WACHEMKA

## ●●●Kombe na mamilioni ya SportPesa Cup vyaenda Kenya kwa mara ya tatu mfululizo...

**Na Faustine Feliciane**

KOMBE la mashindano ya SportPesa litaenda Kenya kwa mara ya tatu mfululizo baada ya Bandari FC na Kariobang Sharks zote za nchini humo kufanikiwa kutinga hatua ya fainali ya michuano hiyo itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Bandari imetinga hatua hiyo baada ya kuwafunga Simba mabao 2-1 katika mchezo wa nusu fainali ya kwanza uliochezwa mapema mchana huku Mbao FC ya jijini Mwanza ikikubali kuchapwa penalti 6-5 na wababe wa Yanga, Kariobang Sharks kwenye mchezo wa nusu fainali ya pili.

Wageni hao walilazimika kusubiri hadi hatua ya penalti baada ya dakika 90 za kawaida kumalizika wakiwa sare ya bila kufungana.

Kwa matokeo hayo sasa, timu za Tanzania zilizobakia katika mashindano hayo, ambazo ni Simba na Mbao zitakutana katika mechi ya kuwania mshindi wa tatu itakayotangulia kesho mchana.

Simba imeungana na watani zao Yanga kwa kuondoka mapema katika mashindano hayo yanayoandaliwa na wadhamini wao, Kampuni ya Kubashiri Matokeo Michezoni ya SportPesa.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, jana walipewa nafasi kubwa ya kushinda mchezo huo lakini makosa ya wachezaji wake yaliwagharimu na kujikuta wakifungwa na timu hiyo inayomilikiwa na Bandari ya Kenya.

Wenyeji hao walikuwa wa kwanza kufunga kupitia kwa Mnyarwanda, Meddie Kagere dakika ya 44 kwa shuti kali akiwa ndani ya eneo la hatari na kuifanya timu hiyo kwenda mapumziko wakiwa mbele kwa bao 1-0.

Hata hivyo tangu kuanza kwa mchezo, Bandari inayofundishwa na mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Ben Mwalala walionekana kuwa watulivu na kuwasoma wapinzani wao.

Kipindi cha pili pamoja na Simba kufanya mabadiliko kwa kuwatoa Juuko Mursheed, Hassan Dilunga na nafasi zao kuchukuliwa na Pascal Wawa na Emmanuel Okwi, bado walikosa umakini wa kuipita ngome ya Bandari.

Dakika ya 61, William Wadri aliisawazishia Bandari bao kwa mkwaju wa penalti iliyotokana na Muzamiru Yassin ambaye nafasi yake ilichukuliwa na Jonas Mkude kumchezea vibaya mshambuliaji wa Bandari ndani ya eneo la hatari na mwamuzi kuamuru adhabu hiyo.

Simba iliendelea kumiliki mpira na kupanga mashambulizi lakini ubovu wa pasi za mwisho za viungo wake na mabeki wa pembeni ziliwanyima washambuliaji wake, Kagere na Okwi kukwamisha mpira wavuni.

Wakati Simba ikiendelea kuliandama lango la Bandari, walijikuta wakishambuliwa ghafla na kupelekea wageni kupata bao la pili dakika ya 78 lililowanyong'onyesha mashabiki wa Simba.

Matokeo hayo yameendelea kuwa mkosi kwa timu kongwe za Tanzania ambapo Simba na Yanga mara mbili mfululizo wameshuhudia Gor Mahia ikitwaa ubingwa wa michuano hiyo.

# Kakolanya asema kitaeleweka Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

GOLIKIPA wa Yanga, Beno Kakolanya ambaye yuko katika mgogoro na kocha wa timu hiyo, Mwinyi Zahera amesema hawezi kuweka wazi suala lake lilivyofikia kwa sababu linafanyiwa kazi na mwanasheria wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kakolanya alisema alijaribu kutumia njia za kawaida kulimaliza sakata hilo lakini ilishindikana na kulazimika kumtumia mwanasheria wake ili kujua hatima yake ndani ya Yanga.

"Kiukweli kwa sasa siwezi kuzungumza lolote juu ya sakata hili, mwanasheria wangu ndio amebeba jukumu la kulimaliza jambo hili", alisema Kakolanya ambaye alikuwa kipa chaguo la kwanza la timu hiyo inayoongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema kuwa suala la kuendelea kuitumikia klabu hiyo au vinginevyo litategemea na mazungumzo ya pande mbili yatakavyofikiwa. Kakolanya amekuwa nje ya kikosi cha Yanga tangu Oktoba mwaka jana lakini akiwa mmoja wa wachezaji wa Timu ya Taifa " Taifa Stars" waliokwenda kucheza mechi ya ugenini dhidi ya Lesotho.

Mara kadhaa Zahera amesisitiza kuwa hatabadili msimamo wake licha ya wadau mbalimbali kumtaka amsamehe kipa huyo ambaye aliamua kutoonekana katika kikosi hicho kwa kushinikiza kulipwa madai yake ya malimbikizo ya mishahara.

Zahera, alisema pia itakuwa ni ajabu kukubali kufanya kazi na kipa huyo wakati meneja wake ni mmoja wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, ambao ni wapinzani wao wakuu hapa nchini. Kwa sasa Zahera anamtumia mlinda mlango, Clatous Kindoki raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kama golikipa namba moja huku akisaidiana na kipa chipukizi, Ramadhani Kabwili.

Kikosi cha Yanga kwa sasa kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi yake ya Kombe la FA dhidi ya Biashara United itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >